# Makao Ya Baadaye Ya Bwana Arusi Wa Mbinguni Na Bibi-arusi Wa Duniani

Jeffersonville, Indiana, USA
Agosti 02, 1964

1 Hebu na tuendelee kusimama kwa dakika moja, tunapoinamisha mioyo yetu sasa mbele za Mungu.

Baba yetu wa Mbinguni, kwa kweli tunashukuru kwa ajili ya majaliwa ya kuwa hapa leo, tumekusanyika pamoja katika Jina la Bwana Yesu. Tunaomba utusamehe dhambi zetu, na tunapokuwa hapa kuelekeza usikivu wetu kwenye mambo ya Milele na Uzima ulio juu ya mwili huu upatikanao na mauti. Sasa tunaomba ya kwamba utatupa maagizo Yako, ya namna ambavyo inatupasa kugeuka, yale yatupasayo kutenda katika siku za usoni, na hata wakati huu sasa, kupata mahali pale ambapo tume … tumekwisha ahidiwa.

Kuna wengi walio wagonjwa na wahitaji nchini, nao hawajakamilisha safari yao. Na adui wetu mkuu, si adui wetu tu, bali adui Wako, amekuja kuwazingira na ku—na kuyakomesha maisha yao, na kuwapeleka kwenye ma—kaburi la mapema. Nasi tunawaombea, leo, ya kwamba Wewe na rehema Zako na neema, Bwana, utaongeza siku zao kwa wakati uliowekwa.

2 Wakiwa wamelala jukwaani, ama mimbarani, hapa kuna leso na vifurushi. Na huko nje kwenye kumbi na kuzunguka mahali kote hapa, ni hao kwenye vitanda, machela, wagonjwa na wanaoteseka, wamesimama kwenye umati wakiwa hawana nguvu za kutosha kusimama.

Ee Mungu wa Milele, Mbarikiwa, jalia usikie maombi yetu asubuhi ya leo, kupitia kwa Damu ya Bwana Yesu; Hatuangalii uovu wetu, bali tukijua ya kwamba Yeye alisimama mahali petu, Naye Ndiye anayetuwakilisha kwa ajili ya maombi haya. Jalia kila mmoja na kila mtu aponywe kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana.

Bariki leso hizi. Wakati zitakapowekwa juu ya wagonjwa, jalia wapate kupona.

Na sasa, Baba, huku tukingojea ibada kuu ya uponyaji, tunaamini itafuata, tupasulie njia ya Uzima, Bwana, tupate kujua kupitia Neno Lako yale tupasayo kufanya. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

3 Kama kawaida, hii inahesabiwa kuwa moja ya majaliwa yangu makuu, ni kuwa katika nyumba ya Mungu na kuzungumza na watu Wake. Na sasa najua watu wamesongamana sana, nami nina somo refu sana. Kwa hiyo ninaninii … Ni—ninatumaini ya kwamba—ya kwamba mtakaa vizuri, kadri mwezavyo kuwa, mpaka tutakapomaliza Ujumbe.

4 Sasa, kuna joto, bali tunashukuru kwa ajili ya kiyoyozi. Lakini, kundi la ukubwa huu, hakuna kiyoyozi kingeweza kulishughulikia, mnaona, kwa sababu mwili wako mwenyewe ni mtambo, kama nyuzi tisini na nane, na daima unatoa joto, na kuketi karibu pamoja kwa kusongamana. Lakini na—natumaini ya kwamba Mungu atawafanya vizuri sana awezavyo.

5 Na wakati tunapokuwa ndani, tunapofanya mikutano kama huu, si—nisingewafanya mje hapa, kwa vyovyote vile, kama sikufikiri ilikuwa na kwa ajili ya kuwasaidia, kama sikufikiri ya kwamba ilikuwa inawafaa , na kwamba mngefaidika nayo, kwa kuja. Na kisha, tukijua pia ya kwamba hatuna muda mrefu zaidi wa kufanya jambo hili, ya kwamba tuna—tunakuja kwenye—kwenye saa za mwisho kabisa, nami ni—ninataka kufanya kila wakati kuwa muhimu, kwamba naweza, kwa ajili ya Ufalme Wake. Na sasa ninatumaini ya kwamba Bwana Mungu atatubariki tunapokusanyika.

6 Nami nataka kuwapongeza, ya kwamba, jana nilikuwa nikienda mahali mbalimbali, huko nje nikiwaona baadhi ya wagonjwa na wanaoteseka, katika hoteli, nami nikakutana na baadhi ya mameneja juma hili, baadhi ya mikahawa. Mfano, nilikuwa huko kwenye Ranchi House juma hili, juu hapa, na meneja alikuwa akinipa mkono tulipoanza kutoka. Naye akasema, aliniita, "Ndugu Branham." Nilishangaa namna alivyonijua. Naye akasema …

Nikasema, "Wewe ndiwe meneja?"

Akasema, "Mimi ndiye mmiliki." Kwa hiyo basi akasema, "Naam, watu wako huwa wanakuja hapa kula, kutoka kule chini." Kasema, "Wao …"

Nami nikasema, "Vema, nadhani wanakusonga kupita kiasi."

Akasema, "Bwana, hilo ni moja ya kundi zuri sana la watu niliowahi kuona." Akasema, "Kwa kweli ni wazuri sana."

7 Nilienda kwenye hoteli moja jana, kumwona msichana niliyependa kuzungumza naye, baba yake na mama yake walikuwepo, nami ilinibidi kwenda kwa meneja ili nijue ni wapi—ninii … chumba walichokuwa.

Akasema, "Nawe ni Ndugu Branham?" Hiyo ni huko huko Oaks.

Nami nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Ninataka kukupa mkono." Yeye alisema … Alinitambulisha kwa mkewe; wanandoa wazuri sana. Walisema, "Kila mtu katika hoteli hii anahudhuria ibada zako. Tuliiweka kwa ajili yao." Kisha akasema, "Wateja wetu wengine wote tuliwakatalia."

Nami nikasema, "Vema, nakushukuru kwa ajili ya jambo hilo."

Akasema, "Ndugu Branham, moja ya kundi zuri sana la watu niliowahi kuwaona, ni watu wanaokuja hapa, wanaohudhuria mikutano yako."

8 Jana usiku nilimtembelea rafiki yangu, Bw. Becker hapa chini, nami daima nilipenda sambusa zake. Yeye ni ninii … Yeye, nilimjua nilipokuwa mvulana; nilimjua maisha yangu yote. Kulikuwako na wenzi wa ndoa walioketi pale kutoka kule chini kwenye—mahali pa kale, huko chini kwenye Hoteli ya Riverside kule chini. Kwa hiyo wao … Bwana Becker akasema, "Billy?"

Nikasema, "Ni kitu gani, Homer?" Tunajuana vizuri sana.

Yeye alisema, "Ninawalisha watu wako wote kule juu."

Yapata watu mia mbili, ama kitu kama hicho, kila Jumapili, hula kwenye Blue Boar. Na kila mahali niendako, ninasikia matamshi ya jinsi mlivyo wazuri.

Jamaa huyu alisema, "Huko chini kwenye—kule Riverview kule chini," kasema, "mahali hapo pote pemechukuliwa na watu wanaohudhuria mkutano." Kasema, "Kuna mamia ambao hawataweza kuingia."

9 Kwa hiyo, kuwa hivyo, kwangu mimi ninyi ni chumvi ya dunia. Ni—ninashukuru sana kujua ya kwamba nina majaliwa ya kuwahubiria watu ambao hata wenye dhambi na watu … Sisemi watu hawa ni wenye dhambi, bali ninamaanisha watu ambao, biashara na kadhalika, ambao wanaweza kusema ya kwamba ninyi ni watu wazuri, nao wanawathamini katika biashara zao, karibu na sehemu zao. Unajua, hiyo ni kukolea chumvi. Ninathamini jambo hilo, tabia yako, jinsi unavyoshughulikia mambo.

Daima nimesema, "Kama mtu akiingia na hana, hana pesa za kushughulikia bili yake, nipigie tu." Mnaona? Nikasema, "Tutashuhgulikia jambo hilo." Nami nikasema, "Walisheni daima, kama wana pesa ama hawana." Mnaona, kila kitu kinaweza kufanywa.

Ninajisikia ninyi ni watoto wangu. Ninyi ni—ninyi ni nyota ambazo mimi … Kama nikiwahi kuwa na moja nitakapofika kule, mtakuwa hicho kito cha thamani, kinachong'aa sana, katika—katika taji ya huduma yangu. Wakati utakapovikwa taji, utakuwa ndio kito hicho.

10 Nami nimekuwa nikiwaambia, katika nyakati zilizopita, kuhusu ile Mihuri Saba, Nyakati za Kanisa, na mambo ambayo—ambayo yamekuwa yakitendeka.

Na sasa, asubuhi ya leo, nina somo muhimu sana. Kwangu mimi, ni la baraka sana. Natumaini itawagusa vivyo hivyo. Na kama ningaliweza tu kuutoa katika uvuvio nilioupokea, uwe mzuri sana, lakini hiyo itakuwa juu ya Mungu kufanya jambo hilo.

11 Nimekuwa nikiwaambia kuhusu mahali na yale yanayotendeka, nasi tunaona mambo haya yote yakitukia.

Sasa ninazungumza, asubuhi ya leo, juu ya: Makao ya Baadaye ya Bwana Arusi wa Mbinguni Na Bibi -arusi wa Duniani, ambapo wataishi. Na, kwa kuwa, ninatumaini ya kwamba kwa neema ya Mungu sisi sote ni sehemu ya uchumi mkuu wa Mungu.

12 Na sasa na—natumaini ya kwamba mtanivumilia, kuwa na Biblia zenu, penseli zenu, ama cho chote mfanyacho kusoma pamoja nami, maana nitarejea kwenye Maandiko mengi. Kujaribu kumaliza kwa wakati wa kutosha kuwaombea wagonjwa; nami niliahidi jambo hilo. Njoni ndani, kuomba kwa ajili ya kitambo kidogo cha mwisho, katika vyumba na kila mahali, kwa wale ambao wako karibu wanyonge na hawana matumaini.

Na, Bwana akipenda, labda nitakuwa na ibada nyingine tarehe kumi na sita, labda tu kuwaombea wagonjwa.

13 Naanza likizo yangu sasa. Tangu Januari iliyopita, nimekuwa nikisafiri, nami ninarudi hapa. Nitakuwa. Ninaipeleka familia yangu huko Tucson asubuhi, kisha nitarudi kutumia wakati fulani hapa Kentucky, pamoja na baadhi ya marafiki zangu, kuwinda, na kuwinda kindi, kwa majuma kadhaa, ama labda saba ama nane, siku kumi, cho chote kile, isipokuwa Bwana aniongoze mahali pengine. Kamwe sijui, mahali utakapokuwa; kamwe hatujui jambo hilo, kwa sababu hilo liko mikononi mwa Mungu, Mungu peke yake.

14 Sasa kwa ajili ya somo hili kuu, sisi—sisi … Nadhani, kama ningechukua wakati wangu kwa jambo hili, kwa sababu inakubidi kuleta mambo mengi, ingechukua majuma. Lakini nimeandika Maandiko machache,

mihtasari michache, kusudi tu nilenge mambo muhimu ya jambo hilo, ambapo itawaacha msome.

Halafu hivi karibuni, labda, Bwana akipenda, mnamo Oktoba, sijui ni lini, lakini wakati wo wote atakaponiruhusu, ningetaka kuwa na—na siku chache, mkutano tu wa kawaida, kwenye sura ya 12 ya Ufunuo, kuinganisha na hii hapa. Loo, ninaamini ingekuwa ni jambo kuu. Ingekuwa tu. Ingekuwa ni furaha kuona jinsi Yeye alivyofanya.

15 Halafu, sisi tukiwa pamoja sasa, nilisema jana usiku, nilisema, "Mwajua, wakati mimi …" Asubuhi, kama vile kila asubuhi, nafikiri, "Nitakaposhuka kuja hapa, nitamtambua kila mmoja wa rafiki zangu aliyepo." Sasa nitafanyaje jambo hilo?

Kuwa pamoja nami hapa, kama rafiki yangu mzuri, Daktari Lee Vayle anayeketi nyuma hapa, mke wake mzuri na binti. Na Ndugu Roy Borders, na, nafikiri, Ndugu Ruddell, Ndugu Beeler, na Ndugu Palmer, na Ndugu Jackson. Na, loo, jamani, ninii—ninii … Hao ndugu wapendwa kutoka sehemu zote mbalimbali! Ndugu Anthony Milano, na, loo, kila mahali unapoangalia, unamwona ndugu mwingine! Kutoka huko chini Arkansas, siwezi kukumbuka jina lao; Ndugu John, Ndugu Earl Martin, na Ndugu Blair. Na, loo, kuna ninii tu … wewe … Haina mwisho, mnaona. Nina furaha sana kuwa na kundi kama hilo lililonizunguka wakati ninapofundisha juu ya Neno la Mungu, watu ambao nadhani ni watu hodari, watu halisi wa Mungu.

16 Ninashukuru kwa ajili ya maskani hii ndogo. Ninashukuru kwa milango yake mitano iliyo wazi kwa umma. Kila mlango … Tuna mashemasi wanne hapa, watu waliojazwa na Roho; wadhamini wanne, watu waliojazwa na Roho. Hao ni wawili kila mlango. Na ina milango miwili mbele, kwa ajili ya wachungaji wawili, wachungaji.

Tunafurahi kuwa nanyi; ninamshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hili. Yeye na awabariki daima.

17 Sasa tunataka kusimama kwa muda kidogo tu, tunaposoma kutoka katika Petro wa Pili sura ya 3, na pia kutoka kwenye Kitabu cha Ufunuo 21.

Tunaposimama, Ee Bwana, jaza mioyo yetu kwa furaha kwa sababu ya kusoma Neno Lako, tukijua ya kwamba Yesu amesema, ya kwamba, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Jua tena ya kwamba Yeye alisema, "Maandiko yote hayana budi kutimizwa." Na tunaposoma mambo haya, jalia tuwe na ufahamu kutoka Kwako, saa tunayoishi. Tunaomba katika Jina la Yesu, Mwandishi wa Kitabu. Amina.

18 Petro 3.

*Wapenzi, waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi; katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa namna ya ukumbusho.*

*Mpate kuyakumbuka maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na amri zetu sisi mitume wa Bwana na Mwokozi;*

*Tukijua jambo hili kwanza, ya kwamba siku za mwisho watakuja wenye kudhihaki, wakifuata tamaa zao wenyewe,*

*Na kusema, Iko wapi ahadi ya kuja kwake? (Kama hilo halikutani na mwanamke huyu kafiri katika …) … tangu baba zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa.*

*Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji, kwa neno la Mungu;*

*Kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.*

*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.*

*Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.*

*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*

*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika . . . siku hiyo mbingu zitatoweka kwa . . . mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*

*Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa,*

*Mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka?*

*Lakini, kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.*

*Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa tunatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane ... katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake.*

*Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi ... Paulo ... alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa;*

*Vile vile kama katika nyaraka zake zote pia ... akitoa humo habari za mambo hayo; ... katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama—- vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe.*

*Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa ... na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.*

*Lakini, kueni katika neema,…katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele. Amina.*

19 Sasa katika U—Ufunuo wa Kristo, katika mlango wa 21, nilisoma Maneno haya.

*Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita; wala hakukuwako na bahari tena.*

*Nami Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*

*Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na mwanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, na kuwa Mungu wao.*

*Naye Mungu atafuta kila chozi katika macho yao; wala mauti haitakuwapo tena; wala kuomboleza, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*

*Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya ... Akaniambia, Andika: kwa kuwa maneno hayo ni amini na kweli.*

*Akaniambia, Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi za maji ya uzima bure.*

*Yeye ashindaye atayarithi mambo yote, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. Hebu na tuombe tena.*

20 Bwana Yesu, tukiwa na ahadi kama hiyo na usemi mkali kama huo ambao Yesu Mwenyewe pamoja na yule mtume ametutolea kuhusu ile saa tunayokaribia, tupe, Ee Bwana, yahusuyo mwelekeo Wako, tupate kujua namna ya kuendea jambo hilo katika njia iliyo sahihi. Kwa sababu, inakuja, tunajua. Maandiko hayana budi kutimizwa, na ndivyo itakavyokuwa. Na sasa, Bwana, tunaomba rehema Yako tena juu yetu sote, tunapojifunza Neno Lako. Uwe pamoja nasi na utufunulie, Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

21 Sasa, sijui kama kungekuwako na njia ambayo labda, labda wangeweza kuzima taa kwenye ukumbi wa mikutano, na kuziacha tu jukwaani hapa, jambo ambalo labda lingekuwa bora zaidi, na kupunguza umeme kidogo. Karibu tuunguze mtambo wa kurekebisha nguvu za umeme, usiku wa juzi. Na kama mlinzii atatufanyia jambo hilo kwa ajili yetu, tungefurahia kuzimwa taa za chini, taa za ukumbi, zizimwe. Na halafu nafikiri mtakuwa na nafasi kubwa ya kuona, kuandika.

22 Sasa, somo tena, kulitangaza, ya kwamba tunakaribia ninii—somo la: Makao Yajayo Ya Bwana Arusi Wa Mbinguni Na Bibi -arusi Wa Duniani.

Sasa kama ilivyokuwa … Itanibidi tu kufanya jambo hili. Hapa kuna joto sana, mnaona. Naam, bwana. Tunapo … Ninajua mke wangu hapendi nifanye hivyo; lakini, hilo, nivue koti langu. Hapa kuna joto sana. Mnaona, Mna hewa huko nje, na imezuiwa tu kwenye kizimba kidogo hapa, mnaona. Sasa, katika—katika siku za usoni, ama …

23 Katika siku za nyuma, hasa, tumejifunza ile Mihuri Saba, Makanisa Saba. Ndugu Vayle na hao wengine wanashughulikia hayo sasa, kwa uaminifu, kuyaweka katika kitabu.

24 Na nikiona mambo haya yote ya ajabu ambayo tumeona yakitimia, ndipo nafikiri, baada ya kufahamu jambo hilo, katika saa tunayoishi, na mahali hapa; hakuna mtu ambaye angetaka kuketi chini kwa busara sana na kuchunguza yale yaliyonenwa, na yale yaliyoahidiwa kutukia, na yale yaliyotukia, ila ambaye angeweza kusema ya kwamba mambo hayo yametimizwa. Mnaona? Kile hasa Mungu alichosema angefanya, Yeye alikifanya sawasawa kabisa. Mnaona?

25 Sasa, nafikiri katika jambo hili, ya kwamba, bila kujua ni wakati gani ambao Bwana Yesu angeweza kutokea, nilifikiri ingekuwa ni vizuri, ilionekana kumpendeza Roho Mtakatifu kwamba tungezungumza juu ya jambo hili, basi; na labda nirudi tena, mara mbili ama tatu, kwa sababu sitakuwa na wakati wa kutosha kutoa haya yote.

Kama vile ambapo unaligusia so—somo ambalo huenda likawa linamkwaza kidogo mtu fulani, huwezi kuliendeleza lote hadi kulifanya dhahiri, ndipo unarudi tena kushika somo linalofuata.

Na halafu baadaye, katika … Bwana akipenda, tunaingia kwenye ile mihuri ya 12, ama la … Samahani. Sura ya 12 ya Ufunuo, ambayo iko kati ya Kuja kwa Bwana na mwisho wa Baragumu, na kadhalika. Tutajaribu kurudisha hilo, kuonyesha kwamba Shetani ni nani, na kile alichofanya, alikotoka, kusudi lake ni nini, na jinsi ambavyo uzuri wake mkuu aliopewa ulisababisha kuanguka kwake. Udanganyifu wake ulisababisha kuanguka kwake; uzuri.

26 Halafu, namna isivyowezekana kwa mtu yeyote anayetaka kuangalia hilo kwa usahihi,huo "uzao" wa nyoka. Ningetoa changamoto kwa hilo, kwa mtu yeyote, mnaona, ambaye angetaka kuliangalia, kwa—kwa ufahamu wa kawaida kabisa. Mtoto anaweza kuliona. Mnaona? Sasa, nasi tutafikia jambo hilo baadaye.

27 Sasa, tunafahamu hapa ya kwamba Maandiko haya mawili … Sababu ya mimi kusoma Petro wa Pili sura ya 3, na kuilinganisha na Ufunuo 21, wote wawili hapa wanazungumza somo lile lile, lakini Yohana kamwe—kamwe hakuandika kama Petro alivyofanya. Mnaona? Tunafahamu ya kwamba Makao haya makuu ya Bibi -arusi yatakuwa hapa duniani.

Na sasa kama ukisoma, kama tu sura ya 21, sura ya 21 ya Ufunuo, mtume hapa alisema, ama nabii alisema, ya kwamba, "Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya." Inasikika kana kwamba kuna kuja maangamizi.

28 Sasa, jinsi ninavyopata Ujumbe wangu daima ni kwa maombi. Nitakuwa nimeketi katika maombi na kitu fulani kinanifunulia. Nami ninalingojea kwa dakika chache na kuona kama ni kweli, ndipo ninasikia likija karibu zaidi. Na halafu wakati mwingine ninaendelea kungojea mpaka ono linatokea. Lakini linapoanza kuja, nami nimeridhika linatoka kwa Mungu, ndipo ninaenda kwenye Maandiko. Mnaona, Hiyo ni, inapaswa kuwa ni thibitisho la kila kitu cha kiroho kinachofanyika, kwa sababu Biblia ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo; unaona, ni Mwili Wake.

Na sasa, katika jambo hilo, labda ninapata mahali katika Maandiko ambayo hapasikiki tu sawa, nami nitashangaa. Ninarudi tena kwenye maombi. Linakuja tena. Ndipo mimi—ndipo ninaanza ku—kuyachunguza Maandiko yangu.

29 Sasa, Biblia yetu imeandikwa katika Kiingereza, na maneno ya Kiingereza hubadilika, wakati wote. Kwa mfano, kama vile Yohana Mtakatifu 14, alivyosema, "Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi," makao katika nyumba. Vema, basi, wewe, kile unachofanya na jambo hilo basi, ni kulirudisha kwenye—kwenye lile la asili na kuona kile Yakobo alimaanisha, ama kurudi kwenye Kiebrania, ama kwa Kiyunani, kutoka kwenye tafsiri ya kwanza. Na ndani humo inasema, "Katika Ufalme wa Baba Yangu kuna majumba mengi ya kifalme." Vema, basi, unarudi kwenye wakati ambapo watafsiri walitafsiri kwa ajili ya Mfalme James, ule ufalme uliitwa, katika Kiingereza, "nyumba," na mfalme alikuwa ndiye baba wa wajumbe wake. Hiyo ndiyo sababu wao walitafsiri, "Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi." Mnaona? Na halafu unapata maneno hayo na inakubidi kuyatafuta.

30 Halafu, unaona, kutokana na uvuvio huo … Mimbara hii asubuhi ya leo, nasema, hakuna hata wakati mmoja imewahi kuwa kitu ila moja kwa moja, Maandiko. Hivyo ndivyo Uzao wa Nyoka na mambo haya mengine yote yanavyokuja. Mnaona? Kwa …

Na ni, kweli, kama jamaa fulani angesoma tu na kusema, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi," kama husimama ukachunguza, kuomba, ungechanganyikiwa kabisa. Mnaona? Lakini endeleeni tu kuomba. Mungu daima hulifanya sawa, kama linatoka kwa Mungu.

31 Sasa, Yohana anaelezea badiliko na ninii … namna linavyokuja … Yeye haelezi jambo hilo, hasa, bali Petro analifafanua. Yohana alisema tu, "Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya; mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zilikuwa zimepita. Hakukuwako na bahari tena. Mimi Yohana niliona ule Mji mtakatifu ukishuka kutoka kwa Mungu Mbinguni, umewekwa tayari kama Bibi -arusi aliyepambwa kwa ajili ya Mumewe."

Lakini, tunarudi kwa Petro wa Pili sasa kuona, Petro anaeleza jinsi utaratibu huu utakavyotukia. Sasa, kama ungeangalia yale Yohana aliyosema, inasikika kama, "Kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita," zimeangamizwa. Mnaona, basi, hilo linasikika la ajabu sana. Kwa hiyo hilo ndilo lililonigusa, nami nikaanza kutafuta neno, "kupita." Na, sasa, lakini ni dhahiri ya kwamba wote hawa, mtume na nabii, walikuwa wakinena juu ya jambo lile lile.

32 Na sasa, pia, katika Kitabu cha Isaya, sasa, ya kwamba mnataka kuyaandika Maandiko haya, katika Isaya 65:17. Isaya, akinena juu ya ule Utawala wa Miaka Elfu, hiyo miaka elfu ya raha kwa—kwa ajili ya watu wa Mungu. Isaya alinena habari zake, naye akasema, "Mimi … Kulikuwa na … Mambo yote ya kale yamekwishapita," na jinsi watakavyojenga nyumba, kukaa ndani yake. Kama tungalikuwa na wakati … Labda tunachukua muda tu na—na kusoma hili kwa dakika moja tu, Isaya 65, na hebu tusome tu kwa dakika chache hapa. Na hili hapa, sahihi, kwa ajili yetu. Sasa, kwa kuanza, Isaya 65:17.

> *Na tazama, mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya.*

Sasa, Isaya, nabii, alikuwa mmoja wa manabii walioandika Biblia nzima hasa katika unabii wake. Yeye anaanza na uumbaji; katikati ya Kitabu chake, yapata sura ya 40, anakuja karibu na Yohana Mbatizaji, Agano Jipya; na anaishia hapa, katika Kitabu chake, katika Ufunuo, katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Kuna vitabu sitini na sita katika Biblia, na kuna sura sitini na sita katika Isaya. Aliandika maelezo kamili.

Sasa, tunaona, hapa sasa anapata sura ya 65, sura moja zaidi, naye anazungumza juu ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Angalia jambo hilo, namna lilivyo zuri.

> *…tazama, mimi naumba mbingu mpya na…nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni. (Hilo ni "yatapita.")*
>
> *Lakini fu—furahini, mkashangilie daima,…hata kwa ajili ya hivi ambayo nimekwishaumba; maana, tazama, naumba Yerusalemu uwe wa shangwe, na watu wake wawe furaha.*
>
> *Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu wangu; sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, kwa kuwa…wala sauti ya kuomboleza.*
>
> *Hatakuwapo tena ... mtoto wa siku chache, na…wala mzee ambaye hajatimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa maiaka mia atalaaniwa. Ndipo ninii.…*
>
> *Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na watakula matunda yake.*
>
> *Nao hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; (hiyo ni kusema, shamba lako, mwanao analirithi, ama baadhi ya warithi wako)…hawatapanda, akala mtu mwingine kule; (wao wanapanda mimea yao wenyewe na kubaki humo; wana Uzima wa Milele)… maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu, na ninii zangu nyingi…na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi.*
>
> *Hawatajitaabisha kwa kazi bure, wala hawatazaa kwa taabu; kwa sababu wao ni wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na watoto wao pamoja nao.*

Sasa angalia, hapa ndipo nitakapofikia, baada ya kitambo kidogo.

> *Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, Mimi nitasikia.*
>
> *Mbwa-Mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja, na simba atakula majani kama ng'ombe;…mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka. Hawatadhuru ama kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema BWANA.*

33 Ni ahadi iliyoje, ya hawa manabii na wakuu wenye hekima, waalimu wa Biblia, huko nyuma kabisa katika siku za kale, wakiona Siku hii tukufu ikija!

Kwa vifungu hivi, mtu anaweza kuwazia, ama kuongozwa, hasa, kuamini ya kwamba sayari yote, ya dunia hii, itaangamizwa, "Ninafanya Mbingu Mpya na Nchi Mpya," mnaona, kwamba mbingu zitatoweka na dunia itakuwa imeondolewa, imeangamizwa kabisa. Lakini tukijifunza kwa makini, na kwa msaada wa Roho Mtakatifu, tunaweza kuona Ukweli wa jambo hili; na hilo ndilo tunaloendea.

34 Ni anga zinazoizunguka tu, na dhambi iliyo juu ya dunia, ambayo itaangamizwa. Mnaona? Sasa, tunatambua ya kwamba mbingu zinamaanisha "anga za juu." Mnaona?

35 Kunafanya nini? Wakati huo, michongoma hii, na magonjwai, na mauti, na siasa, na mwanamume mwenye dhambi, na mwanamke mwenye dhambi, na pepo wachafu, wote wataondolewa na kuangamizwa. Mnaona? Haina budi kufanywa hivyo, kwa sababu tutaishi papa hapa. Tutathibitisha jambo

hilo kwa Biblia. Papa hapa ndipo tutakapoishi. Sasa angalia, mbigiri, viini vya magonjwa, magonjwa yote na kadhalika, yataondolewa kabisa. Yote haya, uwepo wake ulioko duniani sasa, mifumo ya kujibunia, siasa, dhambi, kila namna ya pepo wachafu ambao wameuchafua ulimwengu, na mbingu zote zilizo juu yetu humu, zimechafuliwa na pepo wachafu. Sasa tutazama kwa kina na kwa muda mrefu, katika jambo hili, mnaona.

Yote haya yapo katika mbingu, ama katika anga, na dunia ambayo ni iliyoko sasa. Dunia hii inashikilia vitu hivyo, bali haikufanywa kwa kusudi hilo. Dhambi ilisababisha iwe hivyo. Mnaona? Ilifanywa na Mungu, Muumba. Lakini wote …

Na miili yetu yote, tunayoishi ndani yake sasa, iliwekwa duniani wakati Mungu alipoiumba, kwa sababu wewe umetoka katika mavumbi ya nchi. Yote iliwekwa nje hapa. Wakati Mungu Mwenyewe alipoiumba, ulikuwa katika mawazo Yake. Na ndani Yake, yulemkuu wa Milele, kulikuwako na wazo, ambalo ni sifa Yake.

Na sasa dhambi ilisababisha haya yote kutukia. Na Mungu, katika wakati huu, anakusanya zana Zake.

36 Shetani angali yupo hapa. Hiyo ndiyo sababu mambo haya yote yanatukia. Yeye yungali hapa, na majeshi yake yote maovu bado yako hapa. Angalia, hiyo ndiyo sababu dunia sasa ni chafu sana. Hiyo ndiyo sababu uchafu na mambo ya kipuuzi yanayoendelea; umwagaji damu, vita, siasa, dhambi, uzinzi, kila namna ya uchafu unaendelea, ni kwa sababu ya kwamba Shetani ndiye mtawala wa dunia hii na anga hili.

Unasema, "Anga- …?" Naam, bwana!

37 Mbingu na nchi sasa zimechafuliwa na pepo wanaoweza kutushtaki mbele za Mungu. Yesu yupo Kule kutuombea. Mnaona? Wakati washtaki wakiendelea kutunyoshea kidole, "walifanya hivi, walifanya hivi, walifanya hivi," lakini Damu ingali inafunika. Yeye alikuja kuwakomboa hao Wateule ambao alitangulia kuona. Hiyo ndiyo sababu ni chafu sana leo.

38 Hapa, mtume, katika Petro wa Pili hapa, sura ya 2, na ya 5 na ya … na aya ya 5 na ya 6. Naam, nimelipata. Yeye anarejea kwenye hatua tatu za dunia. Unaona, yeye—yeye anapata hatua zake tatu. Angalia jinsi anavyowaleta.

"Dunia ya kale ilitokea kutoka majini," sasa, hiyo ilikuwa dunia kabla ya gharika.

Sasa, ile iliopo, dunia ya sasa tunaoishi sasa, iliitwa "dunia."

"Dunia ya kale iliyotokea majini," Mwanzo 1:1. Sasa na "dunia" ambayo ipo sasa. Halafu basi, tena, yeye ananena juu ya nyingine, "dunia ijao," Nchi Mpya. Dunia tatu; hatua tatu za dunia.

39 Na tazama jinsi Mungu anavyoweka wazi mpango Wake wa ukombozi. Loo! jambo hili liliifurahisha nafsi yangu wakati nilipoliona, jinsi Yeye anavyotuwekea wazi hapa sasa mpango Wake wa ukombozi. Sasa linganisha kile tunachoona na macho yetu wenyewe. Kile ambacho Mungu amefanya kuukomboa ulimwengu Wake, Yeye amefanya mpango ule ule wa kuwakomboa watu Wake, kwa maana Mungu asiyebadilika habadiliki katika mipango Yake yo yote wala cho chote kile. Ni jambo la utukufu ulioje!

40 Jinsi alivyotuongoza Kwake, kwenye maskani ndani yetu, kwa hatua tatu za neema; kama tu vile Yeye alivyoongoza ulimwengu katika hatua tatu, kuja ulimwenguni. Kama vile Mungu atakavyokuja ulimwenguni baada ya kupitia katika hatua tatu mbalimbali za utakaso, hivyo ndivyo hasa Yeye anavyotujia kupitia hatua tatu za neema. Nilifundisha jambo hilo hapo mwanzo; Sijabadilika kamwe, tangu wakati huo. Ni Neno la Mungu.

41 Inakubidi kuweka tatu zako pamoja, saba zako, kumi na mbili zako. Hesabu za Biblia hazina budi kuwa kamilifu la sivyo utachanganya picha yako kabisa. Kama huwezi kuelewa jambo hilo, endelea tu kuomba. Angalia, litaingia moja kwa moja, sahihi kabisa. Mungu hukamilishwa katika utatu. Mnaona?

42 Angalia, "ile dunia ya kale," ile iliotangulia ile gharika; "dunia" iliopo sasa; na Ile ijayo.

Sasa, hatua ya kwanza ambayo Yeye anatuleta kwa … Unaona, mpango Wake wa ukombozi ni sawa kabisa kwa kila kitu. Yeye hutumia njia ile ile. Yeye habadiliki kamwe. Yeye alisema, katika Malaki 3, "Mimi ni Mungu, wala sibadiliki." Namna anavyofanya jambo hilo, kwa hiyo, kama alimwokoa mtu wa kwanza aliyepata kumwokoa, kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia, itambidi kumwokoa mwingine; na kila mtu atakayemwokoa itambidi kuwa vivyo hivyo.

Kama Yeye alimponya mtu wakati wo wote katika safari ya maisha; na iwe katika siku za Yesu, mitume, manabii, wakati wo wote ule; wakati masharti yale yale yanapotimizwa, hana budi kufanya hivyo tena. Hiyo ni kweli. Yeye habadiliki. Mwanadamu hubadilika, majira hubadilika, wakati hubadilika, vipindi hubadilika, bali Mungu anabaki vile vile. Yeye ni mkamilifu. Ni tumaini lililoje hilo linapaswa kuwapa watu

wagonjwa!

43 Kama Yeye alipata kumponya mtu, hana budi kufanya hivyo tena wakati hali zile zile zimetimizwa. Yeye aliwahi, aliwahi kumwokoa mtu, hana budi kufanya hivyo kwa misingi ile ile aliyofanya mara ya kwanza. Kama Yeye aliwahi kumjaza mtu kwa Roho Mtakatifu, hana budi kufanya hivyo kwa misingi ile ile aliyofanya mara ya kwanza. Kama aliwahi kumfufua mtu kutoka kaburini, hana budi kufanya hivyo mara ya pili, na kila wakati mwingine, kwa kanuni ile ile.

44 Yeye habadiliki. Loo, ni tumaini lililoje ambalo hunipa mimi! Ni kitu gani? Si katika nadharia fulani ya kujibunia, kitu ambacho makundi ya watu yamekusanyika pamoja; bali ni Neno Lake lisilobadilika.

Unasema, "Je! Ni Kweli?"

Yeye alisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli." "Kwa maana mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." "Maandiko yote yana pumzi ya Mungu, kwa hiyo ni mazuri na yanafaa kwa mafundisho." Na kumbukeni, ya kwamba, "Maandiko yote yatatimizwa," kila sehemu yake.

45 Angalia jinsi Mungu anavyolifanya dhahiri kwetu. Na kama hilo halikuwa thibitisho kuu—jema … baraka kuu, ya upendo kutoka kwa Mungu! Ninapoona jambo hili, na kuona ya kwamba tangu nilipokuwa mvulana, mara ya kwanza Kristo aliponishughulikia, bado daima nimefundisha hatua hizo tatu za neema. Angalia kama si kweli sasa.

46 Sasa, hatua ya kwanza ni "toba kwa Mungu." Na halafu kinachofuata baada ya jambo hilo, ni ubatizo wa maji, "ubatizo wa maji," "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Unaona, ubatizo wa maji hufuata, ikionyesha ya kwamba toba ilikuwa halisi. Ama, "kuondoa" dhambi zetu za zamani, hilo halina uhusiano wowote na dhambi ya baadaye. Inaondoa tu. "Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo." Kwa ajili gani? "Ondoleo." Kuondoa dhambi ya zamani hakuhusiani na wakati ujao. Ni kwamba tu, dhambi yako imekatiliwa mbali, yale uliyofanya.

Huwezi kutubu kwa yale Adamu aliyofanya. Kamwe hukufanya jambo hilo; Adamu alifanya hivyo. Unapata tu msamaha kwa yale uliyofanya. Tabia ya kale ingali pale.

47 Hebu nichukue ubao huu kwa dakika moja. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao — Mh.] Sasa, huu hapa moyo wa mwanadamu. Sasa, mimi si … Mimi niko mbali sana na kuwa mchoraji. Huu hapa moyo wa mwanadamu; na huu hapa moyo wa mwanadamu. Sasa, huyu hapa ana nyoka ndani yake, hiyo ni dhambi, huyu hapa ana uhai wake. Huyu hapa ana hua ndani yake, ambaye ni Roho Mtakatifu, hapa ana Uzima. Vema, huyu hapa, ana kijicho, chuki, wivu; Hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, ni jamaa huyu hapa. Vema, huyu hapa ana upendo, na furaha, na uvumilivu; na Hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, hapa chini.

Sasa, unapoombwa, ama umesamehewa dhambi zako, umefanya hili tu, umeondoa lile. Lakini kitu kilichokufanya ufanye hivyo bado kipo. Hicho ni shina la kale la uovu; ingali iko pale. Angalia, ndipo unatubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba Yeye alikusamehe dhambi zako. Angalia.

48 Halafu, pili, unakuja utakaso, ambao unaweka nia yetu katika utaratibu wa utakatifu, kuwaza sawasawa. Kuondolewa … utakaso ni neno la Kiyunani lenye maana mbili, ambalo linamaanisha "kilichosafishwa, na kuwekwa kando kwa ajili ya huduma."

Kisha, baadae, unakuja ubatizo wa Moto na Roho Mtakatifu, ili Mungu apate kuishi ndani yetu. Nao Moto wa Mungu husafisha mioyo yetu na dhambi, na kumweka Roho Mtakatifu ndani. Ndipo tunaleta Maisha yale yale Huyu aliyoishi, kwa sababu Huyo yumo ndani yetu.

49 Angalia, katika kuzaliwa kwa kawaida, wakati mwanamke anapojifungua mtoto. Maisha ya kawaida ni mfano wa maisha ya kiroho. Wakati mwanamke anapojifungua mtoto, yule wa kawaida, jambo la kwanza linalotendeka ni kuvuja maji, kisha damu, na ndipo roho (uhai). Unamnyakua jamaa huyo mdogo na kumpiga [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja — Mh.], Naye anaondoka, anapiga makelele. Maji, damu, roho.

Na sasa mtoto anapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, yeye huja vivyo hivyo: maji, Damu, Roho.

50 Sasa angalia, utakaso, hatua ya tatu … hatua yake ya pili, husafisha nia; huweka moyo, nia ya moyo, katika utaratibu wa utakatifu.

Mtu anaweza kutubu dhambi na bado anawazia … Vema, labda yeye ni m—mwanamume asiye mwadilifu, kila mwanamke anayeonekaa asiye mwadilifu, bado lingalipo. Labda yeye ni mlevi; kila wakati ana harufu ya hiyo ombe, bado lingalipo. Mnaona?

Lakini basi wakati anapotakaswa, hilo husafisha tamaa hiyo kutoka kwake. Mnaona? Huondolea mbali ile hamu yake. Yeye angali anaweza kujaribiwa, bali huondolea mbali ile hamu yake. Bado, yeye hayuko

sawa bado.

Halafu, yeye amebatizwa kwa Roho Mtakatifu na Moto. Amesafishwa, akaunguzwa, akasafishwa; na halafu akaingizwa katika utumishi wa Mungu.

Utakaso unawaweka tu kando kwa ajili ya huduma.

51 Na angalia jinsi hasa hilo lilivyokuja, jumbe zikija. Martin Luther, kuhesabiwa haki; John Wesley, kutakaswa; Wapentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Zile jumbe, hiyo ndiyo sababu hapawezi kuwapo na nyakati nyingine tena, mnaona. Tuko katika wakati wa mwisho. Hatua tatu. Ubatizo husafisha moyo kwa Roho Mtakatifu.

52 Ni jambo la kushangaza iliyoje sasa, Yeye anapachukua mahali ambapo tunapaswa kuishi, kupitia katika utaratibu ule ule.

Sasa, Yeye ameliita Kanisa kupitia kuhesabiwa haki, akaliita kupitia utakaso, kisha akalijaza kwa Roho Mtakatifu na Moto. Naye akalipitia kwa njia fulani, ili kwamba Yeye Mwenyewe, Roho Mtakatifu Mwenyewe, Mwana wa Mungu, angeweza kuishi katika moyo wa mwanadamu. Sasa, haina budi kupitia humo kabla Yeye hajaingia ndani Yake.

Angalia, Yeye aliufanya ulimwengu, ambapo huyo Bibi arusi ataenda kuishi ndani yake, vivyo hivyo, mpango Wake ule ule wa—wa wokovu.

53 Angalia ulimwengu uliotangulia gharika. Yeye, baada ya huo kutubu, kwa kupitia kwa Bibi -arusi wa siku hiyo, Nuhu, Yeye aliubatiza kwa maji, akaufunika kwa maji. Ndipo, kuhesabiwa haki, kuonyesha ya kwamba Yeye yuko njiani kuiita dunia hii iliyoanguka, kutoka Edeni, kurudi kwenye kurejeshwa kwake tena.

Ndipo Kristo akaja na kumwaga Damu Yake juu yake, akiitakasa na kuidai. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara kadha — Mh.] Mnaona, hiyo ndiyo dunia tunayoishi sasa.

Mnaona jinsi Shetani, hapa katika Maandiko, alivyojaribu kumfanya avunje mpango wa Mungu apate kuipokea, kumpa Yeye wakati alipomchukua mlimani, alijaribu kumpa Yeye hiyo alimpompeleka juu ya mlima, na kujaribu kumpa Yeye hiyo bila ya kununuliwa kwa Damu?

54 Je! Mliona namna Ibrahimu, wakati walipojaribu kumpa ile nchi, aliinunua kwa fedha nyingi sana, mbele ya watu, kama bendera, kama shahidi? "Na ijulikane leo ya kwamba nilinunua mahali hapa pa kuzikia." Mnaona, mnunue hiyo! Naye Shetani alijaribu ku—kumpa Yeye ufalme ambao ni wake sasa. Alijaribu kumpa Yeye kama zawadi, lakini asingeupokea. Kwa sababu ni, mnaona, basi Shetani bado angeweza kuudai. Lakini, ilibidi ununuliwe. Amina. Yeye alikuwa Neno katika utimilifu wake. Wasingeweza kumdanganya katika jambo hilo.

Basi, sasa huo utapata ubatizo wa Moto.

55 Mnaona, sasa ina … Ni kitu gani kilichotukia? Kristo alikuja na akaliita Kanisa kwenye toba, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya ondoleo; kulitakasa Kanisa; pamoja na Moto wa Mungu kushuka na kuteketeza uchafu wote, na kuja na kuishi katika moyo wa mwanadamu.

56 Sasa, dunia, kukombolewa kwa ajili ya mtu huyu aliyekombolewa, Yeye hutumia njia Yake ile ile. Yeye aliibatiza katika maji, baada ya yale maangamizi ya gharika. Akaimwaga Damu Yake juu yake, kuitakasa na kuidai. Ni Yake.

Shetani alijaribu kusema, "Nitakupa Wewe hiyo."

Akasema, "La, bwana, nitanunua." Hebu na iwe ni ushahidi. Yeye aliinuliwa juu, kama ishara, ya kwamba aliinunua. Aliinunua.

57 Lakini sasa haina budi kupitia ubatizo wa Moto, Moto mtakatifu kutoka kwa Mungu, unaosafisha dunia na mbingu zinazoizunguka. Halafu, imenunuliwa ili kwamba waliokombolewa waweze kuishi juu yake, waishi ndani yake kwa amani. Angalia, ubatizo wa Moto ni kuitakasa na dhambi, na magonjwa, na vijidudu vya magonjwa, kutoka kwa wenye dhambi, kutoka kwa ibilisi na kundi lake lote. Yeye lazima atupwe nje, katika Ziwa la Moto. Moto Mtakatifu kutoka kwa Mungu, unashuka kutoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, na kuiteketeza, angalia, kuifanya tayari kwa Mungu kukaa ndani yake. Kwa kuwa, Mungu, katika Ulimwengu Mpya utakaokuja, atakaa duniani. Maana, unasema, "Mungu, Yeye huishi katika moyo wa mwanadamu." Lakini, Yeye na Bibi -arusi wanakuwa Mmoja, nao wanaenda Nyumbani mwao katika Ulimwengu Mpya. Na mpango ule ule wa ukombozi unatumiwa kukomboa, wote wawili, ulimwengu na watu wanaoishi ndani yake.

58 Mnaona, moyo hauna budi kusafishwa namna hiyo. Kabla Mungu hajashuka katika utu wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Kristo akishuka na kuishi katika moyo wa mwanadamu, lazima kwanza utubu. Haina

budi kubatizwa kwa maji, katika Jina Lake, kuonyesha ni wa nani.

Ndipo haina budi kusafishwa kwa Damu ya Yesu.

Na halafu Moto mtakatifu na Roho Mtakatifu, kutoka kwa Mungu, hushuka na kuchoma tamaa zote za dhambi, maumbile yote ya ulimwengu. "Na kwa hiyo, yeye atendaye dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli …" Halafu, tena Biblia ilisema, "haiwezekani …" "Kwa kuwa, m—mtu aliyezaliwa na Mungu hawezi kutenda dhambi; hatendi dhambi." Hakuna njia kwake kutenda dhambi. Anawezaje kuwa mwenye dhambi, na aliyekombolewa, wakati uo huo? Ninawezaje kuwa ndani ya duka la rehani, na nje ya duka la rehani, wakati uo huo? Mnaona? Loo, Yeye alitukomboa kwa Damu Yake; kwa Roho Wake alitusafisha; halafu anakuja kukaa ndani yetu, Kanisa. Si madhehebu, sasa; Kanisa!

59 Angalia kwa makini sasa tunapochukua hili, mahali tunapopaswa ku—kukaa. Sasa, sasa, ile—ile toba iliyotangulia ile gharika, basi, ilileta ubatizo wa maji. Ndipo Kristo akaja na kumwaga Damu Yake juu yake, kuitakasa na kuidai. Na halafu inakuja, inayofuata, kuangamizwa kwa ulimwengu kama ilivyo sasa.

Dhambi zote zilizo mbinguni, "yeye ni mtawala wa nguvu za anga," yeye huzuia (kuzipiga) baraka kutoka kwa Mungu. Humo ndani huja ngurumo ya radi na kuipiga dunia, na kila kitu, kutoka mbinguni, mvua ya nyingi za barafu, na vimbunga, tuf- … tufani na kila kitu, "vinatoka juu," ambavyo ni Shetani, "mfalme wa nguvu za anga."

60 Angalia, angalia jinsi Shetani alivyojaribu kuichukua, kama nilivyosema dakika chache zilizopita, kwa kumpa Yesu bila kuinunua. Halafu, Shetani angali ana madai, kwa sababu imetiwa alama, mnaona. Lakini Yesu anainunua kwa Damu Yake iliyomwagika na kuirudisha kwa mwenye haki. Mnaona? Hivyo ndivyo alivyotununua, kwa Damu Yake, namna alivyolinunua Kanisa.

Na sasa ubatizo wake wa Moto unaisafisha na viini vyote, magonjwa yake yote, maradhi yote, hata mambo yote ya kiroho; ambayo ni kupitia kwetu, pia, inafanya vivyo hivyo; kuifanya iwe tayari kwa Mungu kukaa ndani yake, katika wakati huu mkuu unaokuja, ile Nchi Mpya. Mnaona, Yeye huikomboa kwa njia ile ile anayowafanyia watu Wake. Yeye huifanya yote iwe sawa tu, mpango Wake wa ukombozi. Kwa kuwa, Yeye ni Mungu asiyebadilika, daima ni yeye yule katika mipango Yake.

61 Namna nilivyowaambia, hapo awali, na kuwajulisha jambo hilo, na kwa nyakati zote, ya kwamba Mungu hawezi kubadilika; analifanya lijulikane, kila njia, na yeye yule.

Yeye aliujulisha, ujumbe Wake wa kwanza, katika ulimwengu uliotangulia gharika, kwa nabii Nuhu.

62 Nilikuwa nikizungumza na ndugu mpendwa ambaye ameketi pamoja nami sasa. Jana, alisema, "Jambo moja ulilosema, Ndugu Branham, hilo daima lilinitikisa."

Nikasema, "Ni kitu gani, ndugu?"

Naye akasema, "Hivi ndivyo ulivyosema," na ni kweli, "'Wachache, jinsi kundi dogo litakavyookolewa katika siku za Kuja.' Nasi tulizungumza juu ya jinsi Yesu alivyosema, 'Mlango ni mwembamba na njia imesonga, na ni wachache watakaoiona.' Sasa angalia, Biblia ilisema, 'Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kule Kuja.'"

Nikasema, "Ndugu, una ninii tu …"

Yeye alisema, "Kumbukeni, kuna watu wanane tu pale."

Nikasema, "Una nusu tu ya picha."

63 Hata hivyo, Nuhu alikuwa ni mfano wa wale waliosalia waliovushwa, si kundi lililobadilishwa. Henoko, mtu mmoja, alienda katika Kunyakuliwa kabla ya gharika kuja, akionyesha ya kwamba Kanisa haliingii kwenye ile dhiki wala cho chote kinachoizunguka. Henoko alibadilishwa, mtu mmoja. Loo, kanisa linaweza kuwa watu wengi; bali Bibi -arusi atakuwa ni kundi dogo sana litakalounda Bibi -arusi. Sasa, kanisa linaweza kuwa ni idadi kubwa ya watu; bali, Bibi -arusi, mnaona, linganisha wanane na mmoja. Watakuwa pungufu mara nane, ndiyo watakaokuwa Bibi -arusi, kuliko kanisa.

"Na kama wenye haki wakiokoka kwa shida, mwenye dhambi na asiyemcha Mungu wataonekana wapi," wale wanaojua vizuri zaidi, kufanya jambo hilo, na kuendelea na kulifanya hata hivyo? Wale wanaofuata kanuni za madhehebu badala ya Neno, wataonekana wapi, hata hivyo wanaitwa Wakristo, wakilichukua Jina la Kristo?

64 Sasa, kikamilifu, Nuhu alikuwa ni mfano wa wale waliovushwa. Kumbukeni, wakati Nuhu alipotoka, Hamu alikuwa pamoja naye. Dhambi ilikuwa ingali ndani mle. Dhambi iliendelea moja kwa moja, kupitia kwenye safina. Kutokuamini, shaka, iliingia kwenye safina, ikachukuliwa juu ya ile hukumu. Lakini Henoko alienda juu kuliko safina, alienda katika Uwepo wa Mungu. Lakini Nuhu alipitia na kutoka, na bado kulikuwa na dhambi; mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu, wa hali ya ulimwengu.

Utawala wa Miaka Elfu si mwisho wake. Bado kutakuwako na wakati baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Utawala wa Miaka Elfu ni kipindi cha wakati; bali, si ile Nchi Mpya. La, hasha. Angalia, katika jambo hilo, tutalifikia baada ya kitambo kidogo.

65 Unaona, dunia, iliyokombolewa, inamrudia Mwenyewe wa asili tena. Ilichukua … Aliichukua kutoka kwa Shetani. Yeye alivuta, akaitoa dunia kutoka kwa Shetani, kama tu vile alivyokuondoa kwa Shetani, kama vile alivyomtoa maskini yule mwanamke kisimani kutoka kwa Shetani. Huyo hapo kasisi alisimama, alidhani alikuwa pamoja na Mungu, naye hakuwa na kitu. Mnaona?

66 Ningependa kuwachorea hilo kwa muda kidogo tu. Sasa, tunataka kuliweka hili wazi kabisa, kwa hiyo sasa angalieni kwa makini sasa juu ya mafundisho haya. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao, kwa ajili ya aya chache zifuatazo — Mh.]

Sasa, huyu hapa, huyu hapa ni Mungu. Mungu, ambaye ni wa Milele, bila … Hakuna mwingine ila Yeye. Lakini, katika Mungu, Yeye alikuwa na sifa. Sasa, hii hapa inawakilisha Neno, Neno la Mungu, ambalo lilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu katika utu wa Yesu.

Sasa huyu hapa, jamaa huyu hapa, tutamfanya hivi. Sasa, huyu anaitwa mwanamke kisimani. Huyu ni kuhani, Farisayo. Na mahali unapoona hili, ubao wazi, inamaanisha neema na wokovu.

67 Sasa, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Zile hatua tatu. Ilikuwa ni sifa kwanza, ilikuwa ndani ya Mungu, kwamba Yeye alijifikiria kama mwanadamu; na hilo lilimpeleka kuwa Yesu; na sasa, kama utapata kuwa Mle, ulikuwa pamoja Naye wakati huo. Kwa kuwa, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, huo ni Mungu; nawe ulipaswa kuwa sehemu ya Mungu hapo mwanzo, si kile ulichochagua chini hapa. Yeye alikuchagua. "Wote alionipa Baba watakuja."

68 Sasa mwangalieni kuhani huyu hapa. Tunaona sehemu yake ya chini, hapa, maisha yake ya nyuma, nyuma huku nyuma yake, kuchaguliwa kwake tangu zamani nyuma hapa, ni dhambi.

Hii hapa kuzimu, chini hapa.

Sasa, sehemu hii ndogo hapa, inayoonekana kama ubao, ambayo inawakilisha usafi wake. Alikuwa kuhani. Yeye alikuwa mtu mwenye heshima. Hiyo iliwakilisha hii. Yeye alikuwa, pia, ilibidi awe mtu mzuri, la sivyo asingeweza kuwa kuhani. Lakini unaona jinsi alivyolipata hilo, ilikuwa ni elimu ya kiakili.

69 Sasa, maskini mwanamke huyu, maisha yake ya kwanza, hapa juu, yeye alikuwa ni kahaba, alikuwa ameharibiwa kabisa. Lakini kule chini kabisa ndani yake, hapa, kulikuwa na ufahamu kidogo tu. "Najua Masihi atakapokuja …" Mnaona? Mnaona, hiyo ilikuwa pale.

Angalia, wakati Yesu alipokuja na kulidhihirisha Neno, kwa sababu Neno lilitambua mawazo yaliyokuwa moyoni; kama vile Waebrania 4 inavyosema itafanya, 4:12, kwamba angefanya hivyo. "Neno lilikuwa mtambuzi wa mawazo ya moyo," Naye alikuja kama Mwana wa Adamu, yule Nabii. Ni kitu gani kilichotukia? Kuhani huyu, mwenye elimu tu ya kiakili, alisema, "Ni ibilisi," kwa sababu hilo ndilo dhehebu lake lililiita. Ilifanya nini? Hakuwa na uwakilishi, kwa hiyo lilimtia giza.

70 Lakini maskini mwanamke huyu hakuwa na kitu cha kutoa; alikuwa mchafu na mchafu alivyoweza kuwa. Lakini, angalia, huko chini kabisa ndani yake, ana uwakilishi, unaona. Na, basi, yeye alikuwa akitazamia hili lifanywe mwili.

Na wakati aliposema, "Nenda kamwite mumeo uje naye hapa."

Akasema, "Bwana, sina yeyote."

Kasema, "Umesema kweli, maana una watano, na yule uliye naye sasa si wako. Umekuwa na watano. Hilo linafanya sita uliokuwa nao."

Akasema, "Bwana!" (Si, "Wewe ni," si, "Beelzebuli.") "Ninaona ya kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua Masihi, ambaye anaitwa Kristo, atakuja. Na wakati atakapokuja, Yeye atafanya jambo hili."

Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

Hakuna shaka tena. Haikukubidi kuelezea jambo hilo. Aliliona. Aliamini hilo. Akaondoka akaenda zake! Kwa nini? Hilo lilifanya nini kwake? Ilimkomboa.

Sasa angalia, Yeye alikuja kuwa Mkombozi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Kukomboa kunamaanisha nini? "Kurudisha." Kwa nini hakumpata kuhani? Yeye kamwe hakuwa huko juu. Mnaona? Mnaona, hakuwa na uwakilishi.

Yeye alikuja kukomboa kile kilichoanguka. Katika kule kuanguka, hili lilichafuliwa, pamoja na msichana huyo; bali Mungu alikuwa naye katika mawazo Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Naye alikuja kumtakasa. Mnaona? Kisha Yeye … Alikuwa na Uzima wa Milele. Mnaona?

71 Ambapo, yule kuhani, lilifanya nini kwake? Lilimrudisha moja kwa moja kwenye kikomo chake. Hakuwa na cho chote, cha kuanza, elimu ya kiakili tu.

Sasa sikiliza, rafiki, kama kitu pekee ulicho nacho ni kujifunza kiakili tu, unapata kitu tofauti na hicho. Na kamwe hutaweza kulipata Hilo isipokuwa uwe na uwakilishi. Hiyo ndiyo sababu ninaamini mnatoka mashariki na magharibi, kaskazini na kusini; Neno, likiwa hai, likidhihirishwa.

72 Angalia sasa jinsi anavyoijulisha njia Yake kwa manabii Wake, hapo mwanzo. Yeye kamwe hajaibadilisha.

[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … Wokovu. Yeye alimhesabia mtu haki; akamtakasa; Akamtuma Roho Mtakatifu na Moto, na kuiteketeza dhambi hiyo ndani yake, na akaishi ndani yake, Yeye Mwenyewe.

Yeye huifanya dunia, ambayo ataitumia katika mpango wa ukombozi, vivyo hivyo. Ilitubu na kubatizwa katika maji, katika … na Nuhu. Yesu alikuja akaitakasa, kwa kuinyunyizia Damu Yake, na kuidai. Na katika Nchi Mpya itakayokuja, itakuwa na ubatizo wa Moto mtakatifu, kuitakasa na kila pepo, kila kijidudu cha maradhi, kila ugonjwa, kila kitu kilichopo, na kuifanya upya. "Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya."

Unakuwa mtu mpya. Amina! Sio tu yule wa zamani aliyetiwa viraka, kwa kujiunga na kanisa ama kujaribu kufungua ukurasa mpya, bali wewe ni kitu kipya kabisa. Mungu humchukua mtu huyo wa kale na kumteketeza kabisa, kwa Roho Mtakatifu na Moto, na anakuja Mwenyewe, anatuma uwakilisho wako. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Mpango ule ule; njia ile ile.

73 Shetani alikuwa … ataondolewa duniani, kama tu vile Shetani alivyoondolewa kwako. Shetani hawezi kusumbua; ama, anaweza kumjaribu, bali hawezi kumpata Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Kwa kuwa, Mungu, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, alitangulia kumwona, na akamtuma Yesu kumkomboa, na Damu inanena kwa niaba yake. Anawezaje kutenda dhambi wakati haiwezi kuonekana, hata, na Mungu? Yeye hata … Kitu pekee anachosikia ni sauti yako. Yeye anaona uwakilisho wako. Amina! Hiyo ni kweli. Mnaona?

74 Kwa njia ile ile, kwa maana ulimwengu ni moja ya sifa Zake kama tu vile wewe ulivyo moja ya sifa Zake. Ulimwengu unakuwa moja ya sifa Zake, kwa sababu ilikuwa ni mawazo ya Mungu, hapo mwanzo. Kuwa na dunia, kuwa kwenye Kiti cha Enzi, kuwa Mfalme, kuwa Mkombozi, kuwa Mponyaji, hizo ni sifa Zake.

75 Ni kama tu sifa zako. Siwezi kusema ninii—"mhimili" isipokuwa nifikirie juu ya mhimili. Siwezi kusema "mtu" isipokuwa nimfikirie mtu. Na ninapowazia juu ya mtu, basi nasema "mtu," mawazo ni sifa yangu na kule kutamka ni neno. Mnaona?

Kama vile Isaya, angewezaje kusema, ya kwamba, "Bikira atachukua mimba"? Wazo ni nini?

76 Sasa, wengi wenu mnashangaa jinsi wao, huo utambuzi, unavyokuja. Nitawaambia. Mnaona, ni neno ninalosema. Wala si mawazo yangu, maana sijui. Sijui juu ya kuwazia jambo hilo. Ninawezaje kukwambia wewe ni nani na unatoka wapi, wakati mimi sikujui? Ninawezaje kukwambia yale uliyofanya miaka kumi iliyopita, wakati sijapata kukuona maishani mwangu? Ninawezaje kukwambia mahali utakapofanya na kile utakachofanya miaka kumi tangu sasa? Ninajuaje mambo ya usoni? Lakini ni mawazo ya Mtu mwingine.

"Iweni na nia ile ile ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristo. Hebu nia iliyokuwa ndani ya Kristo na iwe ndani yenu." Mnaona, basi si mawazo yako. Ni mawazo Yake, kupitia kwako. Nawe hutaeleza maneno yako mwenyewe; unatoa Maneno Yake.

77 Hivyo ndivyo ndugu wanavyochanganyikiwa mara nyingi, juu ya kufasiri lugha, na kadhalika. Mnaona, wanasema mambo ambayo si sahihi, hawatambui ya kwamba huyo ni Shetani. Unasema, "Katika bustani ya Mungu?" Ngojeni tu mpaka tutakapomaliza, tuone kama sivyo, ama la. Magugu na ngano hukua katika shamba lile lile. Yote kwa pamoja yanaishi kwa jua moja na mvua ile ile. Mnaona?

"Lakini kama kuna mmoja miongoni mwenu ambaye ni nabii, Mimi Bwana nitasema naye. Na kama yale anayosema yakitukia, basi huyo ni Mimi, unaona, maana yeye haelezi yake. Yeye anaelezea mawazo Yangu, sifa Zangu za mambo ambayo hayana budi kuja, nami nitatumia kinywa chake kuyaeleza. Na baada ya yeye kuyasema, hayana budi kutimia. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe."

Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba." Hilo latosha. Yeye atachukua mimba. Yale aliyosema Mungu, Yeye huyatenda.

78 Loo, kufanya yajulikane, kwa manabii Wake, madhihirisho Yake yote, kwa sababu ni sifa Zake za mawazo Yake yaliyotamkwa.

Sasa, hilo lilikuwa hapa, ndani ya maskini mwanamke huyu. Alikuwa mmoja wa sifa Zake. Mnaona?

Na kulikuwa na kuhani, akiwakilisha ile Nuru. Alikuwa amejifunza jambo hilo kutoka katika Biblia. Alikuwa amejifunza ya kwamba Mungu alikuwa Mungu. Alikuwa amejifunza ya kwamba utakatifu ulikuwa sahihi. Alijifunza kwamba kulikuwa na sheria ya Mungu. Alikuwa amejifunza hilo kwa sababu ya wazo la kiakili. Naye alizaliwa katika ukoo sahihi; alikuwa Mlawi. Bali aliijua tu kwa mawazo ya kiakili. Na wakati Nuru ya wakati huo … Mnaona, alijifunza kwa kile kilichokuwa kimetukia, si kile kilichokuwa kinakitukia; kile kilichokuwa kimetukia! Na wakati alipopata kile kilichokuwa kikitukia, dhehebu lake halikusema kitu juu ya jambo Hilo, kwa hiyo hakuwa na uwakilishi Wake.

79 Lakini hapa alikuwako Mkombozi duniani wakati huo, kukomboa sifa hizo za Mungu, naye aliipokea. Yeye hakulihoji hilo. Yeye alisema, "Masihi ajapo, Yeye atafanya jambo hili," na hilo lilitosha. Naye aliona jambo hilo likitendeka, kwa hiyo … Yeye alisema, "Mimi ni Masihi," kwa hiyo hilo lilitosha. Hakuna swali tena. Yeye alienda tu, akimwambia kila mtu mwingine, "Njoo, umwone Yeye niliyemwona."

80 Utaratibu huu hutufanya safi, hekalu kwa ajili ya makao Yake: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa Moto. Hilo huleta utakaso wa hekalu (letu) hili.

81 Kwa hiyo, kama vile umbo la dunia ya kale halikuangamizwa, kwa maji wakati iliposafishwa; umbo la sayari, sura ya kale, ninii … uchafu wote, vitu vyote ambavyo Mungu aliweka duniani, havikuangamizwa wakati dunia ya kwanza ilipoangamizwa. Na Biblia ilisema ilikuwa "imeharibiwa," bali haikuharibiwa umbo. Iliangamiza tu dhambi na wenye dhambi waliokuwa juu yake. Umbo hilo lilibaki.

82 Lakini, unaona, kama kuhesabiwa haki, kama ninyi Wabaptisti na Wamethodisti mnavyotaka kuwazia jambo hilo, kuhesabiwa haki tu, kuamini na kubatizwa, hilo halitoshi. Utatangatanga uyarudie moja kwa moja mambo ya ulimwengu, na kukata nywele zako na kuvaa kaptura, na cho chote kile. Mnaona, hakuna kitu kilichotendeka bado. Uliangalia tu nyuma ukaona umekosea.

83 Kuhesabiwa haki kuliufanyia nini ulimwengu? Hakukuufanyia kitu; ulianza moja kwa moja tena, ukiwa na dhambi nyingi tu kama ilivyowahi kuwa. Hivyo ndivyo mwanadamu anavyofanya, na huo ndivyo tu umbali yeye huenda.

Hivyo ndivyo mwinjilisti mashuhuri, Billy Graham, anavyopaswa kuona. Yeye alisema, "Ninaenda na kuwapata waongofu elfu thelathini, ninarudi mwaka mmoja baadae na sina thelathini." Huo ndiyo tu umbali walioenda. Mnaona? Na, hakika, wanatubu. Ninaamini wanatubu; wengi wao, ama baadhi yao, angalau. Lakini hilo silo linalohitajika. Inathibitisha jambo hilo hapa.

84 Sasa, kwa hiyo umbo la dunia ya kale wala halikuangamizwa kwa maji. Ulimwengu ulisafishwa tu. Huo ulipata ubatizo wake. Ulibatizwa.

Kwa hiyo umbo litabaki, ingawa utaunguzwa kwa Moto. Hauangamizi dunia, unaona, unaangamiza tu dhambi iliyo juu yake.

85 Angalia hapa, baadhi yenu ninyi wanafunzi wa Biblia, na hasa Daktari Vayle akiniangalia. Angalia katika Petro, katika sura ya 2 ya Petro hapa, sura ya 3, hasa, yeye anatumia neno "ulimwengu," kama neno la Kiyunani kosmos, ambalo linamaanisha, "utaratibu wa ulimwengu." "Dunia itatoweka, viumbe vya asili vitayeyushwa kwa joto kali mno." Mnaona? Haimaanishi ya kwamba dunia, sayari, itatoweka. Lakini ulimwengu, kosmos, siasa, wenye dhambi, mifumo, dhambi, maradhi, vijidudu vya magonjwa, kila kitu kilicho cha makosa, kitatoweka. Kila kitu ambacho wakati mmoja …

Mungu wakati mmoja alitikisa mbingu, lakini wakati huu alisema atatikisa nchi, mbingu na nchi … "Aliitikisa nchi," hasa, "na halafu wakati huu Yeye atatikisa mbingu." Mnaona? "Kwa maana tunaupokea Ufalme usioweza kutikiswa." Ni Ufalme wa Milele. Angalia jinsi anavyoliendea.

86 Angalia hapa, Petro alisema, "Na itayeyuka kwa joto kali mno, na kazi zilizomo ndani yake zitateketea," si sayari. "Kazi zilizomo ndani yake," kazi za wanadamu, wanasiasa wao wote na mipango yao, na madhehebu yao yote na mipango ya kujibunia,v yote vitaamgamizwa pamoja nayo wakati itakapowaka moto.

87 "Na—na mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu." Mliona hapa? "Mbingu zitapita kwa mshindo mkuu." Sikilizeni! Dunia nzima itawaka moto, na itawasha gesi zilizo duniani na kuilipuka. Hiyo ni kweli kabisa. Nena … Biblia ilisema hapa, Petro alisema, "Na mbingu zitapita, pamoja na duniai, kwa mshindo mkuu." Mlipuko kama huo utaitikisa, loo, jamani, maana hauna budi kuua kila ugonjwa, kila mbigiri, kila mwiba. Kila kitu pale kinachopaswa kuteketezwa, Moto utateketeza. Na, kumbukeni, kwa jumla si moto wa kwaida tu, pia ni Moto mtakatifu, mnaona, ambao utamwondolea mbali Shetani na wote walio wake, pepo wote. "Mbingu na nchi," amina, "zitapita," vikiua vijidudu vyote, wadudu wote, uhai wote wa kawaida juu yake na unao izunguka, hata H2O (maji) yatalipuka. Wazia jambo hilo. Nena kuhusu kelele!

Mnafikiri hiyo kelele ndogo hapa Tucson ilikuwa ni kitu fulani, wakati Yeye alipoifungua ile Mihuri sita,

ambayo iliitikisa nchi kote, na kusababisha mazungumzo. Ngojeni mpaka dunia hii itakapopata ubatizo wake!

88 Mwajua, wakati mtu anapopokea ubatizo wa Moto, kuna kelele nyingi sana pale. Wanafikiri hiyo ni aibu, kuwasikia watu wakipiga makelele na kupaza sauti namna hiyo. Ngojeni tu mpaka dunia hii itakapopata ubatizo wake!

Naam, itaelezea … italipuka, H2O, maji, kwa kuwa Biblia ilisema hapa katika Ufunuo 21, "na hakukuwa na bahari tena," italipuka. Jambo hili litabadilisha uso wote wa dunia nzima. Itapasuka na kuvunjika vipande -vipande. Sehemu yote ya nje, uso wa dunia, na mamia ya futi chini yake, zitabomolewa tu kabisa. Anga, gesi zilizoko duniani sasa, ambapo wanapata makombora haya ambayo hayawezi kupitia ndani yake, tufe kuu huko juu, huko juu kabisa katika namna fulani ya duara ambayo kuna kila namna ya gesi, wanasema ; na hilo litapasuka. Ghadhabu takatifu ya Mungu itakuja juu yake, unaona, na itaisafisha, itabadilisha uso wote.

89 Sasa, wengi wenu ambao mnataka kuandika neno hili, neno la Kiyunani, "kupita." Linatokana na neno … Ilinibidi kulitafuta. Nikawaza, "Dunia hii itapitaje, na hata hivyo tutaishi juu yake?" Lakini kama mtaangalia, baadhi yenu ninyi watu mnaotaka kuliandika, nitawatajia herufi zake. Nisingeweza kulitamka, p-a-r-e-r-e-c-h-o-m-i-a. Sijui jinsi ya kulitamka.

Sasa, kwa njia hiyo, kama nilivyosema, nitakapopata … Uvuvio unanigusa kwa ajili ya jambo fulani, ndipo ninarudi nyuma kutafuta neno. Sasa, hapa, siwezi kutaja herufi za neno, ama si—siwezi kulitamka. Lakini, katika jambo hilo, Bwana bado amenipa njia. Ninaenda na kutafuta kujua hilo neno linamaanisha nini, ndipo nilipata. Mnaona? Ndipo nimelipata, tena. Mnaona?

Mbingu na nchi zitapita, sasa, neno hili linamaanisha, "kupita kutoka umbo moja hadi lingine." Halimaanishi "kuangamiza," kama vile neno la Kiingereza lingemaanisha, kupita, ni kuangamizwa. Lakini neno la Kiebrania, au la Kiyunani hapa, halimaanishi kupita; linamaanisha, "kutoka kwenye kitu kimoja hadi kingine." Angalia, lakini, "kupita kutoka hali moja," inasema, "kwenda nyingine."

90 Sasa angalia, Paulo alilitumia, kama unataka kulisoma sasa. Liandike, unaweza kulisoma baadaye. Katika Tito 3:5, Paulo anatumia neno lili hili, linamaanisha kuzaliwa upya kwa mtu, ya kwamba mtu amepita kutoka kuwa mwenye dhambi akawa mtakatifu, hajaangamizwa kabisa. Wakati mtu anapobadilishwa, yeye haangamizwi, bali yeye ni mtu aliyebadilika. Yeye amebadilishwa kutoka kile alivyokuwa kuwa vile alivyo, si kuangamizwa.

91 Yesu alitumia neno lile lile katika Mathayo 19:28; sasa, si 28:19. Sasa, 19:28, Yeye aliwaambia, "Mtaketi pamoja Nami katika Ufalme wa Baba Yangu, mmezaliwa upya," mnaona, "kubadilishwa," wakati mtakapobadilishwa. Alitumia neno lile lile.

Naye alitumia neno lile lile aliposema, kwa mwana -punda, kasema, "Mfungueni mwana -punda mkamwache aende."

Alisema jambo lile lile kwenye ufufuo wa Lazaro, "Mfungueni! Mbadilisheni! Yeye amekuwa amefungwa; mwache aende!"

Inamaanisha nini? Dunia itafunguliwa kutoka mikononi mwa Shetani. Itafunguliwa. Itafunguliwa kutoka kwenye siasa, itafunguliwa kutoka kwenye mifumo ya kidini ya kimadhehebu; kutumiwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kuanzishwa hapa duniani. Lakini mradi tu iko mikononi mwa Shetani, siasa … Shetani mtawala wa dunia, anamiliki; ilikuwa ni mali yake, lakini sasa Kristo ameikomboa.

92 Wakati mmoja, nilikuwa mali yake, lakini si sasa. Wakati mmoja, maskini mwanamke huyo alikuwa mali yake, bali si sasa. Unaona, Yeye alikuja kufungua mfungo wake. Yeye aliufungua mfungo wa dhambi, wa Shetani, juu ya maisha yangu, juu ya maisha yako, na sasa sisi si wake.

Hivi mara nyingi mmenisikia nikisema, katika maombi, "ondoa mikono yako kwenye mali ya Mungu"? Mnaona? Amina! Uwe na imani ya kudai yaliyo yako. Hizo ni haki zako. "Ondoa mikono yako kwa mwanamke huyo! Mwondoe mikono yako kwa mwanaume huyo!" Unaona, imani itafanya jambo hilo. Loo, jamani! Si kuangamiza, bali, tu, "Ondoa mikono yako juu yake," kuifungua, kuiachilia, kuipitisha. Inabadilika.

Dunia itabadilika. Siasa zitabadilika. Dini zitabadilika. Madhehebu yatapita. Siasa zitapita. Ufalme wa Mungu utaanzishwa.

93 Tunasoma katika Yohana, tunasoma Yohana katika Ufunuo 6:14, unaona, "iliondoka kama gombo." Biblia ilisema ninii … ya kwamba … Yohana alisema, "Niliona mbingu na nchi zikiondoka kama gombo." Yohana, Ufunuo 6:14.

Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita," ama, kwa maneno mengine, "mbingu na nchi zitabadilishwa." Mnaona, nilitumia neno lile lile papo hapo tena.

La, si kuangamizwa. Kwa kuwa, baadaye, katika Ufunuo 21:2 hadi 24, aliona Yerusalemu Mpya ikishuka kutoka kwa Mungu kutoka Mbinguni, na kuketi juu ya dunia hii. Haimaanishi itaangamizwa. Mifumo itabadilishwa.

94 Danieli aliona jambo lile lile. Daneili aliona jambo lile lile. Mwamba uliochongwa bila kazi ya mikono uliipiga dunia; na hiyo sanamu yote ya hizo taratibu ikavunjiliwa mbali ikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari, na upepo ukavipeperusha. Na ule Mwamba, Wenyewe, ulikua ukawa Mlima mkubwa ulioifunika dunia. Angalia Mlima huo sasa, katika muda mfupi. Mlima huo uliifunika dunia.

Pia, tunaona hapa, hapa, pia, katika Ufunuo pale, ilisema, "Wafalme wa Nchi Mpya wataleta heshima na utukufu wao ndani yake." Katika nchi, imeketi … Yerusalemu Mpya imeketi juu ya dunia hii. Mnaona, ilibadilika tu.

95 Wewe ni mtu yule yule, katika kimo, uliyekuwa wakati Mungu alipokuita, mwanamke yule yule. Lakini, unaona, jambo ni kwamba, ilikuwa ni kuzaliwa upya. Maisha ya kale yalipita. Tamaa ya kale imepita. Wakati, ulipenda kunywa pombe, na kulaani, na kuzozana, na kula, na kuzurura, na kukosa uadilifu, kitu hicho kilikufa tu. Mnaona? Lakini sasa umetumiwa … Kisha ulikuwa chombo cha Shetani; sasa umekombolewa.

Na hivyo ndivyo ulimwengu utakavyokuwa, vivyo hivyo, kukombolewa, Mbingu Mpya na Nchi Mpya.

Kama tu wewe, "Wewe ni kiumbe kipya." Na neno la Kiyunani pale, mtu yeyote anajua, lilisema, "Wewe ni kiumbe kipya." Amina! Kiumbe kipya katika hekalu lile lile la kale. Haleluya. Angalia jambo linalotokea hapa sasa. Tukufu! Vema.

96 Sasa tunaona ya kwamba dunia hii itashikilia wafalme wa dunia.

Na, tena, katika Mathayo 5:5, Yesu alisema, "Wapole watairithi nchi." Haitaenda kunini, kuwa tu na dunia nyingine. Itakuwa tu nchi ile ile. Ninajaribu kuwaletea—ule mpango wa ukombozi, kabla, kama sipati kitu kingine, mnaona. Ubatizo wa Moto, juu yake, ni kuusafisha tu na kuufanya mahali panapofaa kwa watu Wake wa pole kuishi mle. Mnaona? Loo!

Kama vile alivyotufanyia sisi, uumbaji Wake, kuishi ndani yake. Kabla hajaingia ndani yake, ilimbidi kutupa ubatizo wa Moto; ndipo Roho Mtakatifu akaingia na kuishi, ubatizo wa Moto. Ndipo, unapopata ubatizo huo wa Moto, ndipo Roho Mtakatifu anaweza kuingia. Nini? Anapoingia, anachoma kila kitu kilicho kinyume na Neno, kutoka kwako. Mnaona? Hataamini kitu kingine ila Neno, kwa maana Hilo ni Neno. Mnaona? Mnaona? Mnaona?

97 Sasa, hilo ndilo tulilokuwa tukinena hivi majuzi, thibitisho la Roho Mtakatifu. Mnaona? Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni wakati unapoweza kulipokea Neno; si mfumo fulani, bali kupata uelewa dhahiri. Unajuaje Neno ni dhahiri, unalifahamu Hilo? Angalieni likijithibitisha Lenyewe.

"Vema," unasema, "Ninaona hili likifanya jambo hilo, na lile." Loo, naam, magugu yanaishi vivyo hivyo. Mnaona?

Lakini halina budi kuwa ni Neno lote. Ili uwe Bibi -arusi, huna budi kuwa sehemu Yake. Yeye ni Neno. Mnaona? Na ni sehemu gani ya Yeye? Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii atakapomwita Bibi -arusi Wake. Kuwa sehemu ya Hilo. Mnalipata? Sasa, msi—msipoteze hilo sasa. Angalia.

Naye anaifanya mahali panapofaa kuishi Milele.

98 Angalia, huu bado haujatajwa kunini … Utawala huu wa Miaka Elfu, ile miaka elfu, si ile Dunia Mpya. Mnaona, ule Utawala wa Miaka Elfu ni utawala tofauti. Huo ndio tutakaoingia, ule Utawala wa Miaka Elfu, bali hiyo si Nchi Mpya, Mbingu Mpya. La, la. Hapo ni mahali pa kupumzika tu, mnaona, kipindi cha kupumzika, si Mbingu Mpya na Nchi Mpya kamwe; kwa kuwa, mnaona, katika ule Utawala wa Miaka Elfu kuna vitu ambayo visingeingia katika Huo. Ni mfano wa siku ya saba ya kale, kutoka Edeni; siku ya saba, baada ya Yeye kuumba ulimwengu. Siku ya saba, Yeye alipumzika katika Edeni, na ule Utawala wa Miaka Elfu.

99 Mnaona, ulimwengu sasa una umri wa karibu miaka elfu sita. Mnaona? Kila baada ya miaka elfu mbili imekuwa na ma—maangamizi. Mnaona?

Elfu mbili za kwanza, gharika ikaja, Naye akaubatiza kwa (nini?) Kwa maji.

Elfu mbili iliyofuata, Yesu alikuja kuitakasa na kuidai, akamwaga Damu Yake juu yake, akaiita Yake. Vema.

"Nitakuja tena," a-ha, sasa kama Mfalme pamoja na Malkia Wake, na miaka elfu mbili ya pili (Yeye anafanya nini?) Yeye anakuja na kutoa muda Wake wa kupumzika.

Na halafu anauteketeza kwa moto, na kudai kuwa ni Wake Mwenyewe; anawaweka waliowake Wake

Mwenyewe juu yake.

Na angalia, si ulimwengu mkamilifu, huu Utawala wa Miaka Elfu, ni mfano wa siku ya saba. Ndipo inakuja Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Mnaona, tungali tuna hukumu. Tungali katika wakati, katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Ni siku moja, miaka elfu moja. Ni kipindi cha wakati. Sio, msichanganye hilo na Nchi Mpya, sasa, maana si hivyo.

100 Huenda ukaniambia jambo hili. Sasa ninajisikia tu mtu fulani anaweza kuniambia jambo hili, ya kwamba, "Sasa, Ndugu Branham, utafanya nini sasa? Umeishiwa na saba zako kamili. Unaelekea wapi kufanya nini sasa? Sasa, wewe ni mwana-majira." Ambapo, ndivyo nilivyo. Ninaamini ya kwamba Mungu ndivyo alivyo, pia. Tazama, angalia. "Umeishiwa na mifano yako ya majira. Kwa kuwa, kama utaweka kitu zaidi ya siku hiyo ya saba, utakipataje? Unaelekea wapi sasa?"

Vema, nitahitaji usikivu wako kwa jambo fulani, mnaona. A-ha. Mnaona? Kwa hiyo, mimi sijatoka—sijatoka kwenye majira, bado. Nina Andiko lingine hapa. Na, kumbukeni, yote hayana budi kutimizwa, kila sehemu Yake. Mnaona?

101 Sasa unasema, "Ndugu Branham, unajaribu kuweka kitu fulani huko mbali zaidi baada ya siku hiyo ya saba, hiyo sabato ya siku ya saba."

Kama vile Mungu alivyoumba dunia na kufanya kazi siku sita, na kupumzika siku ya saba, ilikuwa ni mfano tu wa wakati, wakati. Lakini nimesema tu hapa, tunakuwa wa Milele.

"Kwa hiyo mfano wako uko wapi sasa? Ulisema wewe ni mwana-mifano. Kwa hiyo, wewe, umeishiwa na mifano sasa." La, sijaishiwa. Hebu na tuone kama tumeishiwa.

102 Hebu na tuende kwenye Mambo ya Walawi, huko nyuma katika sura ya 23 ya Mambo ya Walawi. Sasa nawatakeni mwone katika Mambo ya Walawi, mahali tulipokuwa Jumapili iliyopita, ama iliyopita … Hili ndilo lililonipa wazo, papa hapa. Sura ya 23 ya Mambo ya Walawi, na aya ya 26.

Sasa kumbukeni, kuna siku saba za sikukuu. Sikukuu ya baragumu, sikukuu ya—ya vibanda, sikukuu ya kutikiswa kwa miganda, ninii … Haya yote, kuna siku saba kuu za sikukuu, hizo zilikuwa tu ni mfano wa zile Nyakati Saba za Kanisa. Nanyi mnakumbuka kulikuwa na sabato ngapi kati ya moja na nyingine? Mnaona, sabato saba kati ya pentekoste na baragumu, ambazo zilikuwa ni Nyakati Saba za Kanisa. Na kulikuwa na siku saba za sikukuu, ambazo zinawakilisha zile Nyakati Saba za Kanisa. Endelea kuhesabu namba zako.

103 Sema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, tayari umeishiwa. Una saba yako."

Vema, hebu tuchukue sikukuu ya mwisho, ambayo ni sikukuu ya vibanda. Sasa angalia hapa katika kifungu cha 36.

> *Ninyi mtamsongezea BWANA sadaka kwa moto siku saba; siku nane—siku ya nane kutakuwa na kusanyiko takatifu (kuna wakati mwingine mtakatifu unaokuja) …kusanyiko takatifu kwenu; nanyi mtamsongezea BWANA sadaka kwa moto; na ni mkutano wa makini huu; msifanye kazi yo yote ya utumishi.*

Sasa tuna "siku ya nane." Sasa, kuna siku saba tu, bali hapa tunazungumza juu ya "siku ya nane," kusanyiko takatifu, kusanyiko. Angalia, "Msifanye kazi yo yote siku hiyo." Siku ya nane, ni (nini?) Kurudi kwenye siku ya kwanza. Mbona, inazungumzia Umilele, wakati inapozunguka bila mahali pa kusimama. Amina. Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

104 Angalia, ilikuwa pia kwenye siku hii ya nane. Siku ya mwisho, siku ya sikukuu ya vibanda, angalia baada ya hiyo, baada ya siku ya mwisho ya sikukuu, baada ya Wakati wa mwisho wa Kanisa, baada ya siku saba nzima za mwisho juu ya nchi, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, ndipo kusanyiko hili Takatifu linakuja.

Kumbukeni, hii ni sikukuu ya vibanda, vibanda, "mahali pa kukusanyika." Amina! Ambapo, "Katika ule Utawala wa Miaka Elfu," Biblia ilisema, "watajenga nyumba; watakaa."

Lakini katika ile Nchi Mpya, Yeye tayari ameenda na kutayarisha mahali hapo. Pameshajengwa Hatuna uhusiano wo wote na kuijengwa kwake. Amina. Milele! Loo, ninapenda tu Neno hilo! Jamani! Kusanyiko Takatifu, siku ya nane. Ambayo, ni siku saba tu. Halafu kwenye siku ya nane, ambayo inarudi kwenye siku ya kwanza tena, inarudi moja kwa moja kwenye siku ya kwanza, siku ya nane ni Kusanyiko Takatifu- … Kusanyiko.

105 Angalia, siku saba, inahusika tu na ule uumbaji wa kale, wakati wa dunia. Siku saba, huo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, siku ya pumziko. Kama vile Mungu alivyofanya kazi siku sita, akapumzika siku ya saba; Kanisa linafanya kazi siku sita, na kupumzika siku ya saba, bali ungali katika kipindi cha wakati. Mimi sizungumzii kuhusu umilele.

Lakini, unaona, hakuna kitu kama siku nane; unarudi kwenye siku ya kwanza tena, mnaona, siku ya kwanza.

106 Sabato inazungumza juu ya torati ya kale, ambayo iliyokuwa ya kupita. Kule kushika sabato, ambayo "ilipita," ama, nimesema, "ilibadilika ikawa nyingine." Haukupita; ilibadilika tu kutoka kwenye ile sheria ya kale, ya kushika siku fulani ya juma.

Isaya, mlango wa 19, ilisema, ninaamini 28:19, ilisema, "Amri lazima iwe juu ya amri; hapa kidogo, na pale kidogo." "Lishikeni lililo jema." "Kwa maana kwa midomo ya watu wenye kigugumizi na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hapa kuna pumziko." Mnaona?

Unaingia katika Uzima, siyo kuadhimisha siku wala kivuli. Paulo alisema, huko katika Waebrania sura ya 4. "Mnashika siku na vivuli, na vitu kama hivyo; nachelea ujuzi wenu." Mnaona, sisi hatuingii katika siku fulani na taratibu "Mmepita mautini kuingia Uzima wa Milele," si siku na nyakati. Mmepita kuingia katika Umilele. Hilo ndilo kusanyiko taka- … kusanyiko, kusanyiko, hasa.

107 Siku saba, angalia, ambazo "hupita," ama, nilivyosema, "zinabadilika kuwa nyingine." Siku nane zinahusiana na uumbaji mpya, mnaona, si uumbaji wa kale. Siku nane ni uumbaji mpya.

Kwa kuwa, ilikuwa katika siku ya nane ambapo Bwana wetu alifufuka katika wafu. Hilo hapo kusanyiko lako lingine, ule utakatifu; bila kutilia maanani sabato, hata kidogo, ama sikukuu ya vibanda, sikukuu ya hii, na sikukuu ya pentekoste. Yesu alifufuka katika wafu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, katika siku ya nane. Baada ya zile sabato saba, ama siku saba, Nyakati Saba za Kanisa, Yesu alifufuka katika wafu. Siku ya nane, ambayo ni kusanyiko takatifu, mnaona, ambayo ni siku ya kwanza.

Mnaona, mmeninii, mmepita katika wakati, na mkaingia katika Umilele tena; si kuadhimisha siku, na kusdhimisha sabato; na miandamo ya mwezi, na mambo kama hayo. "Bali umepita," umebadilisha kabadilisha umbo lako; si kuangamizwa. Utukufu! "Bali kupita kutoka mautini kuingia katika Uzima wa Milele." Loo, mambo ambayo Biblia inatufundisha! Mnaona, kupita kutoka kwa moja kuingia nyingine.

108 Vema, "kupita," ile sabato ya kale imepita. Yesu alifufuka katika siku ya nane. Hiyo ilikuwa ni siku tukufu, takatifu. Na haikuwa siku fulani; maana siku, wakati, ulikuwa umekwisha. Ulipita ukaingia katika Umilele. Mnaona, ilirudi moja kwa moja kwenye siku ya kwanza tena. Mnaona?

Umilele ni kama tu—duara. Huwezi kupata kona yoyote kwake. Huwezi kupata mahali pa kusimama katika duara kamilifu. Unaendelea na kuendelea. Sijali unaenda umbali gani, ungali unaenda. Unaweza kuanza kuzunguka namna hii; uende kupitia sakafuni, kupitia duniani, kupita zaidi ya dunia, ungali una- … [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Vitu vyote vilivyoumbwa chini hapa, vimepotoshwa, havikuumbwa, na Shetani, vitaanguka wakati kengele kuu ya dhahabu itakapolia na Baragumu ikilia.

Na huko nyuma kule mwanzoni, ambapo nguzo ya kushukilia ilifanywa katika Edeni, wakati mwanadamu alipokuja duniani naye akaanguka, mwana -kondoo mdogo alimwaga damu yake, ambaye alinena juu ya Mwana -Kondoo mkuu aliyekuwa akija kumwaga Damu Yake. Kalvari iliinua msalaba, ambao ulifungwa kwa ajili ya Agano la Kale; kwa hao waliohesabiwa haki, walioutazamia huo. Na katika wakati huu mpya, kwenye kule Kuja kwa Bwana, kwenye Nchi Mpya, ile kamba ya wokovu (ile Damu, zile Nguvu za ukombozi ninazonena habari zake, na kupitia katika mfumo ule ule zimewakomboa wanadamu na nchi pia). itafufuka katika Umilele tena. Na lile Ziwa la Moto litateketeza kila kitu kisichomcha Mungu na kisichochaguliwa tangu zamani Kwake. Mnaona jambo hilo?

109 Angalia, siku ya nane, Yesu alifufuka kwa ajili ya kuhesabiwa kwetu haki. Yule Mfalme wa Milele, akiwa na Ufalme wa Milele atakayebatizwa, katika Uzima wa Milele. Si siku saba; haikuwa na uhusiano wo wote na siku zozote zile. Inanena juu ya nyingine, Milele, kuja; ikinena juu ya wakati wa Milele, Ulimwengu ninaonena habari zake.

110 Na, angalia, baada ya siku hamsini, ama sabato saba kutoka hapo, tena kukaja kusanyiko lingine takatifu. Nini kilichotukia? Roho Mtakatifu alishuka kwenye Siku ya Pentekoste, siku ya saba … Ama, siku ya nane, hasa, siku ya nane, iliangukia kwenye siku ya nane. Ilikuwa ni sabato saba baadaye, kikamilifu, baada ya kufufuka Kwake, mnaona; kwa hiyo ingekuwa mara saba ya hizo tena, kuirudisha moja kwa moja kwenye siku ya kwanza ya juma tena, kikamilifu. Mnaona?

111 Hilo hapo kusanyiko lenu takatifu, halina uhusiano wowote na vitu vya kuonekana. Ni zaidi ya hapo. Ni katika Ufalme wa Mungu, pamoja na Uzima wa Milele, pamoja na wale waliochaguliwa tangu zamani ambao hawakuanza kamwe. Haikuanza siku yoyote. Hukuokolewa siku yoyote. Wewe daima ulikuwa umeokolewa. Amina. Yesu alikuja tu kuwakomboa hao; bali uliokolewa, tangu mwanzo, kwa sababu ulikuwa na Uzima wa Milele, kwanza.

112 Samaki wa mtoni hawezi kamwe kuwa samaki sindano ama kiluwiluwi. Huenda akawa ndani ya maji

yale yale pamoja naye, bali alikuwa, tangu mwanzo, samaki wa mtoni. Nyavu ilimshika tu, unaona, bali alikuwa hivyo tangu mwanzo. Kuna hiyo …

Sasa, hatuko nje ya wakati. Sivyo? Tuko moja kwa moja kwenye Maandiko. Siku hamsini baadaye, akaja.

113 Mnaona, nane haiwezi kuhesabiwa pamoja na juma. Unaona, haiwezi kuhesabiwa, siku nane katika juma. Huwezi kufanya hivyo, unaona, kwa sababu kuna siku saba tu katika juma. Ihesabu namna yoyote utakayo. Jumapili ni siku ya kwanza ya juma. Unaona, unahesabu saba, basi huna budi kurudi na kuanza tena. Unahesabu saba, unarudi na uhesabu tena. Mnaona?

114 Nasi tuliishi kupitia mifano hii yote hapa ndani, lakini, unapofikia ya nane, unaingia katika Umilele. Huji kwa torati, na wala kawaida za dini, na taratibu. Unakuja kwa kuchaguliwa kimbele. Amina! Kuna kusanyiko halisi, takatifu! Mnaona? Nasi tunamalizia wakati wa saba wa kanisa, wakati wa kanisa, wakati wa Kipentekoste. Mnaona jambo hilo? Tunaingia kwenye kusanyiko hilo takatifu. Tunaingia katika ule Umilele halisi, wa kweli, ambapo Kanisa limeitwa; si kwenye kituo fulani, madhehebu fulani, bali katika Umilele pamoja na Mfalme wao wa Milele. Mnaona? Hatuna jambo hilo hata kidogo, hakuna kitu kama siku, na kadhalika, na nyakati. Umepita ukaingia katika Umilele, mahali ulikotoka. Ulikuwa kule, kwanza. Mnaona?

115 Kama una Uzima wa Milele, kuna wa aina moja tu, huo ni Mungu, nawe ni sifa iliyodhihirishwa. Mnaona? Kama wewe … Kama haupo, hautakuwapo, hata hivyo. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Mnaona? Ambapo, "hupita," mambo haya yote ya kale; bali mambo haya hayapiti, kwa hiyo yananena juu ya Umilele. Roho Mtakatifu ni wa Milele. Halafu, uko katika Umilele, mahali ulipokuwa wakati wote, bali umetambua tu kile kilichotukia.

Unaona, ulifanywa kwa kusudi la Milele, kwa sababu ulikuwa u—udhihirisho wa sifa iliyokuwa ndani ya Mungu, ambaye aliyokuwazia na akakutamka; Naye akaumba dunia apate kukutwaa toka kwake, na kukufanya mwanadamu. Na dhambi ikaja na kuipotosha njia Yake. Ulikuja, hata hivyo, bali ulipotea pamoja na ulimwengu. Kwa hiyo Yeye alikuja na akakukomboa, ile sifa iliyotamkwa, na pia anaikomboa dunia hii kwa njia ile ile. Ndipo, kusudi Lake linaendelea. Mnaona? Loo! Haleluya! Loo, hilo linanifaa sana, wazia tu yale yaliyo mbele yetu!

116 Sasa, katika Waefeso 1:10, inaitwa … Sasa, kama unaandika, Waefeso 1:1, inaitwa, si majira, si siku ya saba. Unaitwa, "Utimilifu wa wakati." Na wakati "utimilifu wa wakati" umewadia, hapo ndipo wakati umetimia. Wakati hakuna wakati tena, basi unaingia katika Umilele, baada ya wakati wa saba wa kanisa kwisha, na ndio; Wakati wa Luther umekwisha, wakati wa Kimethodisti umekwisha, wakati wa Kipentekoste umekwisha. Na sasa unaingia katika (nini?) Umilele; hakuna saba tena, hakuna tatu tena, hakuna nyingine tena. Wako katika Umilele, ambako hakuna wakati kama namba, na nyakati, na kadhalika. Amina! Loo, jamani! Mnaona jambo hilo sasa?

117 Ama, baada ya wakati kutimizwa, dhambi yote imeondoka, imeondolewa, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, kwenye ile Hukumu kuu ya Kiti Cheupe cha Enzi. (Mfano, kwa Roho Mtakatifu.) Baada ya ulimwengu kuwaka moto na kubatizwa, ubatizo wake wa Moto mtakatifu kutoka Mbinguni; dhambi zote zimekwisha, viini vyote vya magonjwa vimekwisha, pepo wote wamekwisha, majaribu yote yamekwisha, maovu yote yamekwisha. Mfano sasa.) Basi Mungu hufanya nini? Anaweza kuketi juu ya nchi, unaona, kwa sababu dhambi yote imeondoka.

118 Hilo ndilo jambo lile lile analofanya anapokupa ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa Moto. Anaweza kuja na kukaa pamoja nawe, nasi tunaweza kuketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, kwa sababu tayari tuko ndani Yake. Si kwamba sisi "tutakuwa." Sasa tunaketi katika Kristo Yesu. Tunaingiaje katika jambo hilo? Kwa ubatizo mmoja wa Roho Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Kristo," ambapo, tumebatizwa sasa. Si "tutakuwa" ndani ya Kristo; tuko ndani! Yeye ni Mfalme mkuu wa kiroho juu ya Roho aliye ndani yetu, kwa sababu tulikuwa ndani Yake hapo mwanzo.

119 Unaona, Mungu, hapo mwanzo, wakati alipokuwazia na kuwawazia wengine namna hiyo, aliwazia Mwenyewe kuwa anaweza kushikika. Hayo yalikuwa ni mawazo Yake. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye alieleza mawazo Yake kwa Neno. Yeye alisema, "Na iwe." "Iwe," na ilikuwa. "Iwe," na ilikuwa.

Ndipo, baada ya kitambo kidogo, Yeye aliendelea kusema "na iwe," mpaka watu wakasema, siku moja, "Usimwache Mungu anene!"

Yeye alisema, "Sasa nitazungumza nao kupitia kwa nabii." Mnaona? "Tangu wakati huu na kuendelea, nitazungumza nao kupitia kwa nabii."

Naye nabii akasema, "Kutakuja; kutakuwako," na ilikuwa, na ilikuwa. Na ilikuwa hivyo, na ilikuwa hivyo, unaona, hivyo tu. Mnalipata sasa?

120 "Utimilifu wa wakati" umekuja baada ya wakati kutimizwa. Dhambi imeondoka, baada ya ubatizo wa

ulimwengu, baada ya ubatizo wa ulimwengu kuifanya mahali panapofaa; hakuna magonjwa, hakuna viini vya magonjwa; hakuna miiba, hakuna mbigiri; hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna majonzi; hakuna uzee, hakuna kitu kinachowakilisha mauti; hakuna kosa; vema; hakuna kitu cha kawaida. Milele!

Halafu, sifa Zake zimedhiirishwa kwa sababu zilikuwako, kwanza, mwanzoni. Hivyo ndivyo alivyowazia. [Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao — Mh.]

121 Halafu basi ni jambo gani lililotukia? Yeye aliwaweka Adamu na Hawa hapa duniani, na kusema, "Zaeni sasa na mkaijaze nchi." Miili yao yote ilikuwa imewekwa hapa, kwa ajili ya wewe kula na kuufanya mwili wako. Hiyo ndiyo njia aliyokuwa nayo ya kufanya jambo hilo.

Lakini dhambi ilikuja na kukatiza mpango Wake. Nao unaendelea moja kwa moja, vivyo hivyo tu, wakati unaendelea.

122 Lakini Yesu alifanya nini? Mungu alishuka akajidhihirisha Mwenyewe katika umbo la Mwanadamu, mwanadamu; alitoa uhai Wake, badala ya kukaa hapa. Ambapo, Yeye alikuwa Mfalme, bali alijitoa Mwenyewe apate kuwakomboa hao wengine. Mnalipata?

Na wakati yote yatakapokwisha, basi linarudishwa moja kwa moja, na kusudi la Mungu linatimizwa. Huyo hapo Mfalme wa Milele tena akiwa na raia Wake wa Milele, akidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, vile vile hasa alivyokuwa nao; dhambi huondolewa; ibilisi ameondolewa; yote yamekwisha sasa.

123 Ni nini kitakachofanya jambo hilo? Dunia hii isingeweza kuwa mahali pa Mbinguni kuketi sasa. Itazame, ile dhambi. Itabidi kusafishwa.

Hakuna mwanamume, hakuna mtu, hakuna mwanamke, mvulana, msichana, sijali yeye ni nani, anayefaa kwenda mimbarani, ama hata kudai kuwa Mkristo, bila kujazwa na Roho Mtakatifu. Huna haki ya kuiendea meza ya Bwana, wala ushirika wo wote, kutawadha miguu, ama cho chote kile, mpaka umetakaswa na Moto Mtakatifu wa Mungu.

Hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri isipokuwa wewe, kama vile Musa, ukutane Naye huko kwenye ileo ardhi takatifu, ile Nguzo ya Moto ikining'inia pale, mahali ambapo mtu anajijua yupo. Mnaona?

124 Angalia namna, namna tunavyokwenda. Baada ya ubatizo wa Moto ulimwenguni, vijidudu vyote vimekwisha, inafanya mahali panapofaa basi kwa ajili ya Mbinguni kukaa hapa duniani.

Ni mfano, sasa, wa kuketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu; tumepita katika huu, mchafu kama yule maskini mwanamke alivyyokuwa, alivyoingia kwenye sifa ya Mungu iliyoodhiirishwa. "Sasa sisi ni Wana wa Mungu," si tutakuwa. Sisi ni sifa za mawazo ya Mungu. Mnaona?

125 Sasa unasema, "Vema, mwangalie kuhani huyu. Yeye hakuwa mwana wa Mungu?" Ilithibitisha hakuwa. Yeye hakuweza kutambua nini? Je, yeye alisema, "Ninaamini Biblia"? Hakika. Bali asingeweza kutambua Neno lililodhiirishwa la wakati huo. Yeye alikuwa tu na elimu ya kiakili kutoka kwa kundi fulani lililokuwa limerudi kabla yake.

Na ni jambo lile lile leo! Mnaona? Ninajua hilo ni zito, bali ni Kweli.

Kulikuwako na Neno, kama lilivyonenwa hasa kwa ajili ya siku hiyo; na, yeye, hata hivyo alikuwa ni mwanachuoni, hata hivyo alikuwa mtu mashuhuri, bali asingeweza kulitambua hilo. Kwa nini? Haidhuru alikuwa msomi jinsi gani, kitu kama hicho, yeye bado hakuwa na uwakilisho wa kuchaguliwa tangu zamani. Mnaona?

Waliochaguliwa tangu zamani ndio tu wafanyao jambo hilo; ndio tu wanaoweza. Nawe unaweza tu kufanya hivyo … Kwa sababu, angalia, inathibitisha kuchaguliwa tangu zamani. Maana, kama una Uzima wa Milele, ilibidi uwe sehemu ya Mungu wakati wote, maana Yeye Ndiye pekee aliye wa Milele. Mnaona jambo hilo? Loo, jamani! Wazia jambo hilo.

126 Sasa angalia kile kinachotukia katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Dhambi imekwisha, Utawala wa Miaka Elfu sasa umeanza, ni wakati sasa ambapo Roho Mtakatifu anachukua mahali Pake.

Kama tu vile Yeye anavyofanya ndani yetu, "hupita kutoka mautini kuingia Uzimani," tukiishi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo, katika Uwepo Wake wenye utukufu. Hata mauti ya kimwili yatapita wakati huo basi; kama tu vile mauti ya kiroho yamepita sasa.

Hakuna kitu kama mauti ya kiroho sasa, kwa—kwa—kwa mtakatifu wa Mungu aliyebatizwa. "Ingawa alikuwa amekufa, bado ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Maandiko yote, hayana budi kutimizwa. Mnaona? Huwezi kufa. Una Uzima wa Milele. Jambo pekee, Mkombozi amekufanya utambue jambo hilo. Nawe daima ulikuwa hivyo, na hiyo ndiyo sababu unaona siku unayoishi. Ni wangapi wanaoiona? Inua mkono wako. Mnaona? Asanteni. Mnaona? Siku tunayoishi, unaitambua.

127 Sasa, Methodisti ilisema, "Unapopiga makelele, umempata." Wengi wao walipiga makelele wala hawakumpata huyo.

Wapentekoste walisema, "Unaponena kwa lugha, umempata." Wengi wananena kwa lugha, wala hawakuwa naye.

Angalia namna, kila namna ya taratibu walizokuwa nazo Mafarisayo wale, lakini wakati Neno lilipodhihirishwa, wao hawakulitambua. Mnaona? Mnaona?

Na kama wewe ni Bibi -arusi, Bibi -arusi ni sehemu ya Mume. Na kama … Mahali pekee ambapo utapata kulitambua, ni kutambua wewe ni sehemu gani ya huyo Mume (hilo Neno), ama huwezi kutambua kuwa ni Bibi -arusi. Ni wangapi wanaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Mnaona? Mnaona? Huna budi kutambua msimamo wako.

128 Huwezi kutambua mahali pa mtu mwingine. Vipi kama—vipi kama Musa angekuja na ujumbe wa Nuhu? Naye Nuhu alikuwa sehemu ya huo, bali huo usingelitenda kazi. Vipi kama—kama—kama—kama Yesu angalikuja na Ujumbe wa Musa? Usingelitenda kazi. Mnaona, ulikuwa ni wakati tofauti, ulikuwa ni unabii tofauti, sehemu nyingine ya Neno ilipaswa kutimizwa pale. Walikuwa katika siku nyingine ya juma. Siyo, kazi ya Jumanne haiwezi kufanywa Jumatano. Na ya Jumatano haina budi kufanywa Jumatano. Mnaona? Jumamosi haina budi kuwa ni kazi ya Jumamosi. Mnaona?

Na, wao, wao walitambua, "Loo, Musa, tunaye Musa."

Yeye alisema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa maana Yeye ndiye aliyenena habari Zangu. 'Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii kama mimi.'" Unalipata wazo hilo? Loo, jamani! Mnaona?

Ndipo Yesu akasema, katika Yohana 14, "Wakati Yeye, Roho Mtakatifu, atakapokuja, Yeye atawakumbusha mambo haya, unaona, kuwaonesha ni siku gani mnayoishi. Halafu basi, jambo lingine mtakalomjua kwalo, Yeye atawaonesha mambo yajayo," mnaona, mnaona, moja kwa moja kurudi kwenye ya kinabii tena,"atakapokuja." Mnaona?

129 Katika Nchi Mpya na Mbingu Mpya, hazitatiwa giza tena, wakati Dunia hii Mpya itakapokuja. Ibilisi atafungwa … Shetani, angali huru sasa; Yeye ni mshitaki. Lakini katika ile Nchi Mpya, yeye atafungwa na kutupwa katika Ziwa la Moto, katika Moto huu mtakatifu.

130 Halafu, katika Nchi hii Mpya, hebu na tuiangalie kwa dakika chache sasa. Katika Nchi hii Mpya, mbingu hazitakuwa nyeusi tena; la, hilo linatokana na laana, unaona. Kamwe hazitatiwa giza tena na mawingu yenye hasira. Upepo hautavuma juu yake tena namna hiyo. La. Kamwe hazitavunja-vunja miti, na kuvunja-vunja nyumba, na kuangusha vitu. Radi na ghadhabu hazitabubujika kutoka kwa Shetani, na kumwua mtu anayetembea barabarani, ama kuunguza jengo. Mnaona? La, si zaidi. Hakutakuwako tena na tufani zitakazoshuka chini, wala dhoruba na vimbunga, na kubomoa nyumba, na kuwaua watoto wadogo, na kadhalika. A-ha, havitakuwako tena. Kujaribu kuharibu, hakutakuwako huko. Shetani ametupwa nje.

Laiti tungalikuwa na wakati sasa. Ninayapita tu Maandiko, sasa, ili tusichelewe sana. Sina budi kuwaombea wagonjwa.

131 Mbingu na nchi zimekutana; Mungu na mwanadamu wamepatanishwa. Edeni iliyorudishwa imeanza; mnaona, laana yote imekwisha.

Ni kama tu, laana yote ya dhambi imeondoka wakati Roho Mtakatifu anapokukubali. Mnaona, humkubali Huyoo; Yeye hukukubali, unaona, maana ni sifa za Mungu. Mnaona, kama ni Roho Mtakatifu, maana yake ni, Roho wa Mungu; na ni sifa, wazo la Mungu, limekukubali kwa sababu ulichaguliwa kwa kusudi hilo. Mnaona? Hata hivyo, ulizaliwa katika dhambi; bali Mungu alikuwa na sifa hiyo, na hapa ulijidhiirisha mwenyewe hapa duniani, Naye anashuka na kukuchukua. Mnaona, umerudi hapa; hapa ndipo mahali pako. Mnaona? Mnaona, dhambi imepoteza nguvu zake. Hiyo ni kweli. Tamaa ya dhambi imekwisha toka moyoni mwako, wakati Roho Mtakatifu anapoingia. Wewe ni mtu aliyerejeshwa.

132 Na halafu wakati dunia itakaporejeshwa, kwa jambo lile lile, hakuwezi kuwa na laana tena, hakuna dhoruba tena, hakuna tena upepo, hakuna tena vimbunga—vimbunga, hasa. Mmepatanishwa; mwanadamu na Mungu wamekutana. Nchi Mpya itavikwa uzuri wake wa Edeni tena. Nchi Mpya itasambaa, ninii yake, baada ya ubatizo wake wa Moto.

Wazia tu, itashika moto na kuungua. Viumbe vya asili vitaungua kwa—kwa moto mkali. Kazi zote duniani zitateketezwa kwa moto. Maji yote yatalipuka; yatashika moto na kulipuka yote. Kila kitu kitalipuka. Volkeno italipuka na, maelfu ya maili hewani, matope ya mawe moto yataruka. Kila kiini cha ugonjwa … Roho Mtakatifu wa Mungu atasafisha kila chembe ya dhambi na kila kitu. Pepo wote watafungwa na kutupwa katika Ziwa la Moto, ule Moto ulao, hasira ya Mungu ya Moto.

133 Hakuna mnyama atakayekuwapo huku kukuangamiza tena. Unapotembea barabarani, katika bustani za maua, hakutakuwako na nyoka wa kukutolea ukali na kukuuma, kwa mate yake sumu. Loo, jamani! Hilo halitakuwa la ajabu? Sikilizeni. Hakuna sehemu yo yote ya Nchi hiyo Mpya itakayoweka tuta la udongo wa majano na kulundikwa kufanya mahali palipoinuka, ama kaburi; hapatakuwako na yo yote ya hayo.

Mwanadamu na Mungu wamekusanyika pamoja; Bibi -arusi na Bwana Arusi. Mbingu na nchi zimekumbatiana; Mungu ameshuka kuja kuishi kati ya watu. Maskani Yake iko pamoja nao.

Hakutakuwa na dhambi tena, hakuna huzuni tena. Kamwe hakutakuwapo na tone la chozi kutoka kwenye shavu la mama, juu ya mtoto wake. Amina. Hakuwakuwa na hayo, kwenye Ardhi hiyo Mpya. La. Imekombolewa. Ni mali Yake, na kwa ajili ya walio Wake waliokombolewa kutoka kwake. Mnaona?

134 Na, tazameni, ninyi ni sehemu ya hiyo ardhi. Hiyo ni kweli? Na wakati alipowakomboa, Yeye aliikomboa dunia kwa kitu kile kile, nanyi mko pamoja tena. Loo, inaweza kuwa dhahiri namna gani. Mnaona? Huna budi kukombolewa kwa sababu wewe ni sehemu yake. Na kama Damu haikukudondokea, bado hujakombolewa; hujaitwa. Ndipo Yeye huisafisha; hilo ndilo jambo lile lile Yeye analofanya katika Moto. Hata japokuwa, Damu ilimwagika, bado haina budi kusafishwa kwa Moto, hiyo ni kweli, kwa ajili ya mahali pa kukaa pa Mungu.

Mungu tayari amechukua makao Yake, kwa uwezekano. Ufalme wa Mungu umo duniani sasa, katika mioyo ya watakatifu Wake. Ni sifa Zake alizoanza hapo mwanzo. Sasa sifa Zake zimekombolewa. Anangojea nini? Kuikomboa dunia, kuweka sifa Zake juu yake, kutimiza hasa mpango Wake uliochaguliwa tangu zamani. Mnaona jambo hilo?

135 Angalia, hakuna makaburi, hakuna matone ya machozi, kamwe, hakuna umwagaji damu tena. Yeye hatalowanishwa na chozi wala damu. La. Hakutakuwako na vita tena. La. Hakuna mawingu ya majira ya baridi kali. Hakuna theluji yenye baridi kifuani mwake; Haitakuwepo hapo tena juu yake. Jua kali halitaninii, choma nyasi zake kamwe. Haleluya! Hata jangwa litazaa waridi. "Lile jangwa la kale lenye nata litachanua, siku moja, kama waridi," Mungu alisema hivyo; wakati anapokombolewa, wakati anapochukua ubatizo wake wa Moto. Kuna kila namna ya minyaa na miiba na kila kitu pale sasa, bali inangojea ubatizo wa Moto unaokuja.

Kama vile mtu huyo alivyokuwa, wakati alipokuwa bado ana chuki, husuda na ugomvi ndani yake; wakati ubatizo wa Moto ulipokuja, ulivisafisha. Hakuna tena wivu, hakuna tena kitu cho chote; ni mahali pa kuishi pa Mungu kabisa. Na, kumbukeni, hao ndio wawakilishi Wake watakaomlaki kule ng'ambo. Amina! Loo, ni ninii …

136 Hiyo si hadithi tu; hiyo ni Kweli. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema. Hivyo ndivyo alivyoahidi. Hicho ndicho Bibi -arusi anachoendea. "Hata jangwa," Yeye alisema, "litachanua, litakuwa waridi."

Shetani, dhambi, na wenye dhambi, wameondolewa, milele. Yote yamekwisha; yakaunganishwa katika Umilele. Na yote yaliyokuwa yamepotoshwa, yule malaika mkuu aliyeketi pale siku moja, Shetani, aliyefanya maovu haya yote, ataangamizwa. Mnakumbuka, Biblia ilisema, "Kama nafsi hiyo haitafanya kama alivyofanya Yeye, aliyosema yafanywe, Yeye ataangamiza hata nafsi hiyo."

Lakini, mnaona, Yeye hawezi kujiangamiza Mwenyewe na kubaki Mungu. Kwa hiyo, kama nafsi hiyo ni ya ulimwengu, haina budi kuangamizwa. Lakini kama ni ya Milele, pamoja na Mungu, kamwe haikuanza, kwa sababu ni sehemu ya Mungu na haiwezi kuangamizwa kamwe. Amina! Ni mrembo iliyoje! Ni—ni shukrani iliyoje, ya kwamba Kanisa linapaswa kuona jambo hilo!

137 Enyi watu, yote mliyofanya yamewekwa papa hapa. Hivi ndivyo ninavyojaribu kusema. Ninaacha baadhi yake kwa sababu ninataka kurudi kwenye jambo hilo tena.

138 Hata mambo haya, Shetani, wenye dhambi, wameondolewa, Milele; hatakuwako tena. Wote … Mnaona, Shetani hawezi kuumba. Kama anaweza, yeye ni Mungu. Mnaona? Yeye anaweza tu kupotosha kile kilichoumbwa. Mnaona? Na upotovu wote kutaninii, kupotosha, kutaondolewa. Na mauti ni upotoshaji wa uzima; na wakati upotovu utakapomalizika, hakuwezi kuwa na mauti tena. Uzee ni ishara ya mauti; na wakati uzee unapoondolewa, uzima unaingia. Ishara zote za upotovu na kila kitu kingine kimeondolewa. Miiba na mbigiri ni ishara ya dhambi, "nchi italaaniwa pamoja nayo," nayo itaondolewa. Magonjwa yanakuja, kwa njia hiyo; yataondolewa. Mauti itaondolewa. Umwagaji damu utaondolewa.

139 Hakuna kitu kitakachougusa huo udongo ila utakatifu, hao Waliokombolewa. Loo, jamani! Naam. Loo, ninajisikia vizuri sana. Mungu, na uumbaji Wake; na viumbe Vyake vya uumbaji huu vimekombolewa kwa Damu Yake Mwenyewe. Vimetakaswa kwa utaratibu Wake wa utakaso; Utaratibu Wake wa kuua viini vya magonjwa, mchakato wa kuua dhambi!

Kama vile kitu cho chote kimetakaswa kuondoa vijidudu, utakasaji bora sana tuliopata kuwa nao umekuwa ni moto. Unaweza kuchukua chochote na kukiosha kwa sabuni na kemikali hizi zote

wanazonena, bado siyo safi. Lakini unachoma mara moja!

140 Na wakati Moto mtakatifu wa Mungu unapoitakasa ardhi kwa Kemikali; Yeye amemwinua Bibi -arusi Wake, ambaye anaweza kuingia Mbinguni pamoja Naye, wakati hili jambo likiendelea. Na kurudi juu ya nchi tena, Mbingu Mpya na Nchi Mpya. Kile kipupwe cha baridi ya kale hakiwezi kudhuru. Vipindi vya kiangazi chenye joto hakiwezi kudhuru. Majangwa yatachanua kama waridi. Dhambi na wenye dhambi wameondolewa.

Mungu, na viumbe Vyake na uumbaji, wanaishi pamoja katika upatano mkamilifu. Kama vile mbingu na nchi ni mume na mke, vivyo hivyo Kristo na Kanisa, nao wote wanakutana katika mpango mmoja mkubwa sana wa ukombozi na wanaingizwa moja kwa moja kifuani mwa Mungu tena. Mnaona jambo hilo?

141 Na, katika ile Nchi Mpya, kuna Mji Mpya. Loo, jamani! Sasa sikilizeni kwa makini. Msisahau jambo hili. Ya kwamba, Yesu alisema, katika Yohana 14, Yeye angeenda kuandaa. "Msifadhaike mioyoni mwenu." Wakati anapoondoka, "Nina sababu ya kuondoka. Mmemwamini Mungu,"Yeye alisema,"niaminini na Mimi." Hawakuweza kuona ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Kasema, "Umemwamini Mungu, sasa niaminini na Mimi. Nami nitawaandalia Mahali. Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi; katika Ufalme wa Baba Yangu kuna majumba mengi ya kifalme." Kristo yupo kule, akiujenga Yerusalemu Mpya sasa. Sasa sikilizeni kwa makini. Msisogee. Msininii, msikose jambo hili. Kristo yuko Mbinguni, leo, akiandaa Yerusalemu Mpya.

142 Kama tu vile Mungu alivyoumba dunia katika siku sita, akaifanya dunia katika siku sita, ama miaka elfu sita. Kama alivyosema, "Msiwe wajinga," tunasoma katika Maandiko, "miaka elfu moja ni siku moja."

Naye Kristo ameenda na anaandaa Mahali, palipokuwa pakijengwa kwa miaka elfu nyingi sana, akitayarisha Mahali. "Na kama nikienda na kuandaa Mahali, nitakuja tena, na kuwapokea; ili kwamba popote nilipo, nanyi mwepo." Angalia Mkombozi na Waliokombolewa!

143 Laiti tungalikuwa na wakati sasa. Nimepawekea alama hapa, Sulemani akinukuu, "msichana huyu, Bibi -arusi." Loo, hatuna budi kupaacha tu; tumechelewa sana, mnaona. Nitaparejea, tena. "Wakati anapojaribu kumchukua, bali ameposwa na mvulana mchunga wanyama." Wengine labda walidhani huo ulikuwa wimbo alioimba. Loo, la. Sulemani alikuwa ndiye mrithi wa kiti cha enzi cha Daudi, duniani, lakini ilionyesha ya kwamba ufalme huo ulipaswa kupita. Ilikuwa ni mfano wa Kristo akimpenda Bibi -arusi. Mnaona?

144 Angalia ya kwamba Yesu alisema, Yohana 14 sasa, "naenda kuwaandalia mahali."

Loo, pataonekanaje? Mlipata kuwazia sasa, Bibi -arusi, jinsi itakavyokuwa? Pameandaliwa na kusanifiwa na Mbunifu wa Kiungu. Mji huo utaonekanaje? Sasa, tutazungumza juu yake kwa dakika chache. Mbunifu wa Kiungu ameuandaa, ameubuni. Na, angalia, Yeye ameubuni kwa mikono myororo, kwa ajili ya Bibi -arusi Wake mpendwa. Utaonekanaje?

Ungeweza kuwazia mwanamume akimwoa mke, mwanaume mwenye uwezo, namna anavyojenga na kuweka kila kitu kidogo hasa kwa mguso wake, kile tu mkewe angependa? Amina.

145 Sasa, Mbunifu wa Kiungu ameubuni Mji Mpya, ambapo Yeye ataishi na Bibi -arusi Wake, kwa ajili ya mguso wa Mkewe tu. Si ajabu mtume alisema, "Jicho halikuyaona, sikio halikuyasikia, wala hayakuingia moyoni mwa mwanadamu." Hebu tuone kama tunaweza kulichunguza kwa muda kidogo tu, tuone namna utakavyokuwa.

Mbunifu wa Kiungu ameubuni huu kwa ajili ya Mpenzi Wake. Mnaona? Loo! ni mahali pa namna gani, wakati, tabia ya Mungu, mbunifu hodari wa kiungu, amebuni kwa ajili ya sifa za kiungu ambazo zimechaguliwa kiungu tangu zamani na Mungu mtskstifu Ambaye—Ambaye ndiye mwanzilishi wa uzima wa Mungu! Mji huo utaonekanaje! Wazia jambo hilo.

146 Kumbuka, si Mbinguni. Yohana alisema, "Niliiona ukishuka kutoka Mbinguni." Haina budi kuwa duniani. Mnaona?

Si dunia hii itakayopita; ni dunia iliyokombolewa. Mungu hakusema atainua kizazi kipya; Yeye ataenda kukikomboa kile kilicho hapa. Yeye hatainua kizazi kipya; Yeye atakikomboa kile kilichoko hapa tayari. Yeye hataufanya ulimwengu mpya; ni huu papa hapa. Yeye atauunguza tu moto, autakase, kama alivyokufanyia wewe. Mipango Yake haina budi kudumu milele. Sasa, angalia, itakuwa hivyo.

147 Kumbuka, haitakuwa ni Mbinguni. "Unashuka kutoka Mbinguni." Ni Mahali pa kukaa, Mahali pa kukaa, kuchukua makao Yake. Kama vile, ilikuwa ni Yohana, kwenye kisiwa cha Patimo, hapa katika Ufunuo 21, yeye aliuona "ukishuka." Yohana aliuona ule Mji, "ukishuka kutoka Mbinguni," kama hua, kama alivyoona.

Huyu hapa Mungu anakuja, kwenye maskani Yake ya duniani, Yesu, katika … "akishuka kutoka Mbinguni." Yesu alibatizwa, akaenda moja kwa moja …

Wakati alipokutana na nabii! "Neno humjia nabii." Naye alikuwa Neno. Naye nabii alikuwa amesimama pale, akikana madhehebu yao yote, kila kitu. Na, wakati alipoliona Neno, Neno lilimjia moja kwa moja.

Naye nabii alishtuka sana, akasema, "Ninahitaji kubatizwa na Wewe. Mbona unakuja kwangu?"

Yeye alisema, "Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo (tunajua ujumbe) kuitimiza haki yote. Mimi Ndimi ile Dhabihu; Haina budi kuoshwa." Akamkubalia.

148 Wakati alipotoka majini, alisema, "Niliona mbingu zimefunguka." Nabii aliona jambo hilo. Aliona mbingu zimefunguka.

Na hapa anakuja, akishuka kutoka Mbinguni, mfano wa Hua; na Sauti, ikisema, "Hii ndiyo sehemu Yangu ya dunia niliyoikomboa, na kutoka sehemu hii ya dunia nitakomboa sehemu iliyobaki, kwa kuwa Yeye ni Neno Langu lililodhihirishwa." "Na ulimwengu mzima, niliunena ukawepo kwa Neno Langu," Waebrania 11. "Na Shetani ameushikilia wakati huu wote, bali nimekuja kuukomboa. Kiasi fulani chake kimeufanya mwili Wake, nami ninakuja kukaa ndani yake."

149 Yohana alisema, "Nikaona ule Mji mtakatifu, Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni, kama Bibi - arusi aliyekwisha kupambwa kwa ajili ya Mumewe." Nao ulikaa wapi? Ni kama tu vile ilivyofanya pale; juu ya nchi.

Yesu alikuwa sehemu ya dunia hiyo ambayo Roho Mtakatifu alishuka juu yake, (hiyo ni kweli?) Na akakaa juu Yake milele. Kamwe hawezi kumwacha. Yeye daima yuko pale. Yeye na Mungu ni Mmoja. Daima hana budi kubaki!

Na kwa hiyo Yohana aliuona ule Mji mtakatifu, Yerusalemu Mpya, ukishuka kama kimondo, ama hu—hua, ukishuka kutoka Mbinguni na kukaa juu ya dunia nzima iliyokombolewa, (kufanya nini?) Kudai kila sifa ambazo Yeye alifanya dunia kwa ajili hiyo. Kila mtu aliyewakilishwa katika Umilele, na kila mwanamke, amekombolewa basi. Imesafishwa na kuchomwa kwa moto.

Yesu, katika majaribu Yake ya makali jangwani, kwa siku arobaini. Baada ya hayo, angalia, ilikuwa tayari kwa ajili ya huduma Yake wakati huo.

150 Wazia jambo hilo, Roho Mtakatifu akishuka juu ya nchi, Yesu, na hiyo Damu takatifu! Sasa angalia, nami natumaini sitaingia kwenye kilindi sana kwanu, mnaona. Damu takatifu ambayo iliumbwa na Mungu; ile Damu, Uzima, uumbaji wa Mungu. "Yesu alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Loo! Mnaona jambo hilo? Mungu, akifanywa katika uumbaji. Yeye alikuwa ni Roho. Biblia ilisema, "Yeye ni mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Yeye alianzaje? Katika tumbo la uzazi la mwanamke. Ambaye ni nini? Mwanamke si …

Kama vile vile hao vipofu wasivyoweza kuona "uzao" wa nyoka papa hapa. Mnaona? Hawa aliwekwa hapa duniani, na, kabla Shetani hajawahi kumgusa, ama cho chote kile, Mungu aliwaambia, "Zaeni mkaijaze nchi." Hiyo ni kweli, bali Shetani anaingia hapa. Na, kama huyo alikuwa ni mwana wa Adamu, basi wapi …

Adamu alitoka moja kwa moja kwa Mungu. Nawe unachukua tu tabia ya mzazi wako.

Na wakati unapozaliwa mara ya pili, unachukua Asili ya Mzazi wako, wa Mbinguni. Na Mzazi wako wa Mbinguni ni sifa ya Neno … Ama, Neno ni sifa ya Mzazi wako. Basi, unawezaje kulikana, kwa ajili ya madhehebu? Loo, jamani!

Natumaini hamtakosa jambo hili. Ninajua Limetoka kwa Mungu.

151 Yesu. Huyu hapa anakuja, akishuka; na kulikuwako na Yesu, ile sifa ya Mungu.

Sasa, "yule mwanamke," yeye. Angalia. Mungu alisema, "Kwa sababu walifanya jambo hili," kasema, "Nitaweka uadui kati ya Uzao wako na uzao wa nyoka." Hiyo ni kweli? Na mwanamke huyo hana mbegu yo yote. Je! Ulipata kuwazia jambo hilo? Yeye ana shamba, si mbegu. Unaona, nyoka alikuwa tayari ameweka "uzao" wake hapo.

Basi, kama mwanamke hana mbegu, hana budi angojee kusudi apate Mbegu.

152 Mnaona, kupitia kwa kujuana kimwili hapa, alikuwa amemleta kutoka kwa Shetani, yule nyoka, ambaye hakuwa kiumbe kitambaacho; alikuwa na miguu, maana miguu yake iliondolewa kwake. Yeye alikuwa ndiye mwerevu sana, mnyama pekee ambaye ange—angeshirikiana na mwanamke.

Mbegu ya mnyama haitafanya jambo hilo sasa, wala cho chote kile. Wamejaribu. Haiwezekani. Mnaona, mbegu ya uhai kutoka kwa dume la mnyama fulani hautaingia katika mwanamke. Haitafanya hivyo.

153 Lakini hicho kilikuwa ndicho kitu cha karibu sana. Mnaona, hawawezi kupata kiumbe hicho kati ya sokwe mtu na mwanadamu. Mnaona, kila kimoja, kilipokuwa kikipanda kwenda juu, kutoka kwa ndege, na

kuendelea juu hadi kufikia tumbili, na kadhalika, hadi sokwe-mtu, basi kuna "kilichopotea." Hicho kilikuwa ni nyoka, si nyoka wa kawaida; kila umbo limepotea kwake, kwa sababu alilaaniwa.

Sasa, Mungu hakumlaani Adamu; huenda angefanya jambo lile lile, bali Yeye aliilaani dunia, "miiba na michongoma."

Yeye hakumlaani Hawa, bali alisema Adamu angekuwa "mtawala" wake. Tangu sasa na kuendelea, yeye hajaribu kuhubiri lo lote wala cho chote kile, Adamu ndiye mtawala wake. "Na siku zote za maisha yako, na katika huzuni, nawe utaleta … uhai wako duniani." Lakini Yeye alisema, "Nitaweka uadui kati ya Uzao wako …"

Sasa, yeye hakuwa na mbegu yo yote, kamwe hajawahi kuwa nayo, kwa hiyo, ilimbidi kupokea Mzao kwa njia fulani. Mungu alimpa Mzao, si kwa kujuana kimwili, bali kwa uumbaji.

Hivi ninyi vipofu hamwezi kuona huo ndio "uzao" wa nyoka? Loo, jamani! Shetani alifika pale kabla ya Adamu; huo ulikuwa ndio ule "uzao."

Lakini mwanamke alipokea Uzao. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu Mwenyewe. "Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu."

154 Sasa angalia wakati Sethi alipozaliwa, ama Habili, alikuwa mtu mwenye haki, kutoka kwa baba yake. Sethi ni vivyo hivyo.

Yule jamaa mwovu alitoka wapi; muuaji, mwongo? Mnaona, mnaona mahali alipotoka? Ilibidi iwe "uzao," kwa sababu yeye alikuwa ni mzao; Kaini alikuwa mtu.

Loo, hao watu vipofu wako wapi? "Mungu wa ulimwengu huu amewapofusha." Vema, si ajabu, Yesu alisema hakuna mtu anayeweza kuliona jambo hilo. Mnaona?

Unasema, "Kwa nini wao hawalioni?"

Yesu alisema wakati mmoja, kwa mwanafunzi Wake, "Mmejaliwa kuujua Ufalme wa Mungu, bali kwao sivyo."

155 Na hiyo ndiyo sababu mnatoka kutoka kwenye maili elfu moja na mia tano mraba, mnaona, "Umejaliwa kuujua Ufalme." Angalieni, jamaa wanakuja hata kutoka Afrika Kusini na kila mahali, wakati huu wa kuchelewa wakati Bibi -arusi ameandaliwa kwenda katika Ufalme.

Sina tu wakati wa kutosha. Angalia. Angalia sasa, mnaona.

Sasa mnaweza kuona "uzao" wa nyoka pale, mnaona jinsi alivyofanya jambo hilo? Ni kamilifu, mnaona. Sasa baadhi yao walisema …

Sasa, kama yule jamaa huko Tucson hivi majuzi, akijaribu … Aha, huenda akasikiliza kanda hii. Lakini, kama ndivyo ilivyo, ewe mtu, nataka kukwambia jambo fulani.

Wakati aliposema, "Hawa alisema," hapa ndipo wanapoelekea, "'Nimepata mwana kutoka kwa Bwana, ama mtu kutoka kwa Bwana.'" Mbona, bila shaka. Mungu ana sheria.

156 Tazama, hebe chukua mbegu na uipande nje hapa kwenye shamba ambalo kuna ngano, nawe upande michongoma huko nje. Sijali, jua lile lile na mvua ile ile hufanya mbegu hiyo iote. Mungu ana sheria, na sheria hiyo haiwezi kuvunjwa.

Sijali kama ninii—kama ninii … mwanamke aliye mchafu sana mjini na mwanamume aliye mchana sana, na hawajafunga ndoa na kila kitu, angekuwa na—na uhusiano wa kimapenzi, na kuishi pamoja na kumzaa mtoto; mtoto huyo angepaswa kuja kwa sheria ya Mungu, maana hakuna njia nyingine. Usipofanya hivyo, unamfanya Shetani kuwa muumba, halafu yeye ni mungu. Loo, namna unavyoweza kuwa kipofu! Mnaona, sheria ya Mungu, hakika.

Kama uliwahi kupata mtoto mchanga, sijali kama alikuwa ni Esau, Yakobo, ye yote yule, ama mtu yeyote mwenye sifa mbaya, kama alikuwa Yuda, ilimpasa aje kwa njia ya Mungu. Mungu ana sheria.

157 Biblia ilisema, "Jua huwaangazia wenye haki na wasio haki; mvua huwanyeshea wenye haki na … " Waebrania sura ya 6, na inasema ya kwamba, "M—mvua huinyeshea nchi mara kwa mara, kuinywesha, na kuitayarisha kwa kile inacholimiwa, mwajua, hushiriki baraka; bali miiba na michongoma huishi kwa maji yale yale, jua lile lile." Kwa kuwa, ni sheria ya Mungu, kuivisha kila mbegu, kuifanya kila mbegu ijizae yenyewe.

Kwa hiyo, ilibidi itoe "uzao" wa nyoka. Na hilo kamwe ha—halikumzuia Mungu kamwe; lilitimiza mpango Wake mkamilifu, lilimfanya Yeye Mkombozi. Kipofu ye yote anapaswa karibu aone jambo hilo, isipokuwa limefichwa. "Mungu wa ulimwengu huu" amewaficha. Ni dhahiri tu kama cho chote unachoweza

kuona. Hivyo ndivyo ilivyo. Huo hapo "uzao" wako wa nyoka. Sasa angalia.

Lakini, "Yesu alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu."

158 Sasa mwanamke anafanya nini? Wakati, chembechembe ya uhai inapotoka kwa mwanaume. Sasa kanusha hilo? Mwanamke huyo hana uhai ndani yake, hata kidogo. Yeye ana yai dogo tu, ambalo ni shamba nje hapa.

Kama vile ulivyochukua shamba na kulilima lote, na—na kulinyunyizia dawa ya wadudu, na kunyunyizia vijidudu vyote kutoka kwake. Wala si—hata nyasi wala cho chote kingeweza kukua ndani yake; halafu unarutubisha tena, unapanda mbegu nzuri mle ndani. Kama adui akija na kupanda mbegu nyingine, sheria ile ile ya Mungu itaivisha mbegu zote mbili.

Vema, Mungu hakukusudia hilo liwe, mnaona. Lakini ni jambo gani lililotukia?

159 Mnaona, mbegu kutoka kwa mwanamume hubeba hemoglobini, ambayo ni damu. Katika damu mna uhai. Na kama ukiwahi … Nimeiangalia, katika kuwazalisha ng'ombe na kadhalika. Mimi na Ndugu Shakarian tumepita kwenye jambo hilo, na madaktari na kadhalika, tukiangalia namna hizo zinavyoingia, wale wakemia. Mnaona? Halafu hapa zinakuja mbegu kutoka kwa jike, ambazo ni kundi la mayai. Hizi hapa zinakuja mbegu kutoka kwa mwanamume, ambazo ni kundi la chembechembe za uhai.

Huyu hana chembechembe za uhai hata kidogo ndani yake. Ni kitu tu kichotolewa kwa mwanamume. Hivyo ndivyo mwanamke alivypata kuwa hapa, kwanza, naye ni shamba tu. Kuna yai; lina ardhi yenye rutuba kwa ajili ya maisha haya. Na uhai huu unaingia na kutambaa. Hiyo hapo siri, namna ambavyo …

160 "Labda," unasema, "vema, ya kwanza inakutana. Hizo zingine zinakufa." Vema, vipi, ni nani anayeamua jambo hilo? "Vema, ya kwanza." Je, itakuwa ni ile iliyo mbele; yai la kwanza lililoko mbele, na chembechembe ya uhai ya kwanza? La, la.

Huenda ikawa ni yai moja; kule moja nyuma kabisa, kule nyuma, katikati ya hizo mbegu za kiume, itatokea chembechembe ya uhai iende ikutane nalo. Inaonyesha ya kwamba akili fulani huamua kama atakuwa na nywele nyekundu, nywele nyeusi; kama atakuwa mdogo, mkubwa; wa kiume ama wa kike. Mnaona? Huwezi, huwezi kufanya jambo lingine kulihusu; halitafaa kitu. Unaweza kuyachanganya pamoja, na kila kitu, haitaleta tofauti yoyote. Mungu huamua jambo hilo. Na baada ya kitambo kidogo, chembechembe ya uhai moja ndogo itatambaa na kuingia kwenye shamba hilo, yai. Ni kitu gani kilicho na mkia mdogo, kitu kama hicho, juu yake, ikijitikisa-tikisa; inaanguka, na hapo unaanza mgongo wa mtoto mchanga.

161 Yeye mwanamke ni nini basi? Yeye hana mbegu. Yeye ana shamba la kupokea mbegu. Kwa hiyo ninii …

Mnaona, adui aliyetoka kwenda. Wakati mpanzi mwemai alipotoka kwenda, akaipanda Mbegu njema; na adui akaja nyuma yake, akaipanda mbegu potovu. "Lakini mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki; jua." Zote hazina budi kukua.

Yesu alisema, "Ziacheni zikue pamoja. Siku ile yatakusanywa yafungwe matita-matita, yale magugu." Na yanakusanyika sasa, katika madhehebu makubwa; yakielekea kwenye lile tita kubwa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na mwisho ulikuwa nini? Ni kuteketezwa. Lakini nafaka itawekwa ghalani. Mnaona? Ambapo, zote mbili zinaishi kwa kitu kile kile, maji yale yale, mvua ile ile.

162 Mti jamii ya mchungwa, ambao ni—huo ni mchungwa, utazaa, itabidi uzae; utazaa juu yake, kama umepandikizwa, komamanga. Utazaa limau. Utazaa balungi. Mnaona? Lakini halitakuwa ni chungwa, bali linaishi kwa uhai ule ule ambao unatolewa na mti wa chungwa.

Madhehebu yameingizwa kwenye Mzabibu. Kwa sababu, kama wanadai "Wakristo," wanaishi kwa jambo hilo. Kayafa alikuwa; mnajua kile alichokuwa, na hata hivyo yeye alitabiri. Mnaona? Mnaona, wanaishi kwa jambo hilo.

Loo! laiti ningalikuwa na juma moja, ambapo tungejifunza jambo hilo lote, na kulifanya wazi sana ha—hamwezi mkakosa kuliona. Sasa nitaacha baadhi ya mambo haya.

163 Sasa angalia. Angalieni, mikono hiyo iliubuni jambo huu kwa ajili ya Bibi -arusi Wake Mpendwa, ikaubuni kwa upendo mwema kwa Bibi -arusi Wake.

Kumbukeni ya kwamba Roho Mtakatifu alishuka juu ya Yesu, ambapo, Yesu alikuwa ni sehemu ya dunia. Kwa nini? Chembechembe ya uhai ya Mungu, Uzima wa Mungu, ulibuniwa katika tumbo la uzazi la mwanamke (hiyo ni kweli?), ambalo lilikuwa ni dunia. Vema. Na ndipo Uzima wa Mungu ukaingia, kwa hiyo, "Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Mnaona? Na halafu hiyo Damu ya Mungu, iliyokuwepo pale kwa hiyo chembechembe hai; wakati ilipomwagika pale Kalvari, ikadondoka juu ya nchi. Kwa nini? Kuikomboa dunia. Sasa, imehesabiwa haki; imetakaswa; ikaitwa, na kudaiwa; na sasa itapokea ubatizo

wa Moto, na kusafishwa kwa ajili ya Yesu na Bibi -arusi Wake.

Nawe ndiwe sehemu hizi zingine ambazo zilizotolewa kutoka kwenye dunia hii. Dunia, wewe ni sehemu ya dunia; mwili wako. Nafsi yako ni sehemu ya Mungu, sifa ya Mungu, iliyoonyeshwa hapa duniani katika mwili. Mwili unapaswa kukombolewa.

Sasa, nafsi imekombolewa, kwa sababu ilikuwa katika dhambi. Kwa hiyo Mungu akashuka, kwa utaratibu wa kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na akaikomboa nafsi yako.

164 Nawe, ukiwa sehemu ya dunia, umekombolewa nayo. Uko katika mchakato sasa. Inaendelea kukua. Mwili wako ulihesabiwa haki chini ya ubatizo wa Nuhu. Amina! Na, mwili wako, wakati uliposhuka juu pale. Na dunia itasafishwa kwa Moto, mahali ambapo utaishi, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu; Makao ya Kristo na Bibi -arusi Wake, Yerusalemu Mpya.

165 Angalia mji huu; dunia, utakaa duniani. Sasa unaweza kuona dhahiri kama nilivyosema, ninii … badiliko hili, dunia haina budi kubadilishwa. Haiwezi kuwa nayo namna hii. Kanisa halingeweza kwenda … Ama, ulimwengu usingeweza kuendelea moja kwa moja, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, bila kubadilishwa. Mnaona? Kuwa na Mahali kama hapo ndani yake, itabidi ubadilishwe.

Ni kama tu, hatuna budi kubadilishwa na Moto Wake mtakatifu, kusudi tutayarishe na kuandaa mahali Yeye anapoweza kuishi ndani yetu; hiyo ni kusema, Roho Mtakatifu.

166 Angalia sasa, kutakuwa na nafasi tele katika Nchi Mpya. A-ha. Mnaona, nafasi tele! Itafanywa upya, hiyo ni kweli, kwa Moto, bali hakutakuwako na bahari tena. Angalia, ule Mji una maili elfu moja na mia tano mraba.

Sasa sikilizeni kwa makini sana tunapochora vipimo hivi. Ninataka kufuta ubao, kwa muda kidogo tu. [Ndugu Branham anafuta mifano yake ya awali — Mh.]

Huu hapa ufunuo wa kina kutoka kwa Mungu. Hapa, nitasimama hapa tu. Hakuna moja ya haya mengine … Nitaleta haya mengine, Bwana akipenda.

167 Angalia sasa dunia ni … Vema, hebu fungueni Kitabu cha Ufunuo, mnaweza kuona jinsi alivyoupima kwa dhiraa na kwa maili. Elfu mbili na mia tatu… Kwa hiyo sasa tunaona ya kwamba ule—ule Mji umepimwa, "maili elfu moja na mia tano" mraba.

Mnajua hilo lingefikia umbali gani? Niliupima, juma hili. Ingefikia kutoka Maine hadi Florida, na kutoka bahari ya mashariki hadi maili mia sita huko nyuma, magharibi ya Mississippi. Kwa maneno mengine, nusu ya Marekani, kwa ajili tu ya Mji huo.

Mnasema, "Hakuna nafasi."

168 Wakati bahari itakapoondoka kutakuwako na nafasi, maana karibu nne ya tano yake iko kwenye maji. Hiyo ni kweli? Mlipuko huo hukausha bahari, hulipua dunia. Loo, jamani! Kumbukeni, maili elfu moja na mia tano mraba, ni Mji ulioje! Na, lakini, kumbukeni, bahari imeondoka.

"Na upana na urefu ni sawa." Hilo lingefanya maili elfu moja na mia tano upande huu, maili elfu moja na mia tano upande ule; maili elfu moja na mia tano; marefu kwa mapana na kwa kimo. Maili elfu moja na mia tano, wazia jambo hilo, dhahabu safi sana. Na ule Mji ulikuwa na ukuta kuuzunguka.

169 Sasa, sasa, hiyo haimaanishi, kwa kuwa sawa … Ilisema, "Na zile kuta zilikuwa sawa sawa na msingi msingi wake," hilo halimaanishi kwamba ni mchemraba au mraba. Kuna kipimo kingine cha kijiografia, kwamba vipimo ni vile vile, hicho ni, piramidi. Mraba, "ni wa mraba," na kuta zilikuwa sawa sawa.

170 Hebu niuchore. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao — Mh.] Tazama: urefu, upana, kimo. Tutaingilia jambo fulani, hakika kabisa. Mnaona? Angalia, vipimo vya kona hii ni sawa kabisa, vyote, urefu kwa—kwa kimo. Kuna kipimo kingine, piramidi, ambacho kinathibitisha jambo hilo.

Hii, ikiwa hivi, lingejibu hasa ishara ya Henoko kule Misri, ile piramidi. Sivyo? Henoko, kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, wakati kuhesabiwa haki kulipokuwa kunakuja, yeye alitoa ishara, na katika piramidi hii kuna hatua saba zinazoelekea kwenye chumba cha mfalme. Angalia kwenye ile hatua ya saba, kama uliwahi kuchunguza vipimo vya piramidi, nani anayekuja kumlaki mja, kumtambulisha kwa mfalme. Angalia ni kituo cha nani kinachosimama pale, nawe utaona siku unayoishi, katika piramidi.

171 Sasa, Mungu alifanya Biblia tatu. Sasa, kuna fundisho la piramidi ambalo ni upuuzi, bali kuna piramidi halisi. Mnaona? Angalia. Sasa, Mungu, Biblia ya kwanza … Yeye alifanya tatu. Lazima kuwe na kila kitu katika tatu.

Yesu anakuja mara tatu. Kuja, mara moja, kumkomboa Bibi -arusi Wake; mara ya pili, kumchukua Bibi -arusi Wake; mara nyingine, pamoja na Bibi -arusi Wake. Mnaona?

172 Sasa angalia jinsi linavyopendeza. Mnaona? Na katika piramidi hii kulikuwa na hatua saba, na halafu chumba cha mfalme. Nasi tuko katika wakati wa saba wa kanisa, kabla Mfalme hajachukua Kiti Chake cha Enzi. Na, kumbukeni, piramidi kamwe haikuwa na jiwe juu yake.

173 Biblia ya kwanza ya Mungu ilikuwa angani, Zodiaka; inaanza na kupitia katika kila wakati. Wa kwanza, mwanzo wa Zodiaka, ni bikira; hivyo ndivyo Yeye alivyokuja, kwanza. Umbo la mwisho katika Zodiaka ni Leo yule simba; kule Kuja kwa pili. Kabla tu hakujakuwako na wale samaki waliokingamana, ambao ni wakati wa kansa; tunaishi sasa.

Kulikuwako na piramidi baada ya jambo hilo, Henoko, ambalo lilishuhudia sawa sawa kabisa. Tusingekuwa na wakati wa kuingia katika jambo hilo, lakini, siku moja, kwa msaada wa Mungu, nitawaonyesha, inachora sawa sawa kabisa vipimo vya wakati tunayoishi. Mnaona?

Angalia, lakini kipimo hiki cha kijiografia tulicho nacho sasa, ambacho vipimo vyake ni sawa, haimaanishi kwamba lazima kiwe ni m—mchemraba. Angalia, hii ingejibu nini ya Misri … ama ile ishara ya Henoko huko Misri.

174 Katika wakati wa kutakaswa duniani, kwa ubatizo wake wa Moto, kutakuwako na nini ya kivolkeno, kitu kama kulipuka kwa dunia hii, na itasukuma kitu kama Mlima unaofanana na piramidi. Mnaona? Nafasi ya kutosha kufanya jambo hilo! Jambo hili lote litabadilishwa. Uso wote utabadilishwa. Mmelipata? Itasukuma juu Mlima kama piramidi.

175 Hii hasa ingeambatana na Neno kama ikifanya hivyo, ambalo itafanya hivyo. Sasa angalia, kwa kuwa, katika Isaya 65:25, ambapo tumesoma tu, Yeye alisema.

> *Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu, asema BWANA.*

Loo! "Mlima Wangu wote mtakatifu!" Kumbuka, daima ni "Mlima."

Kama kuta zingekuwa zimenyoka juu na chini, Mji huo ungeweza kuonekana tu kutoka nje … ama kutoka ndani, Kiti cha Enzi kinaweza tu kuonekana kutoka ndani; lakini angalia ingeonekana tu kutoka ndani.

Lakini sasa tunaona ahadi ya Isaya 4:5. Hebu na tulisome tu.

176 Mna haraka? [Kusanyiko linasema, "La." - Mh.] La, msiwe na haraka sasa. Sisi—sisi—tunaelekea—tunaelekea kwenye jambo fulani maalum sasa, wakati mwingi—wakati mwingi—mwingi sana ambapo hamna budi kuelewa sasa papa hapa. Maana, ninataka kuweka jambo hili wazi. Halafu basi tutakapolirudia tena, nita—nitawaonyesha basi mahali tulipo—mahali tunapozungumzia, ni nini, katika somo letu linalofuata juu ya jambo hili, wakati mwingine.

177 Loo, Bwana Yesu asifiwe! Angalia hapa, jinsi Maneno yasivyoweza kushindwa. Sasa angalia hapa katika Isaya. Nimeliandika hapa, kama ninaweza kulipata tena, kwa dakika moja tu. Isaya 4:5. Sasa sikilizeni, yeye anazungumza juu ya Kuja kwa Bwana, jinsi ambavyo wanawake wangekuwa waovu sana. Loo, yeye alisema, "Wanawake saba …" Sikilizeni. Hebu na tulisome tu. Angalia hapa.

> *Na siku hiyo wanawake saba watamshika mwanamume mmoja, wakisema, Tutakula chakula chetu wenyewe, … kuvaa nguo zetu; lakini tuitwe tu kwa jina lako, utuondolee aibu yetu.*

Huo ndio wakati wa mwisho, ambapo tunaishi sasa; ndoa, talaka, na ukahaba, na chochote kile.

> *Siku hiyo chipukizi la BWANA litakuwa zuri, lenye utukufu,…matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza…ajili ya Waisraeli…waliookoka. (Jinsi mlivyookoka hukumu hiyo yote! Mnaona?)*

> *Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye ambaye ameachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa…(hebu tuone)…ndani ya Yerusalemu ataitwa mtakatifu; yaani kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu, mnaona:*

> *Ambapo Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao binti wa Sayuni (kumbukeni, huyo daima ni Bibi-arusi, mnaona)…na atakuwa ameisafisha damu ya Yerusalemu (hao ni Wayahudi waliosalia, pamoja na Bibi-arusi, mnaona)…na kati yake, pamoja na roho ya hukumu, moto…*

Hiyo daima ni hukumu ya Mungu, wakati anapofanya hukumu Yake ya mwisho. Anakuita, anakuhesabia haki, na anakuleta kwenye ukombozi; ndipo hukumu Yake inakushukia, na Roho Mtakatifu na Moto husafisha dhambi. Ndipo wewe ni Wake.

Jambo lile lile analoifanyia dunia, wakati anapoisafisha kwa Moto, "na kwa roho wa kuungua." Sasa angalia. Sikilizeni! Uko tayari?

*Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya kusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa…moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa Sitara.*

178 [Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao — Mh.] "Bwana, katika siku hiyo, juu yake, ataumba Moto wa Nuru uangaze wakati wa mchana." Na inaendelea na kusema, "Itakuwa mahali pa kukimbilia, mahali pa kustarehe, mahali pa kujificha." Angalia, kufanya hasa yale Biblia inenayo, sawa kabisa Kuta hizo zilikuwa zimenyoka moja kwa moja juu na chini, usingeweza kuziona. Haina budi kuegemea upande. "Mlima Wangu wote mtakatifu …" "Yeye ataumba Nuru hii juu ya Mlima huu, na itakuwa ni kwa ajili ya ulinzi." Loo, tunaimba wimbo huo:

Loo, huo Mji juu ya Mlima Sayuni,
Kama msafiri, hata hivyo ninaupenda bado;
Sasa na katika nyakati hizo,
Nitakapofika kwenye Mji ule ulio Kilimani. Mnaona?

179 Angalia, Mlima Sinai ndipo Mungu aliposhuka juu yake, wakati aliponena na Israeli katika Nguzo ya Moto. Alishuka juu ya mlima, Mlima Sinai.

Kwenye Mlima wa Kugeuzwa, wakati Yeye alipotangaza, "Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye," alishuka katika Nguzo ya Moto na mwanga mkuu, juu ya kilele cha mlima, mbele ya Petro, Yakobo, na Yohana. Na, mle ndani, Yeye aliwakilishwa pamoja na Musa na Eliya pia; walionyakuliwa, na wafu waliofufuliwa. Utukufu!

180 Mji Mpya na Nchi Mpya; uumbaji mpya; ule Mji ulio Kilimani, pamoja na Kiti cha Enzi juu yake. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao, kwa ajili ya aya chache zifuatazo — Mh.] Kile Kiti cha Enzi hapa juu, kwenye kilele; na wakazi, kote juu na chini, kwenye Mlima huu.

Na ukuta uliozunguka huu, ulikuwa na misingi kumi na miwili. Na kila mmoja wao alikuwa na jiwe la kifua lililokuwa na Haruni, ambalo liliwakilisha makabila kumi na mawili ya Israeli.

Na, kwenye malango, walikuwa na malango manne yaliyowekwa sawa kabisa na hekalu kule jangwani, kama vile hema lilivyokuwa jangwani. Angalia kila mmoja, ulikuwa—ulikuwa na mitume, watatu kila upande, mitume kumi na wawili. Kila … Na ulikuwa na urefu wa dhiraa mia na arobaini na nne. Dhiraa mia na arobaini na nne ni kulingana kabisa na futi mia mbili na kumi na sita, zikifanya urefu wa kila moja ya mawe hayo makubwa karibu futi ishirini urefu wa kwenda juu, ile dirii kwenye lango lile, zikifanyiza ukuta huo uliouzunguka ule Mji.

181 Sasa huo, ule Mji, haukai juu ya ukuta, maana mji, maili elfu moja na mia tano, usingeweza kufanya hivyo. Ni ukuta hapa unapoingia, kama milango ya Yerusalemu ya kale. Uliingia kupitia ukutani, ukaingia humo.

Na kila mmoja wa hizi, ulikuwa na misingi kumi na miwili, na kila mmoja ulikuwa na zumaradi na mawe mbalimbali, ambayo yaliwakilisha makabila kumi na mawili ya Israeli.

Nao mitume, kila mmoja, juu ya lango hilo kubwa, la lulu tupu, waliweka jina la mtume mmoja. Na je! Yesu hakusema, "Mtaketi kwenye viti kumi na viwili vya enzi, mkiyahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli"? Ni nani aliyeketi langoni, kuhukumu, wanapoingia Mjini? Loo, jamani! Hivyo ndivyo walivyo. Wafalme wa duniani wakiingia katika ule Mji, wakiingia mbele ya hakimu wa kimitume, kama Yesu alivyoahidi. Loo, jamani!

182 Juu ya Kiti hiki cha Enzi, juu yake, maili elfu moja na mia tano kwenda juu, ulimwengu wote utaona Nuru ya ulimwengu, Yesu, ameketi kwenye Kiti cha Enzi juu ya ulimwengu, juu ya Kanisa, juu ya Mlima Sayuni; ambayo ni maili elfu moja na mia tano, nusu ya ukubwa wa Marekani, na unainuka moja kwa moja mpaka unaweza kumwona Yeye kote ulimwenguni, maili elfu moja na mia tano kwenda juu.

183 Na pote juu-na-chini hapa, watakuwako Waliokombolewa. Kutakuwako na nyumba za dhahabu safi. Kutakuwako na barabara kuu, na bustani kubwa, na bustani. Nao ule Mto wa Uzima ukija, ukitiririka kutoka kwenye kile Kiti cha Enzi, na ukitiririka kupitia kwenye magongo madogo na, loo, juu ya matuta. Na Mti wa Uzima utakuwa ukichanua katika kila uwanja; na kuzaa matunda Yake, mara kumi na mbili kwa mwaka, tunda tofauti kila mwezi.

Na wafalme wa dunia wataingia humo na kuletea heshima zao. "Na hayo majani ni kwa ajili ya kuyaponya mataifa," wakati wafalme watakuwa wanaishi kwa amani huko nje. Wanapotoka, watachuma mti, jani namna hiyo. Kama vile yule hua alivyorudi, ya kwamba hasira ya Mungu ilikuwa imetulizwa, naye akalileta lile jani la mtini ndani ya safina. Kwa hiyo wakati mfalme huyo anapoondoka, akileta utukufu wake kwenye chumba cha Bibi-arusi hapa kwenye ule Mji, yeye atamwinulia jani jirani yake mfalme, na, "Sisi tuna amani milele." Amina! Kuwaponya mataifa! "Yote yamekwisha. Wakati mmoja tulipigania damu za mmoja kwa mwingine, ndugu. Nasi tumefurahia, na kupiga makelele; na kutupiana risasi, na kuwachoma moto watoto, kila kitu. Lakini sasa kuna amani, uponyaji." Si kuponya magonjwa; yote

yamekwisha. Kuwaponywa taifa! Amina!

184 Mji wenye Kiti cha Enzi juu. Ufunuo 21:23, "Nao hawahitaji taa, kwa maana Mwana-Kondoo na Bwana Mungu ndiye Nuru yake." Mnaona? Bwana Mungu ndiye ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli jangwani. Naye amepanda kwenye Kiti cha Enzi, katika ule Ufalme mkamilifu…ambapo wakati…"Ule Ufalme ambao Yesu atautoa kwa Baba, ili Mungu apate kuwa yote, na katika yote. Yesu anaketi juu ya Kiti Chake cha Enzi hapa, kama Yusufu wetu. Naye Mfalme ndiye ile Nuru itakayokuwa juu ya Mlima Sayuni, na Nuru Yake takatifu itaufurikia Mji mzima. Haleluya!

185 Maili elfu na mia tano kwenda juu, na maili elfu na mia tano mraba, pamoja na paradiso za Mungu zimejengwa kote katika Mji huo; mitaa, barabara kuu! Soma Ufunuo 21 wako, uone kama si sawa. Mnaona, "Hawahitaji nuru pale, kwa maana Mwana -Kondoo ndiye ile Nuru." Na kwenye kile Kiti cha Enzi anaweza kuonekana, ameketi, maili elfu moja na mia tano.

Hauendi juu moja kwa moja namna hii. Unaondoka, kama piramidi. Unalala upande, kama piramidi. Kama ungekuwa ni nusu ya huo urefu, basi hiyo ingeenda juu namna hii, mnaona, kutoka mji mmoja hadi mwingine…sasa kama ukitazama, kutoka kwenye upande mmoja wa Mji hadi mwingine.

186 Ningeingiza kitu kidogo hapa kama mnataka nifanye hivyo. Je! Mliona lile kundi dogo hapa? Ni kama tu sehemu hiyo, ukubwa wa mzunguko wa eneo lake. Georgia, California, mpaka Saskatchewan; kutoka Kansas, mpaka kwenye pwani ya miamba ya Maine; hizo ndizo zilizokusanyika. Hiyo ni kuhusu kile kinachowakilishwa papa hapa, kama maili elfu moja na mia tano mraba.

Loo, wanatoka Mashariki na Magharibi,
Walitoka nchi ya mbali;
Kufanya karamu pamoja na Mfalme wetu; kula (Vipi? "Mtu hataishi kwa mkate tu."
Kwa Mkate, Neno!) … kula kama wageni Wake;
Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!

Ulimwenguni, sina budi kusema, sijawahi kuona watu kama hao.

Loo, wanautazama uso Wake mtakatifu
Unaometameta kwa Nuru ya Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watang'aa kama vito kwenye taji Yake.
Loo, Yesu yuaja hivi karibuni,
Shida zetu zitakwisha wakati huo.
Loo, vipi kama Bwana wetu akija wakati huu?

187 Haitachukua muda mrefu. Kila kitu ni kikamilifu. Kijiografia, Sodoma, wale wajumbe; kila kitu kimekaa sawa kabisa. Mnaona? Inamaanisha nini? Waziani tu, wakija kwenye maskani hii moja ndogo, maili elfu moja na mia tano mraba, kutoka kwenye eneo lile lile.

Ni kwa nini Mungu aliwazia sana na kupajali sana mahali pale padogo pa Palestina, mnaona, pakiwa tu mahali padogo sana? Lakini pale pale ndani lile hekalu limewekwa. Hapo ndipo Yerusalemu Mpya itakapotokea, papo hapo. "Mzeituni, Mlima wa Mzeituni utapasuka, sehemu moja iende kulia na kushoto," hakika, utakaposukumwa kutoka chini. Siyo, wao wanavyosema, ni unasukuma na kuachana namna hii. Ni kusukuma juu, "Katika siku ile atakapoiweka miguu Yake mitakatifu juu ya Mlima." Angalia, kwenye Kiti Chake cha Enzi, maili elfu na mia tano kwenda juu!

188 Kumbukeni, Shetani alijitahidi kumjaribu, wakati mmoja, juu ya mlima. Mnaona?

Ule Mji Mpya una misingi kumi na miwili, kama tulivyopitia, wale wazee kumi na wawili; dhiraa mia na arobaini na nne; zikiwa ni ile dirii ya Haruni; milango kumi na miwili ya lulu, majina kumi na mawili ya wanafunzi.

Yesu atasimama, lile Jiwe la Kichwani, kwenye Kiti cha Enzi, wakati watakatifu Wake wamekwisha kumvika taji, "Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana." Naye ndiye lile Jiwe la Kichwani.

189 Sina kitabu changu cha mfukoni. Lakini kama utaangalia katika kitabu chako cha mfukoni, kama una noti ya dola moja, wana muhuri ya Marekani; tai upande mmoja, ameshika mikuki, kama nembo; na mwisho wa upande wake wa pili, ina piramidi, pamoja na jicho lionalo kila mahali juu yake. Unaona, wao hawakujua walichokuwa wakifanya. Na pale juu imeandikwa Kilatini, nawe utaona inasema, huu ni "ule muhuri mkuu." Wao hawakujua walichokuwa wakifanya. Wala Kayafa hakujua alikuwa akitabiri.

[Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao — Mh.] Huo hapo ule Muhuri Mkuu. Huu hapa, unaona, ule Mji. Si kwamba ni mchemraba tambarare kama huu, mnaona, bali huegemea ili uweze kuonekana. Na juu ya Mlima huu mtakatifu wa Bwana, Bwana atashuka juu ya Mlima Wake; Huyu hapa. Hiyo ndiyo sababu lile jiwe la kufunika halikuwekwa na Henoko. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu Jiwe la Kifuniko halina budi kuja sasa. Nao Mlima huo utasukumwa juu, nao utakuwa ni Mlima wa Bwana.

190 Na hapa ndani watakaa Waliokombolewa. Hii, mitaa mikubwa yenye miti na barabara kuu, basi, mashamba mazuri ya kutembelea, na Mto wa Uzima utabubujika, upitie moja kwa moja mle. Na kila nyumba itatengenezwa kwa dhahabu safi. Na barabara zitatengenezwa kwa dhahabu. Na miti ya Uzima itakuwa pale, nayo itazaa aina kumi na mbili za matunda. Na wafalme, na watu wenye heshima wa dunia, wataileta heshima yao na utukufu malangoni. Wala malango hayatafungwa usiku, kwa maana hakuna usiku huko.

Katika Mji ule ambamo Mwana -Kondoo ndiye Nuru,
Katika Mji ule ambako hakuna usiku;
Nina jumba kubwa kule, ambalo halina taabu wala mashaka,
Loo, ninaenda mahali ambako huyo Mwana -Kondoo ndiye Nuru.

191 Hivi huoni ya kwamba miji, majiji, majumba, makazi, yana—yananena habari zake sasa hivi? Mambo haya yote ya kawaida ni kivuli.

Chukua kivuli, kwa mbali, kama mkono wangu. Kabla hakujakuweko na—na kitu halisi … ama negativu, hapana budi kuwe na kitu halisi. Na, unaona, kivuli hicho, inaonekana kama kwamba nina vidole dazani, lakini basi unapoanza kuvileta pamoja, vinaonekana vizuri kama kimoja, ndipo hicho kivuli kinaishia kwenye mkono.

Na hivyo ndivyo, mara nyingi, watu wanafikiri kuna Miungu watatu au wanne. Unaangalia kule nyuma sana katika yale matengenezo ya mwanzoni. Mnaona? Shuka chini sasa na, unaona, uangalie vizuri sana mpaka uone Mmoja. Hiyo ni kweli kabisa.

192 Kuna Bibi -arusi mmoja; si dazani moja, madhehebu. Bali Bibi-arusi mmoja, huyo ni yule aliyeteuliwa, kutoka kwenye kila… kutoka kwenye—kutoka kwenye dunia ambaye amechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya jambo hili, wale wanaoweza kutambua mahali pao katika ule Ufalme.

193 Juu ya Kiti hiki cha Enzi, angalia, juu sana! Kwenye Kiti hiki cha Enzi, angalia, juu sana! Ule Mji Mpya; wenye misingi; milango kumi na miwili; Yesu, Jiwe la Kichwani; mitume, wakihukumu; makabila kumi na mawili.

Piramidi ya Henoko haitoi kivuli wakati wo wote wa siku. Nimekuwa huko Misri, kwenye mapiramidi. Imewekwa kijiografia kabisa, na kwenye vipimo vya umbo hili kuu la kijiometri; ambapo, hata jua liwe upande gani, hakuna kamwe kivuli kando ya piramidi. Mnaona jinsi ilivyo?

Na hakutakuwa na usiku huko kamwe. Yeye juu ya Mlima, anaujaza kwa utukufu Wake. Nuru Yake ya Utukufu itakuwa pale wakati wote. Hakutakuwa na usiku kule. Yesu, Jiwe la Kichwani!

194 Sasa angalia. Kwa hiyo, Waliokombolewa watatembea katika Nuru. Tunaimba sasa, "Tutatembea katika Nuru, hiyo Nuru nzuri." Kuna kitu fulani ndani yetu kinachoita. "Tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ni kwa sababu hilo linangojea. Mnaona? Hiyo ndiyo sifa yake, tunayojisikia.

Hakika, hii ni … Uko tayari? Huu ndio Mji ambao Ibrahimu alikuwa anautafuta. Mnaona? Akiwa nabii, alijua ya kwamba Mji huo ulikuwa mahali fulani. Biblia ilisema hivyo. Naye akauacha mji alioishi, akaenda kule; angalia mahali alipoenda, mahali pale pale hasa utakapokuwa. Mnaona? "Alikuwa akiutazamia Mji ambao Mwenye kuubuni na Kuujenga ni Mungu," mnaona, akiwa nabii.

195 Yesu alienda kuandaa, kwa mikono ya Kiungu, Mji wa Kiungu; Mjenzi hodari wa Kiungu, kwa ajili ya watu walionunuliwa na Mungu, kwa ajili ya watu waliochaguliwa tangu zamani. Ameenda kuandaa.

Ibrahimu alikuwa akiutazamia. "Naye akakiri ya kwamba alikuwa msafiri na mgani, kwa kuwa aliutazamia Mji ambao Mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu." Huyo nabii, akijua ilikuwa mahali fulani! Yohana aliuona ukishuka, bali Ibrahimu alifikiri hauna budi kuwa duniani wakati uo huo. Kwa nini? Yeye alikutana na Melkizedeki, Mfalme wake, na akampa fungu la kumi. "Ambaye hakuwa na baba, wala mama. Hakuwa na mwanzo wa uhai Wake wala mwisho wa uhai Wake." Ibrahimu alikutana Naye, nao wakafanya ushirika mahali pale pale hasa ambapo huo Mji utakapojengwa, ule Mlima Mtakatifu wa Bwana, ambapo Waliokombolewa wataishi. Loo, jamani!

Wakati huo haukomi. La, tuko katika wakati; baada ya kitambo kidogo tutaingia kwenye Umilele.

196 Loo, Mlima mtakatifu! Kutakuwako na barabara za dhahabu ya safi sana, barabara kuu; na nyumba, na maeneo ya kutembelea. Kama ukitaka kusoma hili, Ufunuo 21:18. Mti wa Uzima utakuwako; aina kumi na mbili za matunda, moja kila mwezi, yatazaliwa juu yake. Watu watakaokula matunda haya, watabadilisha mlo wao kila, kila mwezi.

Na ni—ni kutoka … kwa washindi tu. Mnajua jambo hilo? Si kwa ajili ya madhehebu.

Unasema, "Unamaanisha hivyo, Ndugu Branham?"

Hebu na tufungue Ufunuo 2, kwa dakika moja, na tuone hilo. Ufunuo 2:7. Hebu na tuone kama kweli

ni Kweli ama si Kweli. Ufunuo 2:7 inasomeka hivi.

*Na yeye aliye na sikio, na asikie yale Roho …*

Sasa, kumbukeni, Yeye hazungumzi na Wayahudi sasa. Hili ndilo Kanisa, Mataifa.

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa; Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.*

197 "Washindi tu, wanaomshinda yule mnyama, wanaoshinda alama yake," huo ni Ukatoliki, Uprotestanti, umadhehebu, "wanaomshinda yule mnyama, alama yake, herufi ya jina lake." "Yeye atakuwa na haki ya kuuendea huo Mti wa Uzima, kuingia katika milango ambapo hakuna kitu kinachotia unajisi kinachoweza kuingia kamwe." Mnaona? Wazia jambo hilo. Sasa, hebu kidogo tu sasa, tunapoendelea mbele kidogo. Mti wa Uzima utakuwa kwa ajili ya washindi tu.

Yale majani yatakuwa kwa ajili ya kuyaponya mataifa. Hiyo ni kusema, wafalme wanaoishi mle ndani, wakileta heshima zao ndani, watakapokuwa wanaleta heshima zao ndani na kuziweka mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu. Ni kama tu kule nje, yale kumi … yale makabila kumi na moja yalileta, kila mmoja wao, fungu la kumi kwa Lawi, mnaona. Wakati wanapoleta heshima zao kwenye … kutoka kwenye nchi iliyobarikiwa, katika hiyo, watanyosha mkono wao kwenye ule Mti wa Uzima, watavunja jani la mti … ama jani la Mti wa Uzima, nao watatoka watembea pamoja. Hakuna vita tena. Kila kitu kina amani. Majani hayo ni kumbukumbu, kwa ajili ya kuponywa kwa taifa.

198 Mti ule ule, si kama Adamu, yeye … Kulikuwako na Mti wa Uzima katika bustani ya Edeni, ambao angaliweza kula kama hakuanguka. Huo Mti wa Uzima ulimkumbusha, wakati wote, ya kwamba nini yake mpya … ujana wake ulikuwa unaendelea daima. Mnaona?

Vivyo hivyo na mataifa. Majani yatakuwa kwa ajili ya kuyaponya mataifa; angalia, si magonjwa sasa. Ungekuwa na haki zile zile ambazo Adamu alikuwa nazo, kama yule hu- … hua aliye na jani la mtini, yote ni … kila mfalme akichukua jani.

199 Angalia, ule Mto wa Uzima, labda ukifanywa na vijito vingi vidogo. Sasa, katika dunia hii …

Nitafunga katika dakika chache tu. Katika dunia hii … Ama, nitakoma tu. Hicho ndicho kiasi cha mihtasari niliyo nayo. Naam. Angalia.

Katika haya—katika maisha haya, sijaona kitu ambacho kinaondoa kiu sana kama kuwa milimani na kupata, kama nilivyohubiri hivi majuzi usiku, kijito hicho kikibubujika, nguvu zake zitaleta uzima. Ungekuwa mchovu na mwenye kiu, uanguke karibu na kijito kizuri; Huko chini kabisa ambako vijidudu haviwezi kwenda, huko chini kabisa futi mia kadhaa ndani ya ardhi, yanabubujika maji safi, halisi, yaletayo uzima. Tunathamini jambo hilo. Hilo ni dogo. Sasa, dunia ina vijito vyake vingi na maji ya yaburudishayo. Unapokuwa na kiu na unakufa, unapata maji mazuri, baridi kutoka mle, yata—yatakusaidia kuishi.

200 Lakini angalia mahali Haya yanakotokaa. Kutoka kwenye Kiti cha Enzi, hapo ndipo yanapopata nguvu zake ziletazo Uzima. Yanatoka chini ya Kiti cha Enzi cha Mungu, ambako Mungu anaketi.

Yote, dunia hii yote, dunia hii hapa tunamoishi sasa; kila mmoja, kama ni Mkristo au mpagani, ana mahekalu. Je! Ulipata kuwazia jambo hilo? Makanisa, yote.

Lakini Huyu hana cho chote. Biblia ilisema, "Wala hapakuwa na hekalu pale. Lakini Bwana Mungu na Mwana -Kondoo ndio Hekalu lake." Mwana -Kondoo ndiye Nuru. Mwana -Kondoo ndiye Hekalu. Mwana -Kondoo ndiye Kiti cha Enzi. Mwana -Kondoo ndiye Uzima. Yeye ndiye Hekalu hilo. Mnaona, mahekalu haya yote yana kitu wanachoabudu; bali, katika Mji huu, Yeye ndiye hicho kitu. Yeye yuko pamoja na watu Wake. Nuru ya Roho Yake huangaza Mji wa piramidi.

201 Kama vile Petro na Yohana, wakiwa kule juu ya mlima. Nuru ilifunika kilele cha mlima, na Sauti ikanena, ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa."

202 Katika Ufunuo 21:3 na 4, "Maskani ya Mungu iko pamoja na mwanadamu." Mungu amefanya maskani Yake katika mwanadamu, kwa kumkomboa, kwa hatua hizi tatu. Sasa Mungu anaenda kuikomboa nchi na kuiweka maskani duniani, pamoja na raia Wake wa duniani, ambao aliwatoa duniani. Na kwa dhambi ilianguka, lakini ninii … Ilimbidi kuiacha iendelee. Lakini sasa Yeye alimtuma Yesu kuikomboa ile dunia iliyoanguka, ambayo sisi ni sehemu yake. "Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaoangamia." Yesu alisema hivyo. Yeye alisema, "Nitaufufua tena katika siku ya mwisho." Mnaona? Kwa nini? Wewe ni sehemu ya dunia.

203 Mnaona, nilikuwa na mzaha mdogo kuhusu mke wangu akiniambia nilipoteza nywele zangu. Nikamwambia sikuwa nimepoteza hata moja.

Akasema, "Ziko wapi?"

Nikasema, ""Huko zilikokuwa kabla sijazipata." Kokote zilikokuwa, kitu halisi; po pote zilipo, zinaningojea. Mnaona? Hiyo ni kweli. Nitaenda ziliko, siku moja.

204 Mwili huu wa kale, ukikunja makunyanzi na kuanguka, na kupungua mabegani, na kuuma magotini, na—na umepwelewa na sauti kooni. Hilo ni sawa. Unaweza kuizika baharini, lakini Baragumu itaniamsha! …? … Naam, bwana. Tutabadilika, moja ya siku hizi. Mimi ni sehemu ya ulimwengu huu uliokombolewa. Uko ulimwenguni, bali huna cho chote cha kidunia. Uko katika utaratibu tofauti, uliokombolewa.

205 Angalia, "Maskani ya Mungu itakuwa pamoja na wanadamu." Angalia, "Mambo ya kwanza yamepita." Hiki, kitu hiki, kimepita. Hii inamaanisha kwamba Mbingu zimeshuka chini kukaa pamoja na mwanadamu. Mnaona? Mbingu na nchi zimekumbatiana.

Jinsi hasa yule Hua alivyokuja juu ya sehemu ya nchi, ambaye alikuwa ni Yesu; Yeye alikuwa mavumbi ya nchi, mwanadamu. Mungu, akitoka kwenye chembechembe hiyo ndogo ya Uzima, kwa nguvu za kuumba. Na hiyo Damu iliyokuwa kwenye ule … Ule uhai uliokuwa katika ile Damu ulipaa ukarudi kwa Mungu, bali ile Damu ilitiririka juu ya nchi, ipate kuidai. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara kadha — Mh.]

206 Kwa sababu ya damu iliyoletwa, kutoka kwenye chembechembe hai iliyotoka kwa Kaini, mnaona; sasa Yeye anarudi na nguvu za kuumba kama tu alivyomfanya Adamu, akimuumba Adamu, huyu hapa Adamu wa Pili. Na kupitia kule kuvunjika kwa chembechembe pale, ambapo (dhambi) Kaini aliivunja ile chembechembe ya damu juu ya yule mwenye haki, unaona, sasa Chembechembe hii ya Damu… Kwa sababu, alimwua Habili, bali Habili alizaliwa kwa kujuana kimwili.

Lakini Huyu hakuzaliwa kwa kujuana kimwili. "Ilikuwa ni kuumba kwa Mungu, mwanzo wake," nayo iliikomboa dunia. Na kasiamu yote, potasiamu, mafuta, mialimwengu, ulizofanyizwa kwazo, zimekombolewa. "Hakuna hata unywele mmoja utakaodhuriwa. Nami nitaufufua tena katika siku ya mwisho."

207 Basi nini? Mungu anashuka kuja kuishi duniani. Ambapo, Yeye ni sehemu yake, mwili Wake Mwenyewe. Yeye aliufufua kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, nasi tunahesabiwa haki kwa kuamini jambo hilo na kulikubali hilo. Angalia katika mifano, Yesu anakuwa … Katika mfano, Yesu anakuwa mwanadamu; Mungu … ama alichaguliwa tangu zamani kuchukua mahali pake, kutukomboa, kufanya mambo haya yote yawezekane.

Angalia, nje ya kuta zake zinazopendeza, za Mji huu.

208 Sasa mmeupata "ule Mji"? Mnaona, ni Mlima mtakatifu. [Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao — Mh.] "Hakuna kitakachodhuru wala kuharibu katika Mlima Wangu wote mtakatifu, asema Bwana." Mji huo si mchemraba. Ni Mlima. Na u—upana kwa urefu na kimo, ni sawa, mnaona; maili elfu na mia tano kwenda hivi, maili elfu na mia tano kwenda vile, maili elfu na mia tano kuzunguka kote; na maili elfu na mia tano kwenda juu. Kwa hiyo ni Mlima mkubwa tu, kama piramidi, na Mji huo upo Mlimani. Utukufu!

Hivyo ndivyo ilivyo, hizo hapo paradiso za Mungu, Nuru ya ulimwengu, ule Ufalme mkamilifu. Si siku ya saba; ile ya Milele! Mnaona? Si ule Utawala wa Miaka Elfu; Nchi Mpya! Mnaona?

209 Wakati inapopitia kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, inapitia kwenye hatua yake ya utakaswa, bali ingali bado haina budi kuteketezwa moto. Mnaona? Ambapo, ile Damu iliwakomboa watu, inaonyesha ukumbusho huu ya kwamba ni … gharama imelipwa, hiyo miaka elfu. Lakini basi haina budi kusafishwa kwa Moto; kama tu ilivyokuwa kwako wewe, wawakilishi Wake wa Mji huu, wale wawakilishi.

Kwa hiyo kama ukifa ama ukiishi, inaleta tofauti gani? Kama akija leo, ama akija miaka mia moja, ama miaka elfu, nitapumzika tu mpaka kubadilishwa kwangu kuje.

210 Kwa hiyo, mzee na mwanamke mzee, msife moyo. [Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao — Mh.] Kama wewe ni umewakilishwa hapa juu, katika sifa hii ya Mungu; huyu, Mungu; kama unayo, kama umewakilishwa hapa, huwezi … Uko katika Umilele. Na kama umevuka tangu siku hiyo ya saba, ukaingia kwenye ya nane, umeingia katika ya Milele kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, umehusishwa katika Hili. Sasa, kama umetumaini tu mhemko, ama kuruka-ruka, ama, "Ninafanya hili. Ninaitimiza siku yangu ya saba. Mimi sili nyama," na mambo kama hayo, ambayo yataangamia, hata hivyo. Mnaona? Lakini Hii ni ya Milele. Mnaona? HII ni ya Milele, ile Sikukuu baada ya sikukuu ya vibanda. Mnaona?

Sikukuu ya vibanda ilikuwa ni sikukuu ya mwisho, sikukuu ya saba. Sisi tunaabudu sasa chini ya sikukuu ya vibanda, wakati wa saba wa kanisa.

211 Katika ule Utawala wa Miaka Elfu, tutakuwa chini ya sikukuu ya vibanda, tena, katika siku ya saba.

Lakini, basi, baada ya siku ya saba, tuna Kusanyiko Takatifu, tutarudi katika Umilele. Vipi? Kwa njia

ya yule wa Milele aliyekuja na kutukomboa na kuturudisha, akituruhusu kutambua ya kwamba sisi tulikuwa sehemu ya Hili.

Sasa unajuaje wewe ni sehemu? Kwa sababu, hilo, Neno la wakati huu, ahadi ya siku hii. Ni kitu gani? Kurejeshwa nyuma kwenye siku ya kwanza, ya kwanza. "Naye ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao," kuleta kurejeshwa tena kwa kipentekoste halisi, si miamsho; Naye atadhihirisha ile Nuru ya jioni, Mwana yule yule aliyeonekana katika Nuru ya asubuhi, kama ilivyoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Amina na amina!

Tuko wapi, marafiki, tuko wapi? Tunangojea tu sasa kuondoka njiani, kusudi Ufunuo 11 iweze kuninii … ijulikane kwa Wayahudi; hiyo ni kweli, kule Kunyakuliwa kunakuja.

212 Angalieni, nje ya milango ya hizo kuta, yakiwa yamesambaa katika Nchi Mpya, mataifa yatakaa katika amani ya Milele. Sasa nini? Wafalme walioheshimiwa wataleta utukufu wao ndani yake. Hakuna dhambi inayoweza kuwapo kule. Hakuna wanawake waliokata nywele tena watakaoingia katika Mji huo. Nitawahakikishia hilo. Hakuna tena kuvaa kaptura, kuvuta sigara. Waasherati, makahaba, waongo, waabudu sanamu, cho chote walichokuwa, hawataingia Mji huo. La, yote yatakuwa yamekwisha. Dhambi itakuwa imeondoka. "Hakuna kitu cha kuunajisi utakatifu wake kitakachoingia mle." Hivyo ndivyo alivyosema. "Yote yamepita, milele."

Angalieni katika mashamba yake na kuzunguka malango yake;
Dubu atakuwa mpole, mbwa mwitu atakuwa mtulivu;
Na simba atalala pamoja na mwana -kondoo;
Na huyo mnyama kutoka mwituni, ataongozwa na mtoto mchanga;
Nitabadilishwa kutoka kiumbe nilicho mimi.

213 Huku mauti haya yakitenda kazi katika mwili wangu upatikanao na mauti, uzee ukiingia, nitabadilishwa.

Umeusikia wimbo huo? "Dubu atakuwa mpole. Mbwa mwitu atakuwa mpole." Yeye hataruka juu, na kuinuka na kujaribu kukuua. Yeye atatembea pamoja nawe njiani.

Ni nani atakayeirithi? Waliokombolewa. Itakuwa ni akina nani?

Angalia, ninaweza tu kufundisha kwa mifano sasa. Angalia, Ndugu Lee.

214 Ni nani aliyekuja kwenye nchi mpya pamoja na nabii Nuhu? Wale walioingia pamoja naye katika safina. Hiyo ni kweli? Hao ndio wanaotembea juu yake. Mnaona? Wale walioingia pamoja na Nuhu, kwa ujumbe wake, walikuwa ndio waliotembea juu ya nchi mpya baada ya ubatizo wake wa maji.

215 Wale wanaoingia pamoja na Yesu sasa. Unaingiaje ndani Yake? Kwa Roho mmoja; Naye ni Neno. Unakuwa sehemu Yake. Wewe ni sehemu Yake ipi? Neno linaloishi wakati huu, kutambua. Utatembea pamoja Naye katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Hapo ndipo utakapotoka ukatembee. Angalia, si kizazi kipya. Kupandikiza!

Unasema, "Loo, Ndugu Branham!" Loo!

Angalia, kama Mungu aliweza kumwinua Eliya na kumchukua juu, miaka elfu mbili na mia tano iliyopita, akampandikiza duniani tena, apate kuwa nabii kwa Wayahudi, ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza kumfanyia Bibi-arusi!

216 Baada ya Nuhu kutoka katika safina, angalia kile alichoambiwa Nuhu baada ya kutoka kwenye ile gharika, kama tu ilivyokuwa kwa Adamu hapo awali. Baada ya yeye kutoka, juu ya nchi mpya; kasema, "Zaeni mkaongezeke mkaijaze nchi," baada ya gharika. Angalia, "alikuwa aongezeke, akaijaze nchi," kama Adamu hapo kwanza.

Sasa unaweza kuona vizuri hapa. Sasa sikilizeni kwa makini sana.

217 Adamu alikuwa "aongezeke na akaijaze nchi." Hiyo ni kweli? Nuhu alikuwa, baada ya ile mpya, (ulimwengu kuangamizwa), alikuwa "aongezeke na akaijaze nchi." Mmelipata? Sasa hamwezi kuona "uzao" wa nyoka ni kitu gani? Ni kitu gani kilichoijaza nchi? Mnalipata? Vema. Mnaona jinsi Shetani alivyompata Hawa sasa. Hiyo ndiyo sababu mauti yametawala duniani tangu wakati huo. Na mbingu, nchi, mnyama, anga, vyote vimelaaniwa na Mungu kwa sababu yake. Hiyo ndiyo laana, kwa sababu Shetani alimfikia huyu kwanza.

Yesu alikuja kuikomboa airudishe kwa Baba. Ili kufanya jambo hili, Yeye alifanyika sehemu yake; kama nilivyoeleza hivi punde. Na kutokana na vumbi lilo hilo (ile sehemu aliyokuwa Yesu, Mwenyewe) ikikombolewa, kupitia Kwake sifa zote za Mungu zinakombolewa pamoja na dunia.

218 Yeye alikuwa Neno lililonenwa. Sisi tuliokombolewa ni sehemu Yake. Basi, kama unaweza kutambua!

Mnaona?

Mafarisayo walidai walikuwa. Lakini, mnaona kielelezo changu cha kwanza, walikuwa tu hao kwa akili. Wasingeweza kulitambua Neno wakati lilipodhihirishwa moja kwa moja mbele zao. Wakasema, "Mtu huyu ni pepo mchafu."

Sasa, leo, tunaitwa manabii wa uongo. Tunaitwa kila kitu kichafu tunachoweza kuitwa, na watu wa dini, unaona, na watu mashuhuri na wenye akili nyingi. Mnaona, hawafahamu tu. Mnaona?

219 Ubatizo wake wa maji haukutosha kuisafisha; wala wao kwa wao. Utakaso, wa ile Damu, uliirudisha, ukaidai. Lakini ubatizo wa Moto uliisafisha; kama ulivyomfanyia Bibi -arusi Wake. Kama vile kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

220 Hakuahidi kamwe kuinua jamii mpya, kama nilivyokwisha kusema, bali Yeye aliahidi kuwakomboa walioanguka. Hao ambao walikuwa wa—waliochaguliwa tangu zamani, watairithi kama Yeye alivyokwisha kuahidi. Naye ni Mungu asiyebadilika; tunajua jambo hilo.

221 Kumbukeni, Mungu alimchukua Eliya, baada ya kunyakuliwa, na kumhamisha, akampandikiza akamrudisha kwa watu, kuchukua nafasi kama nabii kati ya watu wake; hivi karibuni sana atafanya jambo hilo Na amemhifadhi, akiwa hai, miaka hii mia mbili na mia tano. Yeye atatokea tena.

222 Angalia tena, Yeye alimfufua Musa katika wafu. Kaburi lake liko wapi? Je, mtu ye yote anaweza kulipata? Soma Kitabu cha Yuda. Mnaona? Shetani … Yule Malaika Mkuu akibishana na yule malaika mkuu, Shetani, alisema, alithubutu … "Bwana na akukemee," akibishana juu ya mwili wa Musa. Na hapa Petro, Yakobo na Yohana walikuwa wamesimama pale wakimwangalia, kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura, papo hapo katika nchi ambayo Mlima huo utainuliwa upate kukaa ndani yake. Mnaona?

Naye akaja kuikomboa.

223 Mnaona, kulikuwako na Kanisa lililonyakuliwa wakati huo, lililowakilishwa; kulikuwako na wale waliolala, waliowakilishwa. Wapi? [Ndugu Branham anaonyesha kwenye ubao, kwa aya chache zifuatazo — Mh.] Mjini; kule juu ya mlima. Mnaona?

Kulikuwako na Petro, Yakobo, na Yohana, wakiangalia; tatu, shahidi. Kulikuweko na Eliya, Musa, na Yesu; kama shahidi wa Mbinguni. Mnaona?

Na kulikuwa na Musa, wafu, walikuwa wamefufuliwa. Kulikuwako na Eliya, kunyakuliwa, alikuwa angali hai. Na wote wawili waliwakilishwa kwenye mlima huu mtakatifu.

Na, Yesu, Mkombozi. Wakati Mungu, juu Yake namna hii, alipomfunika, alisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa."

224 Kumbukeni, Yesu alisema, yapata siku moja kabla ya wakati huo, alisema, "Amini nawaambieni, ya kwamba wengine wanaosimama hapa sasa, hawataona mauti, mpaka watakapouona Ufalme wa Mungu umesimamishwa katika nguvu."

Ilikuwa ni kitu gani? Wafu waliofufuka na watakatifu walionyakuliwa, pamoja, walinyakuliwa pamoja kumlaki Yeye hewani. Huku Mungu akimtia uvuli, na Yesu amesimama pale katika kivuli hiki, akisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa na Yeye," utaratibu wa ule Ufalme Mpya. Loo, ndugu, dada!

225 Mauti hayakubadilishi. Mauti hubadilisha tu makao yako. Mnaona?

Kumbuka, Samweli, wakati alipokuwa amekufa na kuzikwa kwa miaka miwili, alikuwa Paradiso. Ndipo yule mchawi wa Endori akamwita, naye Sauli akamtambua; na mwanamke huyo akamtambua, pia, akaanguka kifudifudi. Hakuwa amebadilika, hata kidogo. Alikuwa angali ni Samweli yule yule, baada ya kufa miaka miwili, naye alikuwa bado ni nabii. Akasema, "Kesho utaanguka vitani, mwanao pamoja nawe, na wakati kama huu kesho usiku utakuwa pamoja nami." Na hivyo ndivyo ilivyotukia.

Mnaona? Na wakati Musa atakaporudi, na Eliya, kwa Ufunuo 11, bado watakuwa manabii. Haleluya!

226 Na huko ng'ambo, katika ile Nchi, ule Mji ambamo Mwana -Kondoo ndiye Nuru, nitakujua, Ndugu McKinney. Nitawajua, enyi watu wangu, vito vyangu katika taji. Wanapokuja kutoka Mashariki na Magharibi, kwenye ule Mji; wakati maili elfu moja na mia tano mraba, atakuwa ameketi pale, na ule Mji uliojengwa mraba. Mtakapokuwa mmeketi kule kwenye ule Mlima mtakatifu, ambapo Mungu anaketi juu ya ule Mlima, na Yesu kwenye Kiti cha Enzi. Na ile baragumu ya dhahabu inalia wakati Yusufu anaondoka, na kutembea chini katika Paradiso, na watoto wa Mungu wanapiga magoti na kumwabudu Yeye, wakijua ya kwamba wao walikombolewa. Mnaona? Amina! Haleluya!

Wakati mwingine ninatamani Mbinguni,
Na utukufu nitakaouona kule;

Itakuwa furaha jinsi gani nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!
Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri
Aliouandaa Bwana …
[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

227 Isaya alisema, katika Isaya 9:6, "Na amani Yake na maongeo Yake hayatakuwa na mwisho. Uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake; Naye ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Na uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake; na maongeo Yake na amani Yake havina mwisho." Hata wanyama wapo kule. Loo, jamani!

Dubu atakuwa mpole, na mbwa mwitu atakuwa mtulivu;
Na simba atalala pamoja na mwana -kondoo,
Na huyo mnyama pori, ataongozwa na mtoto mchanga;
Lakini nitabadilishwa.

228 Nitabadilishwa kutoka kiumbe hiki nilicho mimi, Siku hiyo itakapokuja, kwa maana nitaenda kwenye Mji huo. Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri! Ninahisi Nguvu za ukombozi katika moyo wangu wote sasa.

Kama hivi sivyo ilivyo, basi nimepoteza maisha yangu; nimewafundisha wengine mambo ya udanganyifu. Lakini ninapotazama chini na kuona ya kwamba ile ahadi aliyoiweka ya siku hii, na kuiona Hiyo ikidhihirishwa; na kuangalia kusanyiko hili la maili elfu moja na mia tano mraba limeketi hapa, wateule ambao wameitwa kutoka katika madhehebu na jamii na kanuni za imani na kadhalika, wamekusanyika pamoja; huku nikiona Neno likijidhihirisha Lenyewe, ninajua, bila shaka hata kidogo, vito vya taji yangu vitang'aa kuliko kitu cho chote kile ulimwenguni, katika Siku ile.

229 Utafika wakati! Enyi watu, hatukusanyiki hapa bure. Tunangojea tu wakati huo. Muda umeenda sana, sana, bali Yesu yungali karibu, karibu sana. Na, Utukufu Wake, ni wa ajabu. "Jina Lake ataitwa Mshauri." Mji huo, mnaweza kuuona? Hapo ndipo Bibi -arusi na Bwana Arusi watakapokaa, na kamwe hawata nini …

230 Sasa, kama mnafikiri ni ajabu sana tunaposafiri mamia ya maili kuketi hapa na kulisha Neno Lake, ambalo hili ni kivuli tu, itakuwaje tutakapoishi huo Mji pamoja Naye! Ninapoishi jirani yako, na tutakapokula miti hiyo, nasi tutatembea katika barabara hizo, tutakapotembea kwenye barabara hizo za dhahabu hadi kwenye chemchemi, tunakunywa kutoka kwenye chemchemi, tunapoingia katika paradiso za Mungu, huku Malaika wanarukaruka wakiizunguka dunia, wakiimba nyimbo zasifa, loo, itakuwa ni Siku ya ajabu iliyoje! Inastahili kwa vyote. Barabara inaonekana ya kuparuza, wakati mwingine inakuwa ngumu, lakini, loo, itakuwa kitu kidogo sana nitakapomwona Yeye, kidogo sana. Vipi yale majina mabaya na mambo ambayo wao wamesema, hayo yatakuwa nini nitakapomwona Yeye katika Mji ule mzuri, mzuri sana wa Mungu?

231 Na tuinamishe vichwa vyetu.

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri
Bwana Wangu amewaandalia walio Wake;
Ambapo Wote Waliokombolewa wa nyakati zote Wataimba "Utukufu!" kuzunguka Kiti Cheupe cha Enzi.
Wakati mwingine ninatamani sana kwenda Mbinguni,
Na huko utukufu wake nitauona;
Itakuwa furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!

Kwenye kisiwa cha Patmo, Yohana aliona jambo hilo! [Ndugu Branham analia kwa furaha — Mh.]

232 Mpendwa Yesu, tumaini hili, tumaini langu halijajengwa juu ya cho chote kile, Bwana. Huo ni mama wa moyo wangu; ule Mji, yule Mfalme mkuu. Mungu, usiache mmoja hapa aangamie, tafadhali. Jalia tuyachunguze maisha yetu tena, leo, Bwana, tukingojea Kuja kwa Bwana. Ambapo, hao wote Waliokombolewa, huko ng'ambo katika uwanja huo mkubwa wa michezo huko Rumi, ambako hao Wakristo waliliwa na simba, mavumbi yatatokea siku moja!

Hakutakuwako na makaburi kwenye kilima cha Utukufu. Hakuna vitasa vya mlango vitakavyoshikilia shada la maua ya mazishi. Hakuna chozi litakaloanguka mle. La, la. Hakuna kichuguu cha udongo kitakacholundikwa mle. Hakuna tufani itakayoupiga. Yote yatakuwa na utukufu pale.

233 Tusaidie, Bwana. Kama kuna mmoja hapa … ambaye ameitwa kwenye Karamu hii ya Arusi ya Mwana -Kondoo, miaka hii elfu moja ya Utawala wa Miaka Elfu, na kisha kuingia Mjini baada ya Fungate kwisha. Ule utawala wa Miaka Elfu ni fungate tu. Ndipo Yeye, Bibi -arusi, anamchukua nanii Wake… Bwana arusi anamchukua Bibi -arusi Wake Nyumbani. Ni Wake. Bwana Arusi Wake; Bibi -arusi Wake. Loo, ameenda kuandaa Nyumba, kwa kuwa ameposwa.

Hebu tuwe waaminifu Kwake Yeye aliye Neno, kwa kuwa Yeye ni Neno. Haidhuru wengine wanajaribu

kutushambulia, tuweke mbali na Hilo; Bwana, nivute karibu zaidi.

Kwa maana wakati mwingine ninatamani Mbinguni,
Na utukufu wake Mimi Kule nitauona;
Itakuwa furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!

234 Makao ya baadaye ya Bwana Arusi na Bibi -arusi! Yeye anarudi … [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … Kwenye Karamu ya Arusi; itakuwa ni siku tatu na nusu. Halafu tutarudi tena, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwenye fungate yetu. Na halafu Yeye—Yeye atauonyesha wazi ule Mji. Kama bwana arusi anavyomshtusha bibi-arusi, jinsi maskini bibi-arusi huyo anavyosimama akiangalia makao yake ya baadaye kwa mshagao mkubwa! Na kwa imani, leo, Bwana, tunaiona huko ng'ambo. Itakuwa papa hapa duniani. Wewe uliahidi jambo hilo.

Kanisa lako litakombolewa kabisa, moja ya siku hizi. Na ndipo ulimwengu Wako utakombolewa, zile chembechembe zilizosalia. Lakini kwanza Wewe umewakomboa watu Wako, miili yao ambayo imefanyizwa kutokana na ulimwengu.

235 Tusaidie, Mungu. Kama kuna mmoja hapa ambaye hana hakika kabisa na jambo hilo, Bwana, jalia walipokee sasa hivi.

Ninajua imechukua muda mrefu na joto, lakini, enyi watu, hatutasimama hapa daima. Sitakuwa mchungaji wenu daima. Hebu na tulihakikishe.

"Kuna njia, Ndugu Branham?"

Naam, kuwa sehemu ya Neno, sehemu ya Neno la siku hizi. Huwezi kuwa sehemu ya Neno la siku za Musa; sehemu hiyo imekamilika tayari, hiyo ilikuwa ni miguu. Tuko kwenye Kichwa sasa. Huyu ni Kristo. Si ule wakati wa mikono, huko nyuma katika Luther, la. Huu ndio wakati wa Kichwa. Kristo, lile Jiwe la Kifuniko, anakuja kwa ule Mwili.

236 Kama hujisikii sawa kabisa kuhusu jambo hilo, po pote uwezapo, hebu inua mkono wako ili niweze kuona. Hebu kila mtu mwingine ainamishe kichwa chake. Mungu akubariki.

Sema, "Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham. Ninataka kuwa pale vibaya sana! Si—sitaki kulikosa, Ndugu Branham. Ni—ninaangalia, ninafanya kila niwezalo, lakini niombeeni sasa, mtafanya hivyo?" Mungu akubariki.

Unapofikiria jambo hilo sasa, omba tu, useme, "Mungu …" Liko moyoni mwako mwenyewe. Mnaona, kama unasikia kitu fulani kikivuta, kikiuwasha moyoni mwako, hicho ndicho. Ni sifa hiyo ikijaribu kujitangaza yenyewe.

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri
Bwana Wangu amewaandalia walio Wake;
Ambapo Wote Waliokombolewa wa nyakati zote
Wataimba "Utukufu!" kuzunguka Kiti Cheupe cha Enzi. Wakati mwingine ninatamani Mbinguni,
Na utukufu nitakaouona kule:
Itakuwa ni furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!

237 Baba wa Mbinguni, tuchukue sasa, Bwana. Jalia yule Mchungaji Mkuu, yule Mchungaji Mkuu Anayekomboa, yule Mchungaji Mkuu Ambaye aliacha Utukufu, akijua ya kwamba baadhi ya zile sifa zilikuwa zimepotea katika yale mambonde makubwa ya dhambi, ambako mbwa mwitu na wale—wale wanyama karibu wangemla maskini kondoo yule; bali Yeye aliacha zile kumbi za dhahabu, akashuka akaja duniani na akawa mmoja wetu, kusudi apate kuutangaza upendo wa Mugu kwetu. Pale akawakuta, baadhi yao wakiwa kwenye madhehebu, baadhi yao katika nyumba za malaya, baadhi yao mitaani, vipofu, baadhi yao kwenye vifungo na kwenye njia kuu, bali Yeye alimkomboa kila mmoja ambaye Baba alikuwa amemchagua Yeye amkomboe.

238 Naye alituagiza, kwamba tungeishi sehemu hii ya Neno kwa ajili ya nyakati zetu. Nasi tunaona yale matengenezo makuu ya Luther, katika wakati huo; na ya Wesley; na Wapentekoste. Sasa tunalitazamia lile Jiwe la Kifuniko cha ule Mji. Ee Mungu, tunajua wakati na ahadi tunayopewa kwa ajili ya siku hii, jinsi ambavyo Hili litarejeshwa tena. "Nuru ya jioni itaivisha tunda lake. Na itakuwa kwamba kutakuwako na siku ambayo haiwezi kuwa mchana wala usiku, itakayoitwa, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru."

Mwana yule yule wa Mungu mwenye utukufu, akijidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu hapa juu duniani, akiifanya ile ahadi iishi yenyewe kabisa, aliyapofusha macho ya Mafarisayo na Masadukayo na Maherodi, na kadhalika.

Na leo hii hilo jambo linajirudia tena, Neno likidhihirishwa tu kama lilivyokuwa. Neno, kujua siri za

moyo, kama tu vile ilivyokuwa hasa, kama Maandiko yalivyosema, ambayo hayawezi kutanguka. Tusaidie, Mungu, kutambua jambo hilo.

Wasaidie hawa sasa walioinua mikono yao. Jalia wakaze mshipi zaidi kidogo; wavae Injili ya Amani; wavae silaha zote za Mungu; washushe chapeo chini; wachukue ngao ya imani; waende mbele, tangu leo na kuendelea. Tujalie, Bwana.

239 Muda kidogo tu, tutaitwa, kisha Kunyakuliwa kutakuja. Kundi dogo tu, kama Henoko, litanyakuliwa.

Halafu, "wazao waliosalaia wa yule mwanamke, wazishikao amri za Mungu," Wayahudi, "wenye ushuhuda wa Yesu Kristo," Mataifa, watasakwa kama mbwa, "nao watatoa maisha yao kwa ajili ya ushuhuda wao."

Kisha, asubuhi moja kuu, kupambazuka kwa ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa ajili ya ile—ile fungate kutaanza.

"Na hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu." Ndipo, mwishoni mwa ile miaka elfu, kulikuwako na Hukumu, ikionesha kwamba Hamu alikuwa katika safina. Na Hamu angali yuko katika wale waliosalia. Wale waliolisikia na kulikataa itawabidi kuhukumiwa.

Sasa, tujalie, Bwana, kwamba tusihesabiwa miongoni mwao, bali tutaitwa kwenye ile Karamu ya Arusi. Kwa kuwa, tunamtambua Yesu miongoni mwetu leo. Tunaingia pamoja Naye; kutoka ulimwenguni, kuingia ndani Yake. Hebu na tutembee katika Mji huo, tutoke pamoja Naye.

240 Ninazeeka, Bwana. Sina mahubiri mengi zaidi ya kuhubiri. Lakini hakika ninakutumaini Wewe. Ninautazamia Mji huo, kama baba yangu Ibrahimu alivyofanya. Kuna Kitu fulani ndani yangu kinachoniambia unakuja. Ninajaribu kila mahali, Bwana, kueneza Nuru na kuwaita. Jalia hata mmoja wa hawa, Bwana …

Jinsi ilivyo vizuri, muda mfupi uliopita, ulinifunulia jambo hilo. Kutoka kwenye mzingo wa kama maili elfu moja mia tano, moja tu hapa na pale, wamewekwa pamoja leo, waliokusanyika kwenye sehemu moja ndogo, wakingojea Mji huo kuonekana. Tunakiri ya kwamba sisi ni wasafiri na wageni. Sisi ni waliotupwa. Makafiri, ulimwengu, unacheka na kufanya dhihaka; madhehebu ya kidini yanadhihaki; bali hatutikiswi na mambo kama hayo. Tufanye sehemu ya Neno, Bwana, wasiotikisika. "Itakuwa katika siku za mwisho." Jalia iwe sisi, Bwana, jalia tuhesabiwe miongoni mwao. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Hebu na tuinue mikono yetu namna hii.

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri
Bwana Wangu ameuandaa kwa ajili ya walio Wake;
Wakati wote Waliokombolewa wa nyakati zote
Wataimba "Utukufu!" kuzunguka Kiti Cheupe cha Enzi.
Wakati mwingine ninatamani Mbinguni,
Na utukufu wake nitakaouona kule;
Loo, itakuwa ni furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!

241 Sasa, kama inatupasa kuishi katika Mji huo pamoja, peana tu mikono na mtu fulani, tuseme, "Mungu akubariki, msafiri. Umetoka wapi? Louisiana, Georgia, Mississippi? Mimi ni msafiri, pia. Ninautazamia Mji huo."

Ninautazamia Mji huo, Ndugu Neville, kule. Tunaenda kule …?… Ndugu Capps, mimi bado ninautazamia Mji huo, usiku wa leo. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha Hakuna Kukatishwa tamaa — Mh.]

Na utukufu wake nitakaouona kule:
Itakuwa furaha itakuwa furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!
Loo, dubu atakuwa mpole, na mbwa mwitu atakuwa mtulivu;
Na simba atalala karibu na mwana -kondoo, loo, naam;
Na mnyama pori kutoka … ataongozwa na mtoto mchanga;
Nami nitabadilishwa, kubadilishwa kutoka kiumbe hiki nilicho mimi, loo, naam.
Loo, kutakuwa na amani bondeni kwa ajili yangu siku moja;
Loo, kutakuwa na amani bondeni kwa ajili yangu. (Sawa! Naam!)
Hakutakuwako na huzuni tena, hakuna majonzi tena, sitaona shida tena;
Na kutakuwa na amani bondeni kwa ajili yangu.

242 Mfalme wetu asiyeonekana, asubuhi ya leo, atadhihirishwa. Nami sitamwona Bill Dauch kwenye umri wa miaka tisini. Hutaniangalia mimi kwenye umri wa miaka hamsini. Lakini nitabadilishwa, Siku hiyo.

Na wakati mnyama kutoka porini, ataongozwa na mtoto;
Lakini nitabadilishwa, kubadilishwa kutoka kiumbe hiki nilicho mimi.

243 Mbona usifurahi? Nywele zenye mvi zitaondoka; mabega yaliyoinama. Lakini uzuri, usiopatikana na mauti, utasimama katika mfano Wake, jua lipate kuangaza. Loo, ajabu!

… Kwa ajili yangu, Ee Bwana, naomba;
Hakutakuwako na majonzi, hakuna huzuni tena, hakuna shida tena nitakayoiona;
Na kutakuwa na amani bondeni kwa ajili yangu.

244 Hilo ndilo lililotuleta hapa. Ni wangapi wenu wanaohitaji nguvu kwa ajili ya safari? Mungu na atujalie! Ni wangapi wenu walio wagonjwa miilini mwenu, askari waliojeruhiwa? Dazeni, ama zaidi. Unaamini Yeye yupo hapa, Mfalme asiyeonekana? Mambo vinavyoonekana; visivyoonekana vinadhihirishwa na vinavyoonekana. Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ni mwili tu. Sasa, kama huyu ni Roho Wake ambaye amehubiri hili kupitia kwangu, Yeye atafanya kazi alizofanya wakati alipokuwa hapa. Loo, ni ajabu iliyoje!

Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi,
Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi;
Loo, ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?
Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi.
Kote kwenye nyanda hizo pana
Inanga'aa Siku moja ya Milele;
Hako Mungu Mwana anatawala milele,
Na kuutawanya usiku.
Loo, ninaelekea kwenye nchi ya ahadi,
Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi;
Loo, ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?
Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi.

245 Watu mia tano wakienda mtoni kule, siku ya kwanza ambapo yule Malaika wa Bwana alipoonekana kwa macho, kuthibitisha, kama alivyofanya kwenye Mlima Sinai, ya kwamba nilikuwa nimekutana Naye. Nilitembea kuingia mtoni, na mamia wakiimba wimbo uo huo kwa ajili ya ubatizo. Huyu hapa anakuja, akishuka, Nguzo ile ile ya Moto mnayoiona kwenye picha pale; ikishuka chini, papa hapa mtoni, na kusema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza, Ujumbe huu utakutangulia Kuja kwa pili." Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo, mnaona.

Loo, ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?
Ninaelekea kwenye nchi ya ahadi.

246 Nguzo ile ile ya Moto iko hapa pamoja nasi. Je! Mnatambua hilo? Yeye amewafanya wengine wetu kwa ajili ya kitu kimoja, na wengine kingine. Kama utaamini, bila shaka moja, kuamini kwamba Yeye yuko katikati ya jengo, ninaamini atajithibitisha Mwenyewe kwenu. Je! Itawaridhisha? Kama sitamfikia kila mmoja … Inaelekea saa nane, lakini kama … Ni kidogo imepita saa saba, hasa. Kama mtaamini, hebu Yeye ashuke juu yetu! Imani yetu iko wapi? Mnaona, huna budi kuamini jambo hilo. Kama hutalitilia shaka, hata kidogo, litatenda kazi.

Ni—ninautambua Uwepo wa Kiungu wa Utu wa Kristo, Ambaye ni Neno. Nayo Biblia ilisema, "Neno ni… lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, nalo linakata viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, na hutambua mawaza yaliyo— yaliyo moyoni, likifunua siri ya moyo."

247 Angalia. Mbona, sikujua mambo hayo, miaka kadhaa iliyopita. Na wakati niliposema jambo hilo, bila kulijua, angalieni jambo Yeye alilofanya. Yeye alisema, "Sasa utawashika watu mkono wao, na, usiwaze lo lote, sema tu sifa utakayoambiwa. Useme ni uvimbe, cho chote kile." Kisha akasema, "Itakuja kutokea ya kwamba haitakubidi kufanya jambo hilo." Mnaona? Mnaona? "Itatambua kitu kile hasa kilicho ndani yao." Tuna kila aina ya miigo, tunajua jambo hilo, karibu iwapoteze walio Wateule kama yamkini. Angalia jinsi jambo hilo lingine linavyoambatana na Neno, ndipo utajua kama ni kweli ama si kweli. Lakini, hata hivyo, Yesu anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.

248 Ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa, na wanajua siwajui? Inua mkono wako, useme, "Na—najua hunifahamu." Loo, ni ninii tu, nadhani, kila mahali. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuliamini tu.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

249 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa juu ya nchi katika siku ya mwisho. Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa, ama, atakapojifunua Mwenyewe katika siku ya mwisho." Sasa, si siku za zamani, siku za katikati; siku ya mwisho, unaona, Yeye angefunua. Na sasa tuko katika siku za mwisho. Sodoma inakaa vile vile kabisa, kila kitu, wale wajumbe, sawa tu.

Ilikuwaje kwa—kwa wale wachache waliosalia walioitwa watoke pamoja na kundi la Ibrahimu?

Kulikuwako na Mmoja aliyekuja miongoni mwao, katika mwili wa kibinadamu; awakilishwa katika mwili wa kibinadamu, kula pamoja nao, kunywa pamoja nao, chakula kile kile wanachokula, kila kitu. Yeye alisimama miongoni mwao, akawaambia Ujumbe. Ndipo akasema, "Nitafanya jambo hili kuu."

250 Naye Ibrahimu akaendelea kuchunguza, " Huyu ndiye? Nimekuwa nikiutazamia Mji. Huyu ndiye Mfalme?"

Naye akasema, "Kwa nini Sara alishuku jambo hili?" Katika hema, nyuma Yake.

Ibrahimu akasema, "Bwana Mungu, Elohimu!" Maana, Yeye alitambua mawazo ya Sara.

Yesu alisema ingejirudia tena wakati Yeye angefunuliwa katika siku ya mwisho, lile Jiwe la Kifuniko likija kwenye ule Mwili. Kuwakomboa ninii … Hao ni wale waliokombolewa, akija kuwachukua walio Wake. Yeye yuko hapa pamoja nasi.

251 Sasa, kuna kama tu dazani moja ya mikono, ama zaidi, iliyoinuliwa. Ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kumponya kila mmoja wenu. Kweli. Ninaamini ndivyo mlivyo. Siamini ya kwamba mtu kweli angeweza kukaa mahali kama hapa bila … katika wakati wa namna hii, na hali namna hii, bila kujua, kutambua kitu fulani.

Ninawatakeni muombe. Ninawataka mwombe. Ninataka mjue shida yenu, katika— katika—moyo wenu, unaona, kisha uanze kuomba, useme, "Bwana Yesu, nifunulie jambo hili. Mimi—ninakuzungumzia Wewe shida yangu. Na sasa Wewe mtume Roho Wako Mtakatifu kwa Ndugu Branham, kutimiza yale aliyosema kuwa ni Kweli, katika Ujumbe huu ambao ameuzungumzia leo kukuhusu Wewe, najua utakuwa ni Kweli. Sasa, nifunulie hilo, Bwana. Nena nami."

252 Sasa limetawanyika, kwa namna fulani hapa na kila mahali. Kwa hiyo omba tu, na uamini tu kwa moyo wako wote, ya kwamba Mungu atakujalia.

Sasa ninawatakeni mniangalie, na kuomba. Kama tu vile Petro na Yohana walivyosema, "Tutazame sisi." Alitaka kitu fulani, naye yuko karibu tu kukipokea. Nawe unataka kitu fulani, nami ninaamini uko karibu tu kukipokea. Akasema, "Tutazame sisi."

Akasema, "Fedha na dhahabu, sina kitu; lakini nilicho nacho, nitakupa."

Sasa, uponyaji, sina wo wote. Huo wote ni katika Kristo. Lakini nilicho nacho, karama ya Mungu, ninakupa wewe, imani ya kumwamini Yeye. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wenu aponywe. Amini hilo. Mnaona? "Kama mnaweza kuamini!"

253 Yule mama anayeketi pale, akiniangalia. Alikuwa analia, dakika chache zilizopita, akiomba. Ana shida ya goita inayomsumbua. Mimi sikujui. Wewe ni mgeni kwangu. Hiyo ni kweli, sivyo. [Huyo dada anasema, "Hiyo ni kweli." - Mh.] Wewe hutoki hapa. Umetoka Chicago. Bibi Alexander. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako. Sasa rudi Chicago ukawe mzima.

Aligusa nini? Kitu kile kile yule mwanamke aliyekuwa na kutokwa na damu alichogusa, upindo wa vazi Lake, si wangu.

Huyu hapa maskini mama anayeketi moja kwa moja miongoni mwa umati, kama ninaweza kumfanya anielewe mimi. Wewe uliyeinua kichwa chako upande. Mimi sikujui. Wewe ni mgeni kwangu, bali una ugonjwa wa tumbo. Mume wako anaketi karibu nawe. Ana kasoro fulani kwenye sikio lake. Jina lako ni Czap. Siwajui. Hamtoki hapa. Mmetokea Michigan. Kama hiyo ni kweli, pungeni mikono yenu. Rudini Michigan, wazima. Imani yenu inawaponya. "Kama ukiweza kuamini, yote yanawezekana."

254 Bibi mdogo pale mwenye ugonjwa wa koo, ameketi papa hapa nyuma, kutoka Georgia, amevaa nguo nyeupe. Rudi, chini Georgia, ukiwa mzima. Yesu Kristo anakuponya. Unaamini jambo hilo?

Bibi anayeketi pale, akiniangalia, moja kwa moja mwishoni mwa kiti. Alipata shida ya nyama za puani. Ataamini, Mungu atamponya. Bibi Brown, amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atafanya … Wewe ni mgeni kwangu, bali Yeye anakujua. A-ha. Unaamini jambo hilo? Inua mkono wako. Hiyo ni kweli.

Anayeketi hapa kwenye haya machela. Mwambie aangalie hapa. Amekuwa akiteseka, akiendelea. Kama ningeweza kumponya, ningefanya hivyo, bwana. Siwezi kuponya. Yeye hatoki hapa; kuja toka mbali. Umetoka Missouri. Shida zako ni za ndani. Lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, wala usione shaka, Yesu Kristo anaweza kukuponya; nawe unaweza kurudi Missouri, ukiwa mzima, na kutoa ushuhuda wako. Unaamini jambo hilo? Basi likubali, na uchukue kitanda chako uende nyumbani. Yesu Kristo anakuponya.

255 Unaamini? Huo ni utambulisho wa Uwepo wa Mfalme wa Milele. Je! Unaamini jambo hilo sasa, kwa moyo wako wote? Sasa, hakika Yeye amefanya duara, moja kwa moja kwenye jengo hili. Je! Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini uko katika Uwepo Wake?

Sasa, unaamini na kukubali ya kwamba wewe ni mmoja wa ujumbe wa Ufalme huu? Inua mkono wako. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sisi ni sisi kwa sisi; wewe ni sehemu yangu, mimi ni sehemu yako; sisi sote ni sehemu ya Kristo. Sasa, pamoja, hebu na tuwekeane mikono.

Papa hapa, yule mwanamke kwenye kitanda amesimama, akitembea huku na huko, akirudi nyumbani apate afya. Amina.

256 Ninyi, kila mmoja, ameponywa, kama mtaamini. Sasa wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine, nanyi ni sehemu hii ya Kristo. Unamwombea mtu uliyemwekea mikono, jinsi tu unavyotaka.

Bwana Yesu, tunakutambua hapa. Wewe ni Mfalme wetu; Unajitambulisha Mwenyewe miongoni mwetu. Tunakushukuru kwa ajili ya Uwepo huu. Na, Bwana, Wewe ulisema, "Mkiuambia mlima huu, 'Ng' oka,' usitilie shaka; amini uliyosema litatimia, linaweza kuwa lako, linaweza kuwa lako lile ulilosema."

Halafu, katika kutii amri hii, katika kutii Neno la Mungu ambalo haliwezi kushindwa, sisi kama wajumbe Wako kutoka maili elfu na mia tano mraba, kama ule Mji, tunamwambia Shetani, ibilisi aliyeshindwa, "Mwisho wako ni kuchomwa moto. Sisi ni ujumbe kutoka kwenye Mji ule wenye mraba, ule Mji ambapo Mwana -Kondoo ndiye Nuru. Sisi ni sifa zilizotamkwa za Mungu Mwenyezi, ambao Yesu Kristo amewakomboa kwa neema Yake."

Shetani, toka nje, na umwache kila mgonjwa aliye humu ndani, katika Jina la Yesu Kristo. Mikono mitakatifu ambayo imekombolewa, kwa sababu wanaamini Neno na wao ni sifa za wazo la Mungu, sasa hiyo mikono imewekwa juu ya kila mmoja. Huwezi kuwashikilia tena. Toka, katika Jina la Yesu Kristo!

257 Sasa, katika Jina la Bwana Yesu, sasa, Yeye yuko hapa. Neno Lake linasema Yeye yuko hapa. Uwepo wako na imani yako hunena, kuhusu, wewe ni mmoja wa wajumbe. Hata kila kipimo cha kijiografia ambacho tunaweza kuonyesha, ndivyo ilivyo. Mnaweza kutambua ya kwamba ninyi ni wana na binti wa Mungu waliokombolewa? Mnatambua huku ndiko Nyumbani kwenu? Huku ndiko mnakoenda.

Hiyo ndiyo sababu mmekuja hapa, hiyo ndiyo sababu mmemjia Kristo, mnakula Neno Lake. Na kama mnaweza kuwa na wakati kama huu, hapa, kwa sifa Zake tu zilizotamkwa, itakuwaje tutakapokuja katika Uwepo Wake? Loo, litafurahisha sana! Kila mmoja wenu ana haki ya kuwaponya wagonjwa, kuweka mikono yenu juu ya wagonjwa. Kila mmoja wenu ana haki ya kubatiza.

258 Kama kuna mtu hapa ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kidimbwi kiko wazi.

Hivyo ndivyo tu pekee utakavyofanya, a-ha, hiyo ni kweli, ni kutii kila Neno. Kumbuka, sehemu moja ndogo ya Neno, hapo mwanzo, ilisababisha kila dhambi duniani. Yesu alisema, "Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hili, ama kuongeza neno moja Kwake, hataingia." Jina lake limeondolewa kwenye Kitabu, mara anapolifanya.

Na hakuna mahali katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa, Kanisani, vinginevyo ila katika Jina la Yesu Kristo. Kama hujabatizwa namna hiyo, afadhali ufanye hivyo.

"Loo," unasema, "haileti tofauti yoyote." Ilileta kwa Hawa.

Shetani akasema, "Loo, hakika, Mungu, unamjua Mungu …" Lakini, Yeye alifanya hivyo. Yeye alisema hivyo.

259 Yeye alimpa Petro funguo za Ufalme, na kile kilichofungwa kwenye Pentekoste kimefungwa milele. Hiyo ndiyo sababu Bibi-arusi aliingia kwenye onyesho la awali, mara ya pili; hapana budi kuwe na Kanisa litakaloitwa kutoka katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku ya kwanza, hasa kabisa. Mti umechipua kutoka kwenye mizizi yake, hadi kwenye Mti wa Bibi -arusi, kama ulivyofanya katika wakati huo; Kipeo cha Mungu tena, kama nilivyosema Jumapili mbili zilizopita, kupelekwa Mjini.

Mungu akubariki. "Sasa naamini."

260 Shetani ameshindwa. Yeye anajua. Yeye yuko duniani, anatembea kama simba angurumaye. Haitachukua muda mrefu kufikia atakapokwisha kabisa, amekwisha Yeye anajua wakati wake. Yeye anatembea kama simba angurumaye.

Lakini, kumbukeni, Mfalme wa Amani anasimama karibu; Yule Mkuu wa Kiungu. Msanifu wa utu wangu, Msanifu Ambaye alinijenga nilivyo mimi, aliyekujenga ulivyo wewe, yuko hapa. Kama Msanifu Majengo, Ambaye anajua jinsi ya kuweka jengo pamoja, mahali pake panapofaa, ni nani ajuaye vema kuliko Msanifu Majengo? Naye yuko hapa kujithibitisha, Mwenyewe, yuko hapa.

Sasa inategemea imani yako. Amini, amini tu! A-ha.

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri
Bwana Wangu amewaandalia walio Wake;

Ambapo Wote Waliokombolewa wa nyakati zote
Wataimba "Utukufu!" kuzunguka Kiti Cheupe cha Enzi.
Wakati mwingine ninatamani Mbinguni, (wakati haya yote yamekwisha),
Na utukufu ule nitakaouona kule;
Itakuwa furaha iliyoje nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!

261 Kumbukeni, kanisani, usiku wa leo, watakuwa wakifanya ushirika. Kama uko hapa mjini, hata hivyo, ungetaka kuja, tungependa kuwa nawe. Ni kumbukumbu ya kile tutakachokula, moja ya siku hizi, pamoja Naye.

Ninawapenda. Sijui jinsi ya kulielezea. Nafikiri ninyi ni chumvi ya dunia. Nami nasikia mwenendo wenu miongoni mwa ulimwengu, basi hilo linanipa kujiamini zaidi kwenu.

Lakini, wazia, kundi hili dogo litakuwa, kama sisi tulivyo, litavunjika, moja ya siku hizi. Tutaota jambo hili. Lakini kama ikitokea mmoja wetu aage dunia kabla hatujakutana tena, tutaninii …

Nitakulaki asubuhi, upande mwangavu wa mto
Wakati huzuni zote zimekwisha ondoka;
Nitakuwa nimesimama karibu na lile lango, wakati milango itakapofunguliwa,
Mwishoni mwa siku ndefu na yenye kuchosha ya maisha.
Nitakutana nawe asubuhi, karibu na mto mwangavu,
Mimi mara nyingi…?…kule chini karibu na mto, na pamoja na unyakuo, kwa furaha tutafanya upya urafiki wetu, (nitawaona wakati huo, nitawajua)
Mtanijua kwenye ile asubuhi, kwa tabasamu nitakalokuwa nalo,
Nitakutana nanyi asubuhi, kwenye ule Mji, Mji ambao umejengwa mraba.

262 Mnaupenda? "Hata twonane!" Sasa hebu na tusimame. Peleka Jina la Yesu, tupe sauti.

Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."] Mnaamini hii ni Kweli? ["Amina."] Je! Unaelekea huko, kwa neema ya Mungu? ["Amina."] Mpaka tutakapofika kule:

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao toka kwa kila mtego;
Utakapojaribiwa,
Pumua tu Jina hilo takatifu katika maombi.

Hilo tu ndilo la kufanya, mpaka tutakapowaona tena. Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na …

[Mtu fulani anasema, "Usiku wa leo?" - Mh.] La.

Litafurahisha moyo,
Peleka jina hilo popote uendako.
Jina la thamani, Lo, ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

263 Sasa, ilinibidi kuruka Ujumbe wangu. Siku moja, Bwana akipenda, nitarudi na kuchukua "hii milango," na kuichukua, mnaona, ambapo tunaweza kuwa na wakati zaidi. Mmekuwa mkipiga makelele kuhusu kutokaa muda mrefu vya kutosha. Tumekaa, leo. Kuna joto. Lakini, sasa, Mungu awabariki. Ninapenda uimbaji huo.

Jirani fulani hapa, alisema, hivi majuzi walipozima spika za nje, kasema, "Nilifurahia huo Ujumbe sana, lakini kwa nini mlikatiza huko kuimba kuzuri, mnaona, huko nje?" Kwa hiyo, jirani, kama unasikiliza asubuhi ya leo, nafikiri tuna majirani bora sana waliopo Jeffersonville. Tunaegesha magari yetu mbele ya nyumba zao na cho chote kile; hawasemi neno juu yake; tunaendelea tu. Kwa hiyo, tunawashukuru sasa.

Loo, jinsi Yeye alivyo wa ajabu! Mungu awe pamoja nanyi sasa.

… Jina, Lo ni tamu ilioje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Mpaka tutakapokutana …

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Mchungaji atatutawanya, katika dakika chache tu. Mungu awe pamoja nanyi!

… Tunakutana miguuni pa Yesu, (kwenye ule Mji mkuu, kwenye Kiti cha Enzi),
Hata tuonane! Hata tuonane!
Mungu awe nanyi hata tuonane.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7